# SUALA LA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI KATIKA HADITHI FUPI TEULE ZA KISWAHILI

**JOYCE KARIMI**

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Kishirikishi Cha Tharaka**

**CHUO KIKUU KISHIRIKISHI CHA THARAKA**

**DISEMBA 2021**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo la Mwanafunzi**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuandikwa wala kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine .

Sahihi........................................................ Tarehe 3/12/2021

Joyce Karimi
AM12/29221/17

**Idhini ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu Kishirikishi cha Tharaka.

Sahihi........................................................ Tarehe 3/12/2021

Dkt. Timothy Kinoti M'Ngaruthi
Idara ya Fani
Chuo Kikuu cha Embu

Sahihi........................................................ Tarehe 3/12/2021

Dkt. Allan Mugambi
Idara ya Fani
Chuo Kikuu cha Chuka

**HATILINZI**

©2021

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kupiga chapa, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Kishirikishi cha Tharaka.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa Mariamu Kang'aria kwa kujitolea bila kuchoka kunilea na kunielimisha licha ya changamoto kadha za maisha. Kwa wanangu Brillian, Favour na Baraka kwa mapenzi yao na kuwa nguzo muhimu katika maisha yangu.

# SHUKRANI

Kwanza ni shukrani kwa baba yangu wa mbinguni kwa neema, kibali, hekima na kunipa afya njema katika kuianza na kuiendeleza safari hii hadi mwisho wake. Shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu ambao pia ni wahadhiri wangu katika kiwango hiki Dkt. Timothy Kinoti na Dkt. Allan Mugambi kwa msaada wao wa kuhakikisha kazi hii imefika kiwango hiki na kwa kujitolea kutufundisha katika kiwango cha uzamili. Ushauri na uelekezi wao ni wa kupigiwa mfano. Mola awabariki sana. Kwa njia ya kipekee nashukuru usimamizi wa Chuo Kikuu Kishirikishi cha Tharaka kwa kunitia motisha na kufadhili utafiti wangu kifedha. Mungu akibariki chuo hiki. Pia, nawashukuru: Dkt. David Kiptui, Bi. Evah Ng'unjiri, Bw. Kimathi Muembu, Bw. James Ndwiga, Bi. Doris Gatuura kwa mchango wao katika masomo na utafiti wangu. Mlinitia moyo na kunifanya kutia bidii zaidi na kuifurahia kazi yangu. Siwezi kumsahau Bw. Josphat Kimathi ambaye alinishauri kuendeleza masomo yangu katika kiwango hiki. Mungu awatende mema.

Shukrani zingine kwa mama yangu mpendwa Mariamu kwa ushauri wa kila mara na upendo wake wa dhati. Mchango wako katika kazi hii hauwezi kulipika. Mungu akupe maisha mema na marefu. Sitamsahau mume wangu Patrick Munene kwa mchango wake katika safari hii. Kwa wanangu Brillian, Favour na Baraka, licha ya umri wenu mdogo mlinipa utulivu wa kutosha katika kuiandaa kazi hii. Ninawapenda sana.

Dada zangu Salome na Virginia, Mungu awe nanyi siku zote. Upendo wenu kwangu ni wa maana. Asante kwa mchango wenu katika maisha haya. Mwisho kabisa, nawashukuru wanafunzi wenzangu na marafiki na wote walionitia moyo katika safari hii. Nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu.

# IKISIRI

Dhima ya fasihi ya Kiswahili katika ulimwengu wa leo haiwezi kupuuzwa kamwe. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii cha kutazamia mambo mbalimbali yanayofanyika katika jamii pana. Fasihi inaweza kutumiwa kusifu au kukashifu jambo fulani katika jamii. Utafiti huu ulichunguza suala nyeti linaloangazia ukiukaji wa haki za watoto na kuathiri watoto wengi wenye umri wa shule. Suala hili ni uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Kazi zilizohakikiwa ni; Hadithi fupi teule katika diwani za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Utafiti huu ulikusudia kubaini chanzo, athari na suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa; kubainisha visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili, kutathmini athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili na kujadili falsafa ya waandishi wa kazi teule za Kiswahili kuhusu suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ambayo hunuia kubainisha na kufafanua kadhia zinazomkutanisha msomaji na kazi ya fasihi na kumpa msomaji uhuru wa kufasiri kazi ya fasihi apendavyo. Waasisi na watetezi wakuu wa nadharia hii ni pamoja na: Wolfgang Iser (1974,1978), Stanley Fish (1980) na James Tompkins (1980). Data ya utafiti huu ilitokana na kusoma hadithi fupi teule za Kiswahili na kuzichanganua kimaelezo kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Mtafiti alisoma hadithi fupi teule kwa kina na kubaini maneno na mafungu ya maneno yaliyohusiana na suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Mtafiti alichunguza visababishi, athari na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama yanavyofafanuliwa na wasanii wa kazi teule. Utafiti huu utatoa mchango katika taaluma ya fasihi kwa kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa fasihi ya Kiswahili katika jamii ukiwemo kuyamulika yanayotendeka kwenye jamii na kutafuta suluhu kwa matatizo ya kijamii. Vilevile, waandishi wa fasihi watanufaika na utafiti huu kwa kuwawezesha kutambua masuala ibuka na masuala nyeti katika jamii. Pia, utafiti huu unatoa mchango kwa watetezi wa haki za watoto kuhusu mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuangazia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni nchini Kenya na kwingineko.

## ABSTRACT

The role of Kiswahili literature in the contemporary world cannot be underestimated. This is because literature is a mirror to the society that portrays various issues that take place in the wider society. Literature can be used to praise or condemn an act in the community. This research focused on a trending issue that violates children's rights hence affecting children of school going age. The researcher focused on premature relationships and teenage pregnancies as depicted in selected Kiswahili literary works, that is; Selected short stories in *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007) and *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). This research evaluated the causes, effects and solutions to premature relationships and teenage pregnancies among children with reference to the selected Kiswahili literary works. The objectives of this research were; to evaluate the causes of premature relationships and teenage pregnancies with reference to the selected literary texts, to evaluate the effects of premature relationships and teenage pregnancies with reference to the chosen Kiswahili literary work and to discuss the philosophy of the writers of the selected literary works concerning the solution to premature relationships and teenage pregnancies. This research was guided by Reader's Response Theory that aims at identifying and explaining occurences that makes a reader interact with a certain literary work. The main founders of this theory include; Wolfgang Iser (1974,1978), Stanley Fish (1980) and James Tompkins (1980). The research data was collected through reading the selected Kiswahili literary works and analysing it through explanations guided by the objectives of the research. The researcher read all the selected stories and extracted words and texts about premature relationships and teenage pregnancies. The researcher looked at the causes of premature relationships and teenage pregnancies, effects of premature relationships and teenage pregnancies and solutions to premature relationships and teenage pregnancies.The findings of this research will benefit the literary field by informing the masses on the importance of Kiswahili literature to the society. It will as well benefit literary writers by informing them on the emerging issues and trending issues in the society. The research will also benefit the people concerned with children's rights on the importance of Kiswahili literature in dealing with the issue of premature relationships and teenage pregnancies in Kenya and the rest of the world.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** ....... ii

**HATILINZI** ....... iii

**TABARUKU** ....... iv

**SHUKRANI** ....... v

**IKISIRI** ....... vi

**ABSTRACT** ....... vii

**YALIYOMO** ....... viii

**ORODHA YA AKRONIMU** ....... xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ....... 1

1.1 Usuli wa Mada ....... 1

1.2 Kwa nini Hadithi Fupi? ....... 4

1.3 Suala la Utafiti ....... 5

1.4 Madhumuni ya Utafiti ....... 5

1.5 Maswali ya Utafiti ....... 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti ....... 6

1.7 Upeo wa Utafiti ....... 6

1.8 Maelezo ya Istilahi ....... 8

1.9 Mwauo wa Maandishi ....... 9

1.9.1 Utangulizi ....... 9

1.9.2 Dhana ya Mtoto ....... 9

1.9.3 Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni ....... 10

1.9.4 Mimba za Mapema Ulimwenguni ....... 11

1.9.5 Mimba za Mapema Nchini Kenya ....... 12

1.9.6 Utafiti wa awali Kuhusu Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni. ....... 14

1.9.7 Misingi ya Nadharia ....... 17

1.10 Mbinu Za Utafiti ....... 20

1.10.1 Utangulizi ....... 20

1.10.2 Utafiti wa Maktabani ....... 20

1.10.3 Uteuzi wa Sampuli ....... 20

1.10.4 Ukusanyaji wa Data ....... 22

1.10.5 Uchanganuzi wa Data ....... 22

1.10.6 Uwasilishaji wa Data ........ 23
1.10.7 Maadili ya Utafiti ........ 23
1.11 Hitimisho ........ 23

**SURA YA PILI: HISTORIA YA WAANDISHI WA HADITHI FUPI TEULE NA MUHTASARI WA HADITHI TEULE ........ 24**
2.1 Utangulizi ........ 24
2.2 Muhtasari wa Waandishi wa Hadithi Teule na Hadithi Teule ........ 24
2.2.1 Kanda la Usufi ........ 24
2.2.2 Mwana wa Darubini ........ 26
2.2.3 Shogake Dada ana Ndevu ........ 27
2.2.4 Mame Bakari ........ 29
2.2.5 Namchukia Babangu ........ 31
2.2.6 Shimo la Maisha ........ 33
2.2.7 Malimwengu ........ 34
2.2.8 Safari ya Maangamizi ........ 36
2.2.9 Shetani Hana Hatia ........ 37
2.3 Hitimisho ........ 38

**SURA YA TATU: VISABABISHI VYA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI ........ 39**
3.1 Utangulizi ........ 39
3.2 Visababishi vya Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni ........ 39
3.2.1 Ubakaji ........ 39
3.2.2 Ukali na Ukatili wa Wazazi na Walezi ........ 43
3.2.3 Mazingira na Majira Mabaya ........ 45
3.2.4 Kutowajibika kwa Wazazi na Walezi ........ 48
3.2.5 Shinikizo la Wanarika ........ 50
3.2.6 Matumizi Mabaya ya Likizo ........ 51
3.2.7 Ukiukaji wa Maadili ........ 52
3.2.8 Ulipizaji Kisasi ........ 54
3.2.9 Kukidhi Mahitaji ya Kila Siku ........ 56
3.2.10 Uyatima ........ 58
3.2.11 Uamuzi Mbaya ........ 59

3.2.12 Matumizi ya Pombe na Dawa za Kulevya ................................................60
3.3 Hitimisho ........................................................................................................61

**SURA YA NNE: ATHARI ZA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI ..........................................................63**
4.1 Utangulizi ........................................................................................................63
4.2 Athari za Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Mapema ................................63
4.2.1 Ujauzito Utotoni Usiotarajiwa ....................................................................63
4.2.2 Unyanyapaa ..................................................................................................67
4.2.3 Usiri ..............................................................................................................68
4.2.4 Kifo ...............................................................................................................70
4.2.5 Ndoa za Mapema ..........................................................................................73
4.2.6 Kufukuzwa Nyumbani ..................................................................................74
4.2.7 Msongo wa Mawazo .....................................................................................75
4.2.8 Kutwika Wazazi na Jamaa Majukumu Zaidi ..............................................78
4.2.9 Kuambukizwa Virusi vya UKIMWI ..........................................................80
4.2.10 Ukosefu wa Amani Katika Familia ..........................................................82
4.2.11 Kunyimwa Nafasi ya Kukaa na Mwanao ..................................................83
4.2.12 Kutomakinika Masomoni ..........................................................................84
4.2.13 Kuachishwa Kazi .......................................................................................86
4.2.14 Kuacha Shule ..............................................................................................87
4.2.15 Majuto ........................................................................................................89
4.2.16 Kisasi ..........................................................................................................90
4.3 Hitimisho ........................................................................................................91

**SURA YA TANO: FALSAFA YA WAANDISHI KUHUSU SULUHU KWA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI ..........................................................92**
5.1 Utangulizi ........................................................................................................92
5.1.1 Kuweko na Sheria ya kutoa Adhabu kali kwa Wanaoshiriki Mapenzi na Watoto ..........................................................................................................93
5.1.2 Wanajamii Washirikiane Kuwasaidia watoto Wanaodhulumiwa Kimapenzi na Kuwaadhibu Wanaowanyanyasa ........................................94
5.1.3 Kuwaadilisha Watoto ifaavyo Kuhusu Suala la Kushiriki Mahaba ............97
5.1.4 Watoto Kufundishwa Namna za Kujikinga na Mimba za Utotoni .............99

5.1.5 Wanaume Wanaoshiriki Mapenzi na Watoto Wanyofolewe ....................100
5.1.6 Mtoto Kutafuta Rafiki wa Kumfaa awapo Mhanga wa Mahaba au Ujauzito ......................................................................................101
5.1.7 Watoto wanaokuwa Wajawazito Kurudishwa Shuleni ............................103
5.1.8 Wanaoshiriki Mahaba na Watoto Wakanunue Mapenzi kwa Makahaba..104
5.1.9 Watoto Wanaodhulumiwa Kimapenzi Wapate Fidia ...............................105
5.2 Hitimisho........................................................................................107

**SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ............108**
6.1 Utangulizi........................................................................................108
6.2 Muhtasari........................................................................................108
6.3 Hitimisho........................................................................................109
6.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye.............................................110

**MAREJELEO ........................................................................................111**
**VIAMBATISHO ....................................................................................115**
Kiambatisho 1: Idhini ya Utafiti.........................................................115
Kiambatisho 2: Kibali cha Utafiti .......................................................116

## ORODHA YA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| **APHRC** | African Population and Health Research Center |
| **CDF** | Children's Dignity Forum (Tanzania) |
| **FORWARD** | Foundation for Women's Health Research and Development (Tanzania) |
| **KDHS** | Kenya Demographic and Health Survey |
| **NACOSTI** | National Commision for Science, Technology and Innovation |
| **NCCK** | National Council of Churches of Kenya |
| **SADHS** | South African Demographic and Health Survey |
| **UN** | United Nations |
| **UNFPA** | United Nations Population Fund |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **WHO** | World Health Organisation |

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Mtoto ni kiumbe ambaye anafaa kulindwa kutokana na aina zote za dhuluma. Katiba ya Kenya (2010) inamweleza mtoto kama mtu yeyote ambaye ana umri chini ya miaka kumi na minane. Shirika la Afya Duniani (WHO) linamtaja mtoto kama mtu aliye na umri wa miaka chini ya kumi na tisa. Sheria mbalimbali zinazowalinda watoto zinaubainisha uhusiano wa kimahaba na ujauzito utotoni kama ukiukaji wa haki za watoto na unyanyasaji wa watoto. Hata hivyo, suala hili limekuwepo kwa muda mrefu licha ya kuwepo kwa sheria zinazolipinga. Ndoto za watoto wengi wa kike wanaosomea katika shule za msingi na upili na wengine wanaofaa kuwa shuleni zimekatizwa hapa nchini na kote ulimwenguni kutokana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Mashirika mbalimbali yametoa ripoti kuhusiana na jambo hili la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kwa mfano, Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO, 2013) ulionyesha kuwa wasichana milioni kumi na sita walio na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi miaka kumi na tisa na wengine milioni moja wenye umri wa chini ya miaka kumi na mitano huwa waathiriwa wa mimba za utotoni kila mwaka. Hii ni idadi kubwa na suala hili linahitaji kutafutiwa suluhu ya mapema kabla ya ndoto za watoto wengi kuangamia.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UN na UNFPA, 2013), kila mwaka watoto milioni saba na laki tatu (7.3) wa kike ambao wako chini ya umri wa miaka kumi na minane hushika mimba na kujifungua. Milioni mbili kati ya watoto hao wana umri usiozidi miaka kumi na minne. Ripoti hii ilieleza kuwa watoto hao hukumbana na matatizo kadha ya kiafya na kijamii kutokana na mimba hizo. Kupitia ripoti ya mashirika haya ni bayana kuwa watoto hushiriki mapenzi hata wakiwa na miaka kidogo kabisa. Pia, ni dhahiri kuwa kuna athari ambazo huletwa na kuwepo na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Nchini Tanzania, wasichana laki nane huacha shule kutokana na kuwa na ujauzito kila mwaka. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya HakiElimu (2011). Maelfu ya wengine huripotiwa kuwa watoro kwani wakipata mimba hawarudi shuleni tena kwa kuhofia kufukuzwa. Isitoshe, ripoti ya Shirika la Kimataifa la Human Rights Watch (2016),

nchini mumo humo, iliyoitwa “Nilikuwa na ndoto ya kumaliza shule,” ilionyesha kuwa asilimia 40 ya wanafunzi wa kike hukatiza masomo yao ya sekondari kutokana na ujauzito.

Katika eneo la Afrika Mashariki, asilimia kubwa ya watoto wanalazimishwa kuolewa wakiwa chini ya miaka kumi na minane. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF, 2017), Sudan Kusini iliongoza kwa asilimia 52, Uganda asilimia 40, Tanzania asilimia 28 na Kenya asilimia 23. Ndoa za mapema ni ukiukaji wa haki za watoto wa kike kwani huchangia uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Ripoti ya Baraza Kuu la Makanisa Nchini Kenya (NCCK,2019) kwa Seneti kuhusu ongezeko la idadi ya watoto wanaopata mimba ilihimiza uzingatifu wa sheria kikamilifu kuhusu dhuluma kwa watoto, hasa dhuluma za kimapenzi. Ripoti hii ilieleza kuwa mimba za utotoni zilisababishwa na ulegevu wa nidhamu na maadili katika jamii. Baraza hili lilisisitiza kuwepo kwa uwajibikaji wa wanajamii katika kuwaadilisha watoto. Ripoti hii ilionyesha kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni havina nafasi hata katika dini ya Kikristo.

Nchini Kenya, suala la mimba za utotoni liliathiri sekta ya elimu. Baraza la Kitaifa la Mitihani Kenya (KNEC) lilikumbana na changamoto pia zilizohusishwa na mimba za mapema. Kila mwaka kuna ripoti za wanafunzi waliofanya mtihani wa kitaifa wakiwa tayari wamejifungua ama ni waja wazito na wengine kujifungua wakati wa mtihani huu. Ripoti ya serikali kupitia Wizara ya Elimu kama alivyoeleza Nyamasege (2018) ilionyesha kuwa takriban watahiniwa mia mbili wa mwaka huo walikuwa wamejifungua katika siku za mitihani ya kitaifa ya shule za msingi na upili. Alieleza kuwa jambo hili lingefanya taifa kutumbukia katika janga iwapo lingeshuhudiwa kila mwaka. Ni kutokana na ripoti hii ambapo wazazi kupitia Muungano wa Kitaifa wa Wazazi Nchini walitoa maoni yao ya kuvumbua mbinu za kukabiliana na suala hili katika shule za msingi na upili. Wazazi hawa walitoa pendekezo kuwa vyombo vya serikali vianze kuwakamata na kuwachukulia  hatua kali wanaohusika na mimba hizi kwa mujibu wa sheria. Pia, walisisitiza kuwa sheria imeharamisha ushiriki ngono na watoto (Atieno, 2019).

Ripoti iliyotolewa na Afisa wa Watoto katika kaunti ya Machakos kwenye siku ya kuadhimisha mtoto wa Kiafrika ilionyesha kuwa, takriban wasichana elfu nne walio na umri wa chini ya miaka kumi na tisa walipata mimba katika kipindi cha miezi mitano, Januari hadi Mei mwaka 2020 (Maundu, 2020). Ongezeko hili lilihusishwa na kuzuka kwa janga la korona humu nchini na kufanya watoto kusalia nyumbani kwa kipindi kirefu. Afisa huyu aliongeza kuwa takriban watoto ishirini na wanane (28) hupata mimba kila siku katika kaunti hiyo. Siku iyo hiyo, wasichana wadogo nchini walitoa wito kwa viongozi kukomesha mimba za utotoni kwani jambo hili liliwanyima haki ya elimu na pia nafasi bora maishani. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Kituo cha Utafiti kuhusu Afya na Idadi ya Watu barani Afrika (APHRC, 2020). Kutokana na ripoti hizi ni dhahiri kuwa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni tatizo linaloendelea kusumbua wanajamii hadi sasa hivi na suluhu ya haraka inahitajika.

Vyombo vya habari hutoa ripoti mara kwa mara zinazohusu kunajisiwa kwa watoto na visa vya mimba za mapema. Ominde na Chepkemboi (2020) walieleza jinsi wanaume watatu walivyoshtakiwa kwa kuwanajisi watoto wa miaka minane, kumi na minne na kumi na saba katika sehemu mbalimbali za kaunti ya Kakamega. Ojamaa (2020) alitoa ripoti ya mwalimu aliyeachiliwa kwa dhamana kutokana na kumnajisi mwanafunzi katika kaunti ya Bungoma. Nyaberi (2020) alieleza jinsi machifu katika kaunti ya Kisii walivyowatafuta wanafunzi waliokosa kurudi shuleni. Hii ni kutokana na watoto kujiingiza katika kazi za kujitafutia pesa kama anasa kwa wasichana iliyochangia kutungwa kwa mimba za utotoni. Wasichana wengi katika kaunti ya Narok pia hawakuwa wamerudi shuleni kuanza muhula mpya baada ya likizo ya Desemba kutokana na mimba za mapema kama alivyoeleza Sayagie (2020).

Watafiti wa Kiswahili pia hawajaachwa nyuma katika kuliangalia suala hili. Kavuria (2008) akitafitia dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili alieleza unyanyasaji wa kimapenzi kuwa aina moja ya dhuluma walizokumbana nazo watoto. Aliongeza kuwa watoto wengine walipodhulumiwa huwa haki haipatikani kwani kesi zao utupiliwa mbali. Maelezo ya mtafiti huyu yalikuwa wazi kuwa haki za watoto zilikuwa zinakiukwa zikiwemo haki zilizohusiana na suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Akieleza kuhusu masuala ibuka, Mayieka (2015) alisema kuwa mapenzi na ndoa na ukiukaji wa haki za watoto ni baadhi ya masuala ibuka. Aliongeza kuwa watoto walidhulumiwa kimapenzi hasa wanafunzi walio katika shule za msingi na upili. Maoni haya yalionyesha kuwa athari ya suala hili ni dhuluma kwa mtoto ambaye bado ni mwanafunzi aliye katika harakati ya kujenga msingi wa maisha bora. Vilevile, uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni ukiukaji wa haki za watoto.

Akishughulikia matatizo ya mwanamke, Ruto (2015) alisema kuwa matatizo mengine yaliweza kuleta athari kama vile kukata tamaa kwa mwanamke, upweke na hata woga. Alitambua matatizo haya kama dhuluma za kimapenzi na kunyimwa haki miongoni mwa mengine. Madai haya yalionyesha kuwa suala la mapenzi na mimba za utotoni ni tatizo kwa mtoto wa kike. Maelezo haya yalimpa mtafiti baadhi ya athari ambazo humkumba mwanamke hasa kutokana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Fasihi ya Kiswahili ilitumiwa na waandishi mbalimbali kueleza hali ilivyo katika jamii zetu. Kwa sababu hii, utafiti huu ulishughulikia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Mtafiti alisukumwa na kuweko kwa ongezeko kubwa la visa vya uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema miongoni mwa watoto wa kike ambao wamo au wanafaa kuwa shuleni. Hii ni kwa mujibu wa ripoti za mashirika na baraza mbalimbali na pia sekta ya habari kupitia runinga, redio na magazeti. Hili ni suala nyeti ambalo lilihitaji suluhu ya haraka kutokana na athari zake kwa wanajamii.

### 1.2 Kwa nini Hadithi Fupi?

Utanzu wa hadithi fupi ulitumika katika utafiti huu kwa kuwa una sifa zilizooana na kazi hii. Wamitila (2002) alieleza kwamba hadithi fupi ina uwezo wa kuyatambua na kuyaelezea mabadiliko yaliyopo katika jamii. Hadithi fupi pia huwa na sifa ya kuzunguka tukio moja kwa kumtumia mhusika angalau mmoja mkuu katika kipindi maalum na hivyo kuibua athari ya moja kwa moja kwa msomaji (M’ngaruthi, 2019). Kwa kuwa hadithi fupi huwa na wahusika wachache, sifa na umuhimu wa wahusika hawa uliweza kubainika wazi. Utanzu wa hadithi fupi pia ni utanzu wa hivi karibuni na falsafa na msimamo wa waandishi wake ulikuwa unashadidia yaliyopo katika jamii ya leo kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Isitoshe, hadithi fupi hizi

zilikuwa katika diwani zenye mkusanyiko wa hadithi kadha zilizoandikwa na waandishi tofauti. Waandishi hao walikuwa na falsafa tofauti kuhusu visababishi, athari na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kazi za waandishi wa kike na wale wa kiume zilitumika ili kutambua iwapo jinsia hizi mbili zina mtazamo tofauti kuhusu mada hii. Uchaguzi wa hadithi fupi katika utafiti huu uliupa utafiti huu mwelekeo wa kitaaluma kwani uliweza kueleza umuhimu wa hadithi fupi za Kiswahili kama chombo cha kujadili masuala ibuka na masuala nyeti kutokana na sifa yake ya usahili na upatikanaji wa mawazo ya waandishi wengi katika mkusanyo mmoja wa kazi ya nathari.

### 1.3 Suala la Utafiti

Suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni ukiukaji wa maadili ya jamii na pia haki za watoto. Fasihi ni mojawapo ya nyenzo muhimu ambazo hutumika katika kuangazia mambo yanayotokea katika jamii na athari zake kwa wanajamii. Licha ya kuwa watafiti wa fasihi ya Kiswahili wametafitia mawanda mbalimbali ya fasihi katika jamii, ikiwemo kushughulikia masuala ibuka na dhuluma dhidi ya watoto, suala nyeti la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika fasihi ya Kiswahili halijachunguzwa kama mada ya utafiti. Kwa hivyo, utafiti huu ulinuia kushughulikia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Mtafiti alichunguza na kueleza visababishi, athari na falsafa ya waandishi kuhusu suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Hadithi fupi teule katika diwani zifuatazo zilihakikiwa; *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016).

### 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria yafuatayo;

i. Kuhakiki visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili.
ii. Kutathmini athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kurejelea waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili.
iii. Kujadili falsafa za waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili kuhusu suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo;

i. Ni nini kinachosababisha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili?
ii. Je, uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zina athari gani kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili?
iii. Ni nini falsafa ya waandishi kuhusu suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika kazi teule za Kiswahili?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawahamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa fasihi ya Kiswahili ikiwemo kumulika yanayotendeka katika jamii pana. Pia, utatoa mchango katika mijadala ya kijamii kuhusu suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Vilevile, waandishi wa fasihi watanufaika na utafiti huu kwa kuwawezesha kutambua masuala ibuka na masuala nyeti katika jamii. Waandishi hawa watahamasishwa kuhusu nafasi ya fasihi kama chombo cha kuyafichua maovu yanayoiathiri jamii na kupendekeza suluhu. Isitoshe, watetezi wa haki za watoto nchini na kimataifa watanufaika na utafiti huu kwa kuelewa mchango wa fasihi ya Kiswahili kuhusu visababishi, athari na hata suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyosawiriwa na waandishi wa kazi teule za Kiswahili.

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia hadithi fupi teule za Kiswahili kuhusiana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Hadithi fupi tisa kutoka kwa diwani nne za hadithi fupi zilishughulikiwa. Diwani hizi ni: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Kazi hizi zote ziliandikwa baada ya kupitishwa kwa sheria za watoto mwaka 2001 nchini Kenya kwani utafiti huu ulimlenga mtoto wa kike.

Hadithi fupi zenye maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zilichaguliwa miongoni mwa hadithi fupi nyingine katika diwani hizi. Utanzu wa hadithi fupi ulitumika kwa kuwa huu ni utanzu wa hivi karibuni na falsafa na msimamo

wa waandishi wake ulikuwa unashadidia yaliyopo katika jamii ya leo kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kazi za waandishi wa kike na wale wa kiume pia zilitumika ili kutambua iwapo jinsia hizi mbili zilikuwa na mtazamo tofauti kuhusu mada hii. Kazi hizi ziliteuliwa kwa kuwa hapa ndipo palipatikana data iliyohusiana na mada ya utafiti. Maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ndiyo yalimwongoza mtafiti huku akiegemea katika madhumuni na nadharia ya utafiti.

### 1.8 Maelezo ya Istilahi

Istilahi hizi zilitumika katika utafiti huu ambapo zilifafanuliwa kurejelea matumizi yake kwenye utafiti.

**Athari:** Ni madhara yanayotokana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

**Falsafa ya Mwandishi**: Msimamo au mwelekeo wa mwandishi kuhusu jambo fulani.

**Kisababishi:** Ni chanzo cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

**Mimba za Utotoni:** Ni hali ambapo mtoto wa kike anapata ujauzito kabla ya kutimiza miaka kumi na minane au kabla ya kuhitimu masomo ya shule ya upili.

**Mtoto:** Mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane. Pia, ni mtu ambaye amesajiliwa katika elimu ya msingi na hajahitimu masomo ya shule ya upili.

**Suluhu:** Utatuzi wa mahusiano ya mapenzi ili kuepuka mimba za utotoni.

**Uhusiano wa Kimahaba Utotoni:** Hisia za kimapenzi kati ya mtoto na mtoto mwingine au mtoto na mtu mzima wenye nia ya kuridhishana kingono au kujiridhisha kihisia.

### 1.9 Mwauo wa Maandishi

### 1.9.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu maandishi na ripoti mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti huu. Mtafiti aliyapitia maandishi mbalimbali yaliyohusu mtoto na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ili kupata msingi wa utafiti huu. Pia, kazi za kiutafiti ambazo zilihusiana na mada ya utafiti huu ziliauliwa ili kujua kina walichofikia watafiti wa awali na kutambua pengo ambalo waliacha katika utafiti wao. Nadharia iliyoongoza utafiti huu vilevile ilielezwa ili kuonyesha mihimili iliyotumika katika utafiti huu.

### 1.9.2 Dhana ya Mtoto

Neno mtoto lina fasiri mbalimbali kutegemea muktadha ambamo linatumika kama vile miktadha ya kisheria, kielimu, kitamaduni, kidini na mingineyo. Katika muktadha wa sheria, Umoja wa Mataifa ulitoa azimio kuhusu haki za watoto ambalo lilikubaliwa na nchi nyingi duniani kuwa mkataba wa kimataifa. Mkataba huu ulieleza kuwa mtoto ni upindi wa mtu hadi anapofikia miaka kumi na minane. Aidha, mkataba wa Kiafrika juu ya haki na ustawi wa watoto (1990) ambao ulikubaliwa na Umoja wa Afrika ulimweleza mtoto kama mtu ambaye hajapitisha umri wa miaka kumi na minane.

Kwa upande wa sheria za kikatiba, katiba nyingi za nchi za Afrika zinafafanua maana ya mtoto. Nchi hizi ni pamoja na Tanzania, Nigeria na Msumbiji. Katiba hizi zinamtaja mtoto kama mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane. Katiba ya Kenya (2010) ina maelezo yayo hayo.

Mashirika mbalimbali pia yalizingatia kigezo cha umri yalipotoa maelezo juu ya mtoto. Shirika la Afya Duniani (WHO) lilieleza mtoto kama mtu aliye na umri wa miaka isiyozidi kumi na tisa. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia watoto (UNICEF) kwa upande mwingine lilimwona mtoto kama mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane. Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Kisayansi na Kitamaduni (UNESCO) lilikuwa na msimamo kuwa mtoto ni mtu mwenye umri wa miaka kumi na minane.

Isitoshe, sheria za elimu zinaeleza maana ya mtoto. Kwa mujibu wa elimu, mtoto huwa mtu ambaye amesajiliwa katika elimu ya msingi na hajahitimu masomo ya shule ya

upili. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya Kenya kuhusu masomo ya kimsingi kifungu nambari 14 cha mwaka 2013.

Utafiti huu ulijikita katika katiba ya Kenya ambapo mtoto ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane, (Katiba mpya ya Kenya, 2010). Vile vile, ulizingatia mtoto kama mtu ambaye amesajiliwa katika elimu ya msingi na hajahitimu masomo ya shule ya upili kwani utafiti huu ulimlenga mtoto wa kike ambaye yumo au anafaa kuwa katika masomo ya msingi.

### 1.9.3 Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni

Kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya utafiti huu, uhusiano wa kimahaba ni uhusiano wa kihisia kati ya mtoto na mtoto mwingine au mtoto na mtu mzima wenye nia ya kuridhishana kingono au kujiridhisha kihisia. Uhusiano huu unaweza kuwa kwa hiari au kwa kulazimishwa. Ubinafsi na unafiki husukuma watu wengi na kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba kama anavyoeleza Burke (1999). Hata hivyo, uhusiano wa aina hii huleta majonzi mengi kwa wahusika (Njogu ,1997). Mayieka (2015) kwa upande wake alieleza kuwa jamii inafaa kuwajibika ili kuweza kuwaelekeza vijana kuhusiana na suala la kimapenzi kwani mapenzi ya kiholela shuleni huwa na athari kama kusababisha ndoa za mapema na pia mimba za utotoni. Mayieka alipendekeza kuwa waliokiuka haki za watoto walifaa kuadhibiwa.

Mimba za utotoni kwa upande mwingine ni pale binti anapata ujauzito kabla ya kutimiza miaka kumi na minane au kabla ya kuhitimu masomo ya shule ya upili. Mimba hizi zinaweza kusababishwa na ukosefu wa elimu mwafaka kuhusu suala la uzazi, shinikizo la wanarika na umaskini (Kiarie, 2015). Athari ya mimba hizi ni kama vifo miongoni mwa wasichana wadogo, athari za kiafya ambazo husababishwa na kuavya mimba, kuacha shule na unyanyapaa (WHO, 2011). Isitoshe, maoni mbalimbali yalitolewa kuhusiana na namna ya kukabiliana na mimba za utotoni.

Utafiti huu ulilenga kushughulikia suala la uhusiano wa kimahaba na ujauzito utotoni kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili. Katika hali hii, mtafiti alieleza visababishi, athari na suluhu kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyoshughulikiwa na waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

### 1.9.4 Mimba za Mapema Ulimwenguni

Katika eneo la Afrika Kusini mwaka 2003, ripoti ya SADHS ilionyesha kwamba asilimia 27 ya wasichana nchini humo walikuwa na watoto katika umri wa chini ya miaka kumi na tisa. Mimba hizi zilitokea nje ya ndoa. Asilimia 90 ya wasichana wenye umri wa kati ya miaka 15-19 walikuwa wameshiriki ngono katika miezi kumi na miwili iliyopita (Pettifor et al, 2005). Ripoti hii ilikuwa dhahiri kuwa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni liliathiri ata nchi zilizostawi kama vile Afrika Kusini na hivyo suluhu ya haraka na ya kudumu iliitajika.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO, 2011) ilionyesha kuwa wasichana milioni kumi na sita (16) ambao wana umri wa kati ya miaka kumi na mitano na kumi na tisa (15-19) na wasichana milioni moja walio na umri wa chini ya miaka kumi na mitano (15) walikuwa waathiriwa wa mimba za utotoni kila mwaka. Ripoti hii ilipendekeza pachukuliwe hatua za mapema za kukomesha hali hii kwani idadi ya waathiriwa iliendelea kuongezeka kila mwaka. Idadi hii ilijumuisha nchi maskini na zilizoimarika kiuchumi. Kwa mfano, shirika hili lilisema kuwa nchini Marekani mwaka 2015 zaidi ya watoto laki mbili walizaliwa na mabinti wenye umri mdogo. Shirika hili la Afya Duniani (2020) liliendelea kutoa ripoti kuwa janga la ugonjwa wa korona lilichangia wasichana wengi katika nchi kadha duniani kujitumbukiza katika mazingira ya kupata mimba za utotoni. Mtafiti alidhamiria kutambua yaliyosemwa kuhusiana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni na waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

Nchini Tanzania, wasichana laki nane huacha shule kutokana na kuwa na ujauzito kila mwaka. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya HakiElimu (2011). Maelfu ya wengine walilipotiwa kuwa watoro kwani wakipata mimba hawarudi shuleni tena kwa kuhofia kufukuzwa. Ripoti hii ilituwezesha kubaini athari nyingine zilizosababishwa na mimba za utotoni kwa mujibu wa waandishi wa kazi teule.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UN na UNFPA, 2013), kila mwaka watoto milioni saba na laki tatu (7.3) wa kike walio chini ya umri wa miaka 18 hushika mimba na kujifungua. Milioni mbili kati ya watoto hao huwa na umri usiozidi miaka kumi na minne. Ripoti hii ilieleza kuwa watoto hao hukumbana na matatizo kadha ya kiafya na kijamii kutokana na mimba

hizo. Ripoti hii ilitoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwani mtafiti aliweza kubaini baadhi ya athari ambazo huletwa na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kimataifa la Human Right Watch (2016), Tanzania, iliyopewa jina "Nilikuwa na ndoto ya kumaliza shule," asilimia 40 ya wanafunzi nchini humo hukatiza masomo yao ya sekondari kutokana na ujauzito. Ripoti hii ilionyesha kwamba suala la mimba za mapema si la Kenya tu bali pia la kimataifa na athari mojawapo ya mimba za utotoni ni kuacha shule. Utafiti huu ulisaidia katika kupata visababishi na athari nyinginezo kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Asilimia kubwa ya watoto walilazimishwa kuolewa wakiwa chini ya miaka kumi na minane. Kwa mfano, Sudan Kusini ina asilimia 52, Uganda asilimia 40, Tanzania 28 na Kenya 23. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF, 2017). Taarifa hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ndoa za mapema huchangia uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni, jambo ambalo ni kinyume na haki za watoto. Utafiti huu ulilenga kazi teule za Kiswahili kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema.

### 1.9.5 Mimba za Mapema Nchini Kenya

Shirika la UNFPA lilitoa takwimu za kati ya Juni 2016 na Julai 2017 na kubaini kuwa watoto takriban laki nne (378,397) wa umri kati ya miaka kumi na kumi na tisa (10-19) nchini Kenya walishika mimba. Walidai kuwa, kati ya watoto watano wenye umri kati ya miaka kumi na mitano na kumi na tisa, mmoja wao alikuwa amejifungua au alikuwa mjamzito. Kwa kuongozwa na waandishi wa kazi teule za Kiswahili, mtafiti aliweza kubaini visababishi vya hali hii.

Ripoti ya Wizara ya Elimu kama alivyoeleza Nyamasege (2018) ilionyesha kuwa takriban watahiniwa mia mbili wa mwaka huo walikuwa wamejifungua katika siku za mitihani ya kitaifa ya shule za msingi na upili, jambo ambalo lingefanya taifa kutumbukia katika janga iwapo lingeshuhudiwa kila mwaka. Ilisemekana kuwa wasichana wadogo walikuwa wajawazito walipokuwa wakifanya mtihani wa kitaifa mwaka huo na wengine kufanyia mtihani katika hospitali mbalimbali nchini baada ya kujifungua. Kutokana na kauli hii, wabunge walipendekeza Kamati ya Bunge kuhusu

Elimu ichunguze chanzo cha mimba za mapema miongoni mwa wanafunzi nchini. Pia, walipendekeza suluhu ya kudumu kwa tatizo hilo ambalo liliwazuia watoto wengi wa kike kujiendeleza kimasomo. Kauli hii ilidhihirisha kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni tatizo kwa wanafunzi wengi nchini. Utafiti huu ulinuia kubaini chanzo cha jambo hili, athari zake na pia suluhu kwa mujibu wa waandishi wa kazi teule kwani waandishi ni wanajamii pia na wanaielewa jamii yao.

Isitoshe, ripoti iliyotolewa na Matheka (2018) ilionyesha maeneo ambako wanafunzi hupata mimba kwa wingi. Ripoti hii ilibainisha kuwa visa vingi hutokea katika maeneo ya mashambani ambako wakaazi ni maskini. Takwimu za KDHS zilionyesha baadhi ya maeneo haya kama alivyoeleza Matheka kwenye ripoti yake. Takwimu hizi za serikali zilionyesha kuwa idadi ya wasichana waliopata mimba wangali wanafunzi ilikuwa inatisha huku baadhi ya walimu wakilaumiwa kwa kuhusika na mimba hizo kwa kuwa na uhusiano wa kimahaba na wanafunzi wa kike. Ojomaa (2020) alieleza jinsi mwalimu alivyoachiliwa kwa dhamana baada ya kudaiwa kumnajisi mwanafunzi. Kuna walimu ambao pia waliachishwa kazi kutokana na tabia ya kushiriki mahaba na wanafunzi wa kike na wengine kuwapachika watoto hao mimba.

Muungano wa Kitaifa wa Wazazi Nchini Kenya (2019) ulibaini mbinu za kukabiliana na mimba za mapema. Hii ni baada ya kupata ripoti kuwa kulikuwa na idadi kubwa ya waathiriwa nchini hasa katika kaunti za; Narok, Kilifi, Meru, Bungoma, Nairobi, Busia, Migori na Homa Bay. Wazazi hawa walitoa pendekezo kuwa vyombo vya serikali vianze kuwakamata na kuwachukulia hatua kali wanaohusika na mimba hizi kwa mujibu wa sheria. Muungano huu ulisisitiza kuwa sheria imeharamisha ushiriki ngono na watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na minane.

Ripoti ya Baraza Kuu la Makanisa Nchini Kenya (NCCK, 2019) kwa Seneti kuhusu ongezeko la idadi ya watoto waliopata mimba ilihimiza uzingatifu wa sheria kikamilifu kuhusu dhuluma kwa watoto, hasa dhuluma za kimapenzi. Ripoti hii ilieleza kuwa mimba za utotoni zilisababishwa na ulegevu wa nidhamu na maadili katika jamii. Baraza hili lilisisitiza kuwepo na uwajibikaji wa wanajamii katika kuwaadilisha watoto. Ripoti hii ilionyesha kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni havina nafasi hata katika dini ya Kikristo.

Mwende (2020) alieleza kuwa takwimu za Baraza la Kitaifa Kuhusu Idadi ya Watu (NCPC) zilionyesha kwamba kuna ongezeko la mimba za mapema miongoni mwa wasichana wadogo. Mmoja kati ya kila wasichana watano wenye umri kati ya miaka 15-19 ni mjamzito au amejifungua. Aliendelea kueleza kuwa baadhi ya visababishi vya hali hii ni pamoja na ufukara, ndoa za mapema na ubakaji. Utafiti huu ulimwezesha mtafiti kueleza visababishi, athari na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyoelezwa na waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

### 1.9.6 Utafiti wa awali Kuhusu Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni.

Ntiba (2011) akitafitia taathira ya dhamira kwa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili alieleza kuhusu ukiukaji wa haki za watoto ikiwemo kudhulumiwa kimapenzi na watu wazima. Alisema kuwa dhuluma hii ilisababisha ujauzito utotoni na pia ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti wa msomi huyu ulichangia utafiti huu kwani sote tuliegemea katika utanzu wa hadithi fupi ambapo falsafa za waandishi wake ziliweza kufaana. Pia, mtafiti alitumia diwani mbili ambazo zilitumika katika utafiti huu ingawa hadithi fupi teule zingine zilitofautiana. Tofauti na utafiti huu, mtafiti huyu aliongozwa na dhamira kwa mtindo katika kazi teule huku utafiti huu ukiongozwa na maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika kazi teule.

Naliaka (2012) alifanya utafiti kuhusu uhakiki wa hali ya vijana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Katika utafiti huu alizungumzia matatizo yaliyowakumba vijana katika riwaya hii kama vile mazingira wanamoishi. Utafiti huu una mchango kwani ulimwezesha mtafiti kuangalia hali ya watoto na ikiwa mazingira yaliweza kuwaathiri watoto. Tofauti na kazi hii, Naliaka aliangalia vijana kwa ujumla huku utafiti huu ukimzunguka mtoto wa kike.

Rono (2013) alitafitia uhakiki wa kimaudhui na kifani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Mtafiti huyu aliongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamii na kutambua maudhui ya mapenzi na haki miongoni mwa maudhui mengine. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwani ulieleza jinsi mapenzi yalichangia mimba za utotoni na hivyo kuzikiuka haki za watoto. Rono alichanganua maudhui ya riwaya hii yakiwemo maudhui ya mapenzi ila hakuzamia katika maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Mwanya aliouacha katika utafiti wake ulizibwa na utafiti huu kwa kuzichanganua hadithi fupi teule na kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

Mayieka (2015) akitafitia masuala ibuka katika riwaya za kisasa kwa kuegemea katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi yangu* na kuongozwa na Nadharia ya uhalisia aligundua kuwa kuna masuala ibuka mbalimbali kama mapenzi na ndoa, haki za watoto na mengineyo. Utafiti wake utatoa mchango katika utafiti huu kwa sababu mapenzi miongoni mwa watoto ni mojawapo ya suala la utafiti huu kama linavyoangaziwa na waandishi wa hadithi fupi teule. Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni suala ibuka ambalo ni ukiukaji wa haki za watoto na hivyo kuoana vyema na utafiti huu. Hata hivyo, mtafiti huyu hakushughulikia visababishi na athari za masuala hayo. Tofauti na utafiti huu mtafiti huyu alishughulikia masuala ibuka kijumla huku utafiti huu ukilenga suala ibuka na suala nyeti la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya za *Anasa* na *Asali chungu* ni suala lililotafitiwa na Wanjala (2015) . Akielekezwa na nadharia ya sosholojia ya fasihi, mtafiti huyu alitambua kuwa asasi ya elimu, mazingira au makaazi huathiri malezi na utambulisho wa vijana. Mchango wa utafiti huu kwa kazi hii ni kuwa mtafiti aliegemea katika malezi ili kutambua jinsi yanaweza kuathiri vijana huku utafiti huu ukiegemea kwa watoto. Tofauti na utafiti huu, mtafiti alinuia kutambua iwapo elimu, mazingira au makaazi yaliweza kuathiri au kuchangia uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Matatizo ya mwanamke katika *Kidagaa Kimemwozea* na *Nyuso za Mwanamke* yalishughulikiwa na Ruto (2015) akiongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Katika matokeo yake, alitambua kuwa matatizo ya mwanamke ni kama dhuluma za mapenzi na kunyimwa haki. Anaendelea kueleza kuwa matatizo haya huleta athari kama kukata tamaa kwa mwanamke, upweke na pia woga. Utafiti wa mtafiti huyu ulichangia utafiti huu kwani ulishughulikia suala la mwanamke na changamoto ambazo humkumba. Hata hivyo, tofauti na utafiti huu mtafiti aliegemea katika matatizo ya mwanamke kwa jumla na hakueleza athari ambazo zinaweza kuletwa na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Utafiti huu ulishughulikia mwanamke mwenye umri

wa chini ya miaka kumi na minane katika maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhalisia, Ondieki (2015) aliangazia usawiri wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili zilizoandikwa na Mohamed Suleiman na Euphrase Kezilahabi. Mtafiti huyu alieleza kuwa watoto wanasawiriwa kama wenye kudhulumiwa kimapenzi na kunyimwa uhuru wa kujieleza miongoni mwa dhuluma nyingine. Kazi ya Ondieki ilichangia utafiti huu kwani mtafiti pia alishughulikia masuala ya watoto. Mtafiti aligundua kuwa tatizo mojawapo la watoto ni kudhulumiwa kimapenzi. Jambo hili limetafitiwa kwa kina katika utafiti huu kwani mtafiti wa awali hakulizamia kiundani. Mtoto wa kike ndiye aliutawala utafiti huu tofauti na utafiti wa Ondieki ambao ulijikita kwenye jinsia zote.

Kiarie (2015) alitafitia sababu zinazochangia mimba za mapema katika shule za umma za kaunti ndogo ya Imenti Kaskazini, Kaunti ya Meru, Kenya. Mtafiti huyu alitambua kuwa tamaduni za watu, mtandao na msukumo wa wanarika miongoni mwa mambo mengine huchangia mimba za mapema katika eneo bunge hili. Utafiti huu, ingawa si wa kifasihi wala Kiswahili uliuwekea msingi utafiti huu kwa sababu mtafiti alitafitia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa hadithi fupi teule za Kiswahili. Mtafiti pia alipendekeza utafiti kufanywa kuhusu athari za mimba za mapema, pengo ambalo litazibwa na utafiti huu wa kifasihi.

Njeru (2018) alifanya utafiti kuhusu suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili: *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*. Utafiti wa msomi huyu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani ulihusu suala ibuka la ardhi sawa na suala ibuka la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Ingawa masuala ibuka ni mengi, suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ambalo kwa sasa limekuwa nyeti lilimpa mtafiti pengo la utafiti wake.

Uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed ni utafiti ulioshughulikiwa na Mwenda (2018). Utafiti huu ulieleza mitindo aliyotumia mwandishi huyu kupitisha ujumbe wake kwa wasomaji. Utafiti huu una manufaa kwa kuwa ulisaidia kuelewa mitindo iliyotumiwa na waandishi wa hadithi fupi teule ili

kupitisha maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwani sote tulijikita katika utanzu wa hadithi fupi. Tofauti na utafiti wake, utafiti huu uliangazia maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema na wala si namna ya uwasilishaji wa maudhui tu.

Mashirika ya Children's Dignity Forum (CDF) na Foundation for Women's Health Research Development (FORWARD) (2018) yalifanya utafiti shirikishi kuhusu mimba na kuwa mama katika umri mdogo katika wilaya ya Mpwapwa, Tanzania. Utafiti huu ulionyesha kuwa mimba za utotoni husababisha dharau kutoka kwa wanajamii. Watafiti walisema mimba hizi huchangiwa na umaskini, uzoefu wa wasichana wa kuwaona wasichana wengine walio na mimba katika mazingira ya shule, ukosefu wa elimu, uduni wa elimu itolewayo nyumbani kuhusu jinsia na mahusiano na ngono za malipo miongoni mwa mambo mengine. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa suala hili si la kitaifa bali la kimataifa na visababishi viliweza kukaribiana. Hivyo basi, utatuzi ukipatikana katika eneo moja unaweza kusaidia katika maeneo mengine. Utafiti huu uliegemea katika kazi teule za Kiswahili kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwani fasihi inaweza kusomwa katika maeneo mengi ulimwenguni na hivyo kutoa mchango hasa wa utatuzi kwa wengi.

### 1.9.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Nadharia hii iliasisiwa na wahakiki wa waasisi wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya 1960. Waasisi na watetezi wakuu wa nadharia hii ni; Wolfgang Iser (1974,1978), Stanley Fish (1980) na Jane Tompkins (1980).

Nadharia hii humweka msomaji katikati ya uhakiki wa fasihi na hujihusisha na namna kazi za kifasihi hupokelewa na wasomaji katika wakati fulani kwa kuangalia athari inazozua kwa msomaji katika kipindi maalum. Kwa mujibu wa Fish (1980), ni jukumu la wasomaji kuyafasiri matini husika katika mazingira tofauti. Hii ina maana kuwa, msomaji ana uwezo wa kuipa matini maana namna anavyoielewa wakati huo maalum na maeneo ilipo. Kwa sababu hii, mtafiti aliweza kuzipa kazi teule maana kutokana na usomaji wake kwa kuegemea katika visababishi, athari na pia suluhu kwa uhusiano wa

kimahaba na mimba za utotoni kwa wakati huu ambapo suala hili limesambaa katika kijamii.
Tompkins (1980) akieleza kuhusu nadharia ya Mwitikio wa Msomaji alidai kuwa kazi ya fasihi aghalabu ina mapengo mengi. Msomaji anapaswa kuyaziba mapengo hayo. Kutokana na kuyajaza, msomaji hulazimika kutunga matini mpya ambazo zimechochewa kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa kwa kuwa usomaji unafanyika katika jamii ya kifasiri. Hivyo ni kupitia matini ya waandishi teule ambapo mtafiti alipata matini mpya ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika utafiti huu. Katika utafiti huu, mtafiti alinuia kuziba pengo la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kuongozwa na matini asili za waandishi wa hadithi fupi teule kwa kuangalia visababishi vyake, athari zake na pia suluhu yake.

Nadharia hii ilinuia kudhihirisha na kufafanua kadhia zinazomkutanisha msomaji na kazi ya fasihi. Hii ina maana kuwa kila kazi inayosomwa huibua jambo fulani kwa msomaji husika. Murfin (1991) akieleza fikra za Adena Rosmarin, kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na hivyo mchongaji wa kinyago hiki hujaribu kukikamilisha. Anasema kuwa, msomaji wa kazi ya fasihi huikamilisha kazi anayosoma kwa kuitolea maana kutegemea tajriba yake, mazingira yake, mtazamo wake na msimamo wake. Kupitia usomaji wa kazi teule, mtafiti aliweza kudondoa visababishi, athari na suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kutokana na kazi kuu ya mwandishi.

Wahakiki na wataalamu ambao walizingatia mwelekeo wa nadharia hii huamini kuwa msomaji wa kazi maalum ndiye huamua maana inayojitokeza katika kazi hiyo (Wamitila, 2002). Mtazamo huu humpa msomaji hadhi kuu kwa sababu humsawiri msomaji kuwa mwenye mchango wa juu katika ubunifu wa maana katika kazi husika.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), kazi za fasihi huwa na athari kwa mwandishi na athari hizi hufasiriwa na wasomaji tofauti kupitia njia mbalimbali. Waitifaki wa nadharia hii hushikilia kuwa kazi ya fasihi hupata maana baada ya matini na msomaji kuathiriana kwani msomaji ndiye huipa maana kazi ya fasihi kwa kuiona na kuilinganisha na uzoefu wake wa maisha. Kila kazi ya fasihi huwa na maana ya kipekee kwa kila msomaji binafsi kutokana na tajriba yake maishani, kiwango chake cha elimu,

historia yake, mazingira yake na pia msimamo na mtazamo wake katika maisha. Kupitia kusoma hadithi fupi teule ambazo zimeandikwa na mtazamo wa waandishi na tajriba zao maishani, mtafiti aliweza kutagusana kupitia usomaji wa kazi hizi na kuzipa maana ya kuangazia visababishi, athari na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kuongozwa na tajriba na mazingira halisi katika jamii.

Mihimili ya nadharia hii ambayo iliongoza utafiti huu ni kama ifuatayo:

i) Kuna uwiano kati ya maana ya kazi inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki. Mhimili huu ulisaidia katika kuchunguza maana ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kutokana na kazi asilia za waandishi wa kazi teule za Kiswahili. Kwa hivyo, kazi za waandishi hawa ndizo zilichangia kuibuka kwa maana ya ufasiri wa mtafiti wa visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

ii) Kila kazi ya fasihi ina maana kulingana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia. Mhimili huu ulimpa mtafiti uhuru wa kufasiri kazi teule kwa namna yake ya kipekee ya kudondoa athari ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Usomaji na upokeaji wa kazi za fasihi unaweza kuathiriwa na matakwa ya kisiasa, kijamii na kibinafsi (Greenblatt, 1980). Hii ina maana kuwa mazingira huathiri upokeaji wa kazi za fasihi. Pia, kila msomaji atakuwa na maana ya kazi ya fasihi kutegemea kipindi ambacho anasoma kazi ile. Utafiti huu ulijikita katika kipindi ambacho jamii imekumbwa na ongezeko la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni miongoni mwa watoto na hivyo kufasiri kazi teule kwa mkondo huo.

iii) Msomaji hutumia vigezo fulani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kutumia kigezo cha maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika kazi teule ili kufanikisha utafiti huu kwa wanajamii ambao ni waathiriwa wa jambo hili. Maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni yalitumika ili kujadili suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Utafiti huu ulihusu usomaji na ufasiri wa kazi teule za Kiswahili kuhusu uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kuangalia visababishi, athari na suluhu yake. Katika utafiti huu, mtafiti alizingatia kuwa nadharia hii inafaa katika usomaji na utafsiri wa

kazi teule za Kiswahili kwani msomaji hafai kufungwa kwa msimamo wowote wa namna ya kuipokea kazi ya fasihi.

## 1.10 Mbinu za Utafiti

### 1.10.1 Utangulizi

Sehemu hii ilielezea mbinu za utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, njia za kukusanya data, namna ya kuchanganua data, uwasilishaji wa data hiyo na maadili ya utafiti. Sehemu hii ni muhimu kwa sababu ilitoa picha kamili ya utafiti mzima kwa kueleza namna data ilivyopatikana.

### 1.10.2 Utafiti wa Maktabani

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Maktaba za vyuo vikuu kama vile Chuo Kikuu cha Chuka, Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha Nairobi zilitumiwa. Vyuo hivi viliteuliwa kwa sababu vilikuwa rahisi kufikika na hivyo kupunguza gharama kubwa ya utafiti. Hadithi fupi teule katika diwani za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007), na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016) zilisomwa na kuchanganuliwa kwa kina. Vitabu, magazeti, majarida, tasnifu na maandishi mbalimbali pia yalisomwa ili kutafuta maelezo yanayohusiana na utafiti huu. Kazi mbalimbali zilizopatikana kwenye mtandao pia ziliauliwa ili kupata yaliyomo kuhusu utafiti huu.

### 1.10.3 Uteuzi wa Sampuli

Fasihi andishi ya Kiswahili ina utanzu wa riwaya, hadithi fupi, tamthilia, novela na ushairi. Waandishi wa kazi hizi huwa wamesukumwa na jambo fulani ili kufanya utunzi wao na hawafanyi uandishi kutoka kwa ombwe tupu. Mwandishi huzungumzia masuala ambayo yanamwathiri au yanaiathiri jamii yake kwani huwa anayaakisi mazingira yake, historia yake, falsafa yake na hisia za kibinafsi kupitia ile kazi anayoitunga. Mtafiti aliongozwa na utanzu wa hadithi fupi ambao huwa unachukua muda mfupi kuisoma hadithi moja na kung'amua yaliyomo kwa haraka. Hadithi fupi huzunguka tukio moja kwa kumtumia mhusika angalau mmoja mkuu katika kipindi maalum na hivyo kuibua athari ya moja kwa moja kwa msomaji (M'ngaruthi, 2019).

Diwani nne za hadithi fupi zilizingatiwa. Diwani hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa kuwa zilikuwa na hadithi fupi zenye maudhui ya kumpa mtafiti data ya utafiti huu. Diwani hizi ni: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007*), Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007), na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Hadithi mahsusi nazo zilizoandikwa na waandishi tofauti ambao wana falsafa tofauti kuhusu visababishi, athari na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ziliteuliwa kutoka kwa diwani hizi. Maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ndiyo yaliyoongoza uteuzi huu. Hadithi tisa kutoka kwa ujumla wa hadithi sitini na tatu ndizo zilizoteuliwa na kutumika kimaksudi. Hii ni asilimia kumi na nne na hivyo kuwa kiwakilishi tosha cha hadithi fupi katika kuangazia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Hadithi fupi teule zilitoa picha ya moja kwa moja ya utafiti huu kwa kuongozwa na wahusika wakuu katika kazi hizi na mgogoro mkuu wa hadithi husika kama mojawapo ya sifa ya hadithi fupi.

Katika kila diwani, hadithi fupi zifuatazo ziliteuliwa:

Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007)

i) Kanda la Usufi
ii) Mwana wa Darubini

Diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007)

i) Shetani Hana Hatia
ii) Safari ya Maangamizi

Diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007)

i) Malimwengu
ii) Shimo la Maisha
iii) Namchukia Babangu

Diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016)

i) Shogake Dada ana Ndevu
ii) Mame Bakari

Kazi hizi ziliteuliwa kwa kuwa hapa ndipo palipatikana data iliyohusiana na mada ya utafiti huu. Maudhui ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ndiyo yaliyomwongoza mtafiti huku akiegemea katika madhumuni ya utafiti. Hadithi fupi

teule zilizohusu watoto na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zilitumika kuwa kiwakilishi tosha cha kazi zote zenye maudhui haya ili kutimiza malengo ya utafiti.

### 1.10.4 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ya utafiti huu ulifanyika baada ya mtafiti kupata kibali cha kukusanya data na pia kujitambulisha kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kusoma na kuhakiki diwani nne za hadithi fupi. Kila hadithi fupi teule ya Kiswahili ilisomwa kwa kina na yaliyoandikwa kuhusu visababishi, athari na falsafa ya waandishi wa kazi teule kuhusu suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kudondolewa na kunakiliwa. Mtafiti aliongozwa na maswali, madhumuni na nadharia ya utafiti. Vifaa vilivyotumika katika kukusanya data hii ni orodha ya maswali ya utafiti, tarakilishi, diski na kalamu na daftari. Kalamu na daftari zilitumika kunukuu maneno, sentensi, na hoja nyinginezo zilizofaa na kutumika katika utafiti huu. Maneno na vifungu vya maneno vilivyobainisha visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni, athari zake na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyoelezwa na waandishi wa hadithi fupi teule vilidondolewa na kunakiliwa. Tarakilishi ilitumika kupiga chapa na kuhifadhi data ya utafiti huu. Diski pia ilitumika kuhifadhi data hii kwa matumizi ya haraka ilipohitajika. Kazi zingine kama vile vitabu, magazeti, majarida na tasnifu ambazo ziliandikwa kuhusiana na mada pia zilipitiwa kwa makini na kudondoa hoja muhimu. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ilichunguzwa kwa kina kwa sababu ndiyo iliyoongoza utafiti huu.

### 1.10.5 Uchanganuzi wa Data

Baada ya kukusanya data iliyohusu visababishi, athari na suluhu ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule, mtafiti aliichanganua kazi hii kulingana na madhumuni na maswali ya utafiti. Mtafiti alijadili visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni, athari ya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kila kazi teule. Nguzo tatu za Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji zilitumika katika uchanganuzi huu.

### 1.10.6 Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia sura mbalimbali. Maelezo haya yaliongozwa na madhumuni ya utafiti huu. Hapa, mtafiti alibainisha visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika sura moja, athari yake katika sura nyingine na suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa kazi teule za Kiswahili katika sura tofauti pia.

### 1.10.7 Maadili ya Utafiti

Mtafiti aliongozwa na mwongozo wa kimaadili wa Chuo Kikuu cha Chuka katika kufanya utafiti wake. Mtafiti aliwasilisha pendekezo la utafiti huu kwenye kamati ya maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka ili itathmini uasilia wake na kutoa kibali cha kufanyika kwa utafiti. Kisha, mtafiti alituma ombi la kupata kibali cha kukusanya data na pia kujitambulisha kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Vilevile, mtafiti alizitambua kazi za wataalamu wengine kwa kuwanukuu katika marejeleo ya utafiti huu. Ili kudumisha hadhi ya utafiti, data iliyokusanywa iliandikwa na kuhifadhiwa ili kuwa na manufaa kwa jamii na kizazi cha baadaye. Pia, utafiti huu uliweka wazi matokeo yake na kupendekeza mada ambazo zinaweza kutafitiwa baadaye kuhusiana na mada ya utafiti huu.

## 1.11 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia misingi ya utafiti. Alifafanua suala la utafiti na umuhimu wake katika taaluma ya Kiswahili na jamii kwa ujumla. Madhumuni na maswali ya utafiti yalielezwa. Pia, aliziaua kazi mbalimbali zilizojenga msingi imara wa utafiti huu. Nadharia iliyoongoza utafiti ilielezwa kwa kina pia. Mbinu za kukusanya na kuchanganua data zilielezwa. Katika sura ya pili, mtafiti alichunguza historia ya waandishi wa hadithi fupi teule na muhtasari wa hadithi teule.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA WAANDISHI WA HADITHI FUPI TEULE NA MUHTASARI WA HADITHI TEULE

## 2.1 Utangulizi

Historia ya mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi ni muhimu. Hii ni kwa sababu maisha yake huchangia mtazamo na mwelekeo wake katika kazi anayoiandika. Kwa mujibu wa Murfin (1991) akieleza fikra za Adena Rosmarin katika kuifafanua nadharia ya mwitikio wa msomaji iliyoongoza utafiti huu, kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na hivyo mchongaji wa kinyago hiki hujaribu kukikamilisha. Alisema kuwa, msomaji wa kazi ya fasihi huikamilisha kazi anayoisoma kwa kuitolea maana kutegemea tajriba yake, mazingira yake, mtazamo wake na pia msimamo wake. Vivyo hivyo, mwandishi pia ana nafasi kubwa katika kazi anayoiandika. Kazi yake inaweza kuchangiwa na kuathiriwa na mazingira yake na tajriba yake miongoni mwa masuala mengine. Katika sura hii, mtafiti alishughulikia muhtasari wa historia za waandishi wa hadithi fupi teule na muhtasari wa hadithi hizo.

## 2.2 Muhtasari wa Waandishi wa Hadithi Teule na Hadithi Teule

### 2.2.1 Kanda la Usufi

Hii ni kazi ya mwandishi Rhoda Nyaga katika Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Rhoda Nyaga ni mwandishi chipukizi na mwalimu wa Kiswahili. Amefundisha katika shule kadha za upili nchini Kenya.

Katika hadithi hii, Sela ambaye ni mwanafunzi kwenye shule ya upili ya Askofu Timotheo anaanza uhusiano wa kimapenzi na mvulana wa shule ya wavulana ya Lenga Juu aitwaye Chris Masazu. Uhusiano huu unaanza katika siku ya tamasha za muziki na drama za shule za eneo la Mlimani ambazo zilifanyika katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo. Wanafunzi kutoka shule zingine walifika akiwemo Masazu ambaye alikuwa na nia tofauti na ile ya tamasha. Aliandamana na wanafunzi wa shule yake kama shabiki. Alipofika pale, alijifanya kuwa kaugua na kumuomba Sela amsaidie kupata matibabu shuleni mwao. Sela alisalitiwa na moyo wake mwepesi na kuingia kwenye mtego wa Masazu barabara. Sela aliandamana naye hadi kliniki ya shule ambapo alihudumiwa na alipopewa tembe za kutuliza maumivu alizitema kwa kusingizia kuwa na kichefuchefu. Aliomba kutulia kwenye kivuli ili maumivu

yapungue na hapo ndipo alipata mwanya kamili wa kujitambulisha kwa Sela na uhusiano wao ukaanza kamili.

Baada ya siku hii, watoto hawa walianza kuandikiana barua za mapenzi na kuandaa mikutano ya faragha wakati wa likizo za shule na tamasha za shule ilipowezekana. Katika likizo ya mwisho wa muhula wa tatu wa kidato cha pili, Sela alikuwa mjamzito. Hali hii ilithibitishwa katika ukaguzi uliofanyika mwanzoni mwa muhula wa kwanza wa kidato cha tatu kama ilivyokuwa desturi katika shule yao. Sela na wenzake wawili waliokuwa na hali kama yake waliombwa kutolewa katika shule hiyo kwani wasingeendelea na masomo humo wakiwa wajawazito. Sela alijiunga na shule ya kutwa hadi pale siku za kujifungua zilikaribia. Baada ya kujifungua kitoto Kadogo, alikaa nyumbani kwa miezi mitatu kukitunza na kisha kukiacha kwa utunzi wa harati Rozina na kurudi shuleni kukamilisha masomo ya shule ya upili. Kadogo alivishwa matambara kutokana na umaskini uliokuweko kwa akina Sela. Alipomaliza masomo ya shule ya upili, Sela alimtafuta Masazu ambaye sasa alikuwa amekamilisha masomo na kujitafutia kibarua Dafina kilichoweza kulipia chumba kidogo na kununua chakula. Waliishi pamoja kama mume na mke huku Kadogo akibaki na harati yake Rozina.

Kutokana na upweke aliokuwa nao Sela wakati Masazu alikuwa kazini, waliona ni vyema wamuendee mwanao. Usiku mmoja Sela na Masazu waliandamana kumwendea mwanao Kadogo kama mpango ulivyokuwa. Hii ilitokana na kuwa Masazu hangemudu utaratibu wa kawaida wa kuenda kwa wazazi wa Sela.. Hivyo, waliamua kumtorosha usiku kutoka kwa mikono ya Rozina ambaye alihusishwa kwenye mpango huo. Mvua ilikuwa imenyesha usiku huo na kufanya hewa kuwa ya kuchukiza. Baada ya kusubiri kwa muda, walipokezwa mwanao aliyekuwa  amelala kupitia dirisha la nyuma ya kijumba cha Rozina polepole kwani kuamka na kilio chake kungeharibu mipango yote. Sela alimkumbatia mwanao ili kumkinga kutokana na matone mazito ya mvua, hofu ya umeme na ngurumo za radi. Walifika mahali ambapo njia ilikuwa pana na mti ulikuwa umeanguka na kukingama njiani. Masazu alikuwa akiongoza naye Sela akimfuata. Masazu alipata kulikuwa na dimbwi la maji na alipojaribu kurejea upande mwingine, kumbe Sela alikuwa kaelekea pale na kutia mguu majini ambayo yalimzoa pamoja na mwanawe. Masazu mara moja alijichupa mle alimosikia Sela akimwitia.

### 2.2.2 Mwana wa Darubini

Mwana wa darubini ni hadithi ya mwandishi Kristina Mwende Mbai katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Kristina ni mzaliwa wa hapa nchini katika kaunti ya Machakos mnamo mwaka wa 1967. Alipata shahada ya kwanza katika Uandishi wa kibiashara. Ni mwandishi na msomi wa kazi za fasihi.

Hii ni hadithi inayomhusu msichana mdogo aitwaye Kananda ambaye kutokana na uchochole, wazazi wake hawakuweza kumsomesha bali walikaa naye nyumbani. Siku moja ami yake Mbao aliwaletea habari njema kuwa kuna mtu mashuhuri aliyekuwa akimtafuta msichana mfanyakazi jijini Nairobi. Habari hii iliwafurahisha wazazi wa Kananda na yeye mwenyewe. Hivi ndivyo Kananda alivyopata kuwa yaya kwa Bw. Mwatela na Bi Maria kumtunza mwanao Sami. Mwatela alikuwa mlevi na mara alipolewa alipenda kumchokoza Kananda kwa kutaka mapenzi. Siku moja Maria alipokuwa ameenda kuwatembelea wazazi mbali na jiji, Mwatela alimnajisi Kananda kitendo ambacho kilimfanya Kananda kubaini alikuwa mjamzito baada ya miezi miwili. Kananda alipomweleza Mwatela kuhusu matokeo hayo, alimtishia kutomwambia mkewe kwani kwa kufanya hivyo angemuua lakini akinyamaza angemfanya mke wa pili baada ya kujifungua. Alimwambia amwambie Maria kuwa alikuwa ametungwa mimba na rafiki yake wa nyumbani alikotoka. Siku ya kujifungua, Mwatela alimkimbiza Kananda hospitalini na huku nyumbani mkasa wa moto ulitokea na mwanao Sami kuteketea humo na mamake kuchomeka vibaya. Mwatela alipofika nyumbani alimkimbiza mkewe hospitalini.

Kananda alijifungua mtoto wa kiume. Hata hivyo, Mwatela hakumuoa kuwa mke wa pili kama alivyomwahidi na badala yake alifanya njama ya kumuuza kama chombo cha mapenzi kwa dereva wa malori ya shehena kutoka Kongo baada ya kumnyang'anya mwanawe. Dereva huyo alimpeleka Kananda Kongo na kuishi naye kwa miezi sita na kisha kumuuza kama mtumwa kwa mtu mwingine. Baada ya taabu nyingi, Kananda aliokolewa na askofu mzungu na kurudishwa Kenya. Wakati huu wote, wazazi wake Kananda walikuwa wamefahamishwa na Mwatela kuwa Kananda alikuwa ametoweka na asijulikane aliko. Aliporudi nyumbani, Kananda aliwahadithia wazazi yaliyotokea lakini hawangeweza kufanya lolote kutokana na umaskini. Nia yake Kananda ilikuwa kumwona mwanawe Mwakitawa. Alifanya juhudi za kutafuta alikohamia Mwatela na

familia yake na hatimaye kupata kujulishwa na rafikiye Mwatela kwa jina Katana kuwa kahamia Mombasa.

Kutokana na hamu ya kutaka kumwona mwanawe, Kananda alifanya mpango wa kupata darubini ambayo angeitumia kumtazamia mwanawe kutoka kwa nyumba ya Mwatela. Mwakitawa alikuwa amepewa masharti kabambe ya kutotoka nyumbani pekee baada ya Mwatela kujulishwa na Katana kuwa kuna mama anayeulizia kwake anayefanana sana na Mwakitawa. Mwatela alimnunulia Mwakitawa manati ya kumlenga yeyote aliye na nia ya kumteka nyara kama alivyoelezwa na babake. Siku moja, Kananda alipokuwa akimtazama mwanawe kwa darubini kama alivyozoea, Mwakitawa alimfyatua jiwe kichwani kwa kuhofia ni jambazi na kutoroka kujificha nyumbani. Kananda aliumia vibaya sana na wapita njia wakamkimbiza hospitalini. Mwakitawa hakuelewa ni kwa nini baba yake hakumpongeza baada ya kumpa habari ya jinsi alivyomfyatua yule mama.

Baada ya wiki mbili, usiku mmoja Mwakitawa aliamshwa na ugomvi kati ya wazazi wake na kumsikia ‘mama’ akifoka kuwa Mwakitawa aitwe mara moja na aambiwe kuwa alikuwa anamuua mama yake mzazi. Punde, Mwatela alipatwa na mshtuko wa moyo na kukimbizwa alikolazwa Kananda kwa matibabu. Alipotoka hospitalini baada ya siku tano, alipata habari kuwa Mwakitawa alikuwa ametoweka nyumbani. Hii ni baada ya Maria kumwambia ukweli kuhusu maisha yake. Mwatela alijuta sana kwa vitendo vyake na kuhofia kuonana ana kwa ana na Kananda. Alimkimbilia wakili wake na barua ya kumuomba Kananda msamaha na kumwambia amwakilishe katika kumtafuta huku akimpa nyumba yake ya kifahari kama malipo ya uovu aliomtendea. Kananda alikubali malipo hayo na Mwakitawa alipojitokeza kutoka mafichoni aliishi na mama yake kwa furaha ambapo masomo yake yaligharamiwa na Mwatela ila hakurudi kwa Mwatela tena.

### 2.2.3 Shogake Dada ana Ndevu

Hii ni hadithi katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Hadithi hii imeandikwa na Alifa Chokocho ambaye jina lake halisi ni Ken Walibora. Marehemu Ken Walibora alizaliwa nchini Kenya mnamo mwaka wa 1965. Alisomea shule za hapa nchini hadi kiwango cha shahada pale chuo kikuu cha Nairobi. Baadaye alipata shahada

ya uzamili na uzamifu katika chuo cha Ohio kule marekani. Hadi kifo chake katika mwaka 2020, Walibora alikuwa mhadhiri katika chuo kikuu cha Riara kutoka mwaka wa 2018. Amewahi kuwa mhadhiri msaidizi katika chuo cha Ohio Marekani na chuo cha Wisconsin-Madison. Pia, alipeperusha habari katika vituo vya runinga na radio hapa nchini. Isitoshe, alikuwa mhariri wa habari na mkalimani. Kutoka mwaka wa 1988-1996 alikuwa mwalimu wa shule ya upili ambapo alifundisha Kiingereza na Kiswahili hapa nchini.

Walibora ni mwandishi shupavu ambaye ameandika vitabu kadha vikiwemo *Siku Njema, Kufa Kuzikana, Kidagaa Kimemwozea* na vinginevyo. Ni mwandishi na mhariri wa hadithi fupi kama vile *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Hivyo, Walibora ni mwandishi mwenye uwezo mkubwa wa kubuni hadithi hasa za Kiswahili.

Katika hadithi hii ya Shogake Dada ana Ndevu, Safia alikuwa binti yake Bwana Masudi na Bi. Hamida. Wazazi hawa walimuona binti yao kama malaika na wala si binadamu. Walimsifu kila mara. Walioingia kwao pia walimsifu kwa jinsi alivyokuwa msaidizi kwa wazazi pale nyumbani. Shuleni pia alikuwa hodari kwani aliibuka wa kwanza kwa kila mtihani. Pia, alijulikana kuwa mcha Mungu.

Kwa muda sasa, Safia alikuwa akiwaomba wazazi wake ruhusa ya kumleta shoga yake Kimwana ili wadurusu naye masomo ili kujiweka tayari kwa mtihani wa kuingia kidato cha kwanza. Wazazi waliitikia ombi hili wakisema hawana cha kuogopa kwani mwanao hujilinda mwenyewe na wala halindwi. Hawakuwa na pingamizi kwa Kimwana pia kwani mwanao mwaminifu alikuwa amewaambia kuwa hana neno.

Walikitumia chumba cha Safia kwa masomo yao. Walipoanza masomo waliombwa kuufunga mlango kwa ndani wasiweze kusumbuliwa na dada yake mdogo Lulua wala wazazi kuwashughulisha na kukatiza majadiliano yao. Walijitayarisha na kufaulu katika mtihani ule.Hata hivyo, miezi sita ilipopita baada ya Safia na Kimwana kuufanya mtihani wao, Hamida alianza kuona dalili zisizo za kawaida kwa mwanao, kutapikatapika na kunyong'onyea. Hakutaka kuamini yaliyoweza kuwa kisababishi ila alianza kumlaani na kumkemea shetani aliyemletea mawazo hayo. Hata hivyo ilibidi

amuulize mwanao ambaye alisema kuwa alikuwa akiugua homa ya malaria. Mamake alipomdadisi zaidi aliamka akifoka na kuelekea chumbani mwake kwa kudai kuwa mama anamfikiria mabaya licha ya kujilinda kwake. Bwana Masudi alimhakikishia bibi yake kuwa jambo alilolifikiria haliwezi kamwe kuwa la ukweli.

Siku moja Lulua alipokuwa na wazazi wake aliwahadithia mambo yalivyojiri siku moja ambayo hawakuwa nyumbani. Rafiki yake alikuja nyumbani wacheze. Walicheza mchezo wa kujificha ambapo Lulua alitafuta mahali mwafaka mwa kujificha asionekane akakosa. Hapo ndipo aliamua kujaribu kufungua chumba cha dada yake ajifiche humo. Kwa bahati, kumbe mlango ulikuwa haujafungwa. Alipofungua aliwaona Safia na shogake wamelala kitandani. Pia, aliona shogake dada alikuwa na ndevu. Kumbe, walipokuwa wanahadithiwa hadithi hii Safia alikuwa ameenda kliniki kuavya mimba. Papo hapo, simu ya bwana Masudi ilianza kuitana na alipoipokea alipata ujumbe kuwa ameshakufa wakachukue maiti. Safia ambaye alikuwa amekwenda kliniki kuavya mimba alikuwa amekufa.

### 2.2.4 Mame Bakari

Mohammed Khelef Ghassany ndiye mwandishi wa hadithi hii iliyo katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Ghassany alizaliwa Kisiwani Pemba mnamo mwaka wa 1977.  Alikuwa mwanachama cha Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI), taasisi ambayo ilikuwa na lengo la kukuza na kueneza Kiswahili. Ghassani aliondoka kwenye taasisi hii mnamo 1998 na kuelekea mjini Dodoma kama mpigaji picha katika kampuni ya Bossphoto Fast. Alielekea Dar es Salaam mnamo Julai 2006 kusomea Shahada ya Kwanza katika Habari na Mawasiliano ya umma. Ghassani aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Habari wa Civic United Front (CUF) ambacho ni chama cha upinzani katika ulingo wa siasa nchini Zanzibar. Alihudumu katika wadhifa huo kwa mwaka mmoja kabla ya kurejea TAKILUKI alikoajiriwa kuwa Mhadhiri Msaidizi wa Kijerumani katika Chuo Kikuu cha Taifa, Zanzibar (SUZA). Mbali na kufundisha kozi za Kijerumani, aliaminiwa pia kuwaelekeza baadhi ya wanafunzi wa Diploma katika Ushairi. Alihudumu chuoni SUZA hadi mwanzoni mwa 2009 ambapo alijiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kusomea Shahada ya Uzamili katika taaluma ya Tafsiri. Mnamo Septemba 2010, alitua Ujerumani alikopokezwa mafunzo ya miezi sita kuhusu utangazaji wa ha bari katika Kituo cha Deutsche Welle (DW)

ambacho hupeperusha vipindi na matangazo mbalimbali kwa zaidi ya lugha 30. Ghassani aliaminiwa kuwa mhariri na mtangazaji wa habari za Kiswahili za DW Sauti ya Ujerumani mnamo Februari 2011, nafasi ambayo anaishikilia hadi kufikia sasa. Ghassani alitambua upekee wa kipaji chake katika uchoraji na uandishi tangu akiwa mwanafunzi wa darasa la tano. Katika umri huo mdogo, alianza kutunga hadithi fupi za kusisimua pamoja na mashairi. Anajivunia kuchapishiwa vitabu Andamo: *Msafiri Safarini, Siwachi Kusema: Uhuru U Kifungoni, Kalamu ya Mapinduzi: Mapambano Yanaendelea, Machozi na N'na Kwetu: Sauti ya Mgeni Ugenini*.

Hadithi ya Mame Bakari inamhusu mhusika mkuu Sara ambaye alikuwa mwanafunzi. Sara alibakwa usiku mmoja majira ya saa tatu unusu alipokuwa akirudi nyumbani kutoka kwa masomo ya ziada (twisheni). Kwa vile alikuwa anamwogopa baba yake kwa kumuona mkali, hakuripoti kisa hiki kwake wala kwa mama yake. Alimwona mama yake kama kiumbe asiyeweza kujitetea mbele ya mumewe na hivyo asingeweza kumtetea yeye katika hali hiyo. Alipofika nyumbani alioga kisha akajikomelea chumbani akilia na kuomboleza. Baadaye aligundua kuwa alikuwa mja mzito. Aliona kuwa hali ile ingemsababishia kutengwa na wazazi, marafiki na hata shuleni. Sara alisononeka sana moyoni asijue la kufanya kutatua yaliyomkumba. Hata hivyo alikata kauli kutoiavya mimba ile. Alimwendea shogake wa dhati Sarina amsaidie kuubeba mzigo huo. Sarina alimpokea kama rafiki na wakaahidiana kusaidiana. Kwanza walikubaliana kuuficha ujauzito siku za mwanzo chini ya vazi liitwalo jilbabu akiwa nyumbani na hata shuleni. Hakuna aliyemshuku Sara kwa vazi hili kwani alijulikana kuwa mcha Mungu. Watoto hawa walitiana moyo na kuamua sehemu ya kujifungua kuwa ingekuwa shambani kwa wazazi wake Sarina. Walipoendelea na mipango yao, walimhadithia Beluwa ambaye alikuwa dada na mlezi wa Sarina. Pia, alikuwa daktari wa uzazi. Aliwaahidi kuwapa msaada wake kuhusu ujauzito. Kila mwezi alichukua vifaa vya kupima mimba na kuvipeleka nyumbani kumhudumia Sara kwani walitaka iwe siri kubwa. Baada ya miezi sita ya ujauzito, Beluwa alimtaka Sara aende hospitalini kwa vipimo zaidi ambavyo visingefanyika nyumbani. Alimwambia kuwa ingekuwa siri bado.

Siku ilipofika, Sara na Sarina waliongozana hospitalini kwa dada yao. Sara alipatwa na mshtuko wa ajabu alipowapata wazazi wake hospitalini wakimsubiri. Kuona jinsi

alivyoshtuka, baba mtu aliinuka ghafla na kuanza kumtuliza mwanawe kwa maneno ya kumtia moyo na kumuonyesha vile walivyomjali na kumpenda. Sara alizidisha kilio na wote wakawa na jukumu la kumtuliza. Hapo ndipo alijua kuwa wazazi wake walifahamishwa kila kitu na Beluwa siku tatu baada ya kumhadithia. Hata matibabu yote ya pale nyumbani yalikuwa yakigharamiwa na wazazi hawa. Wote walimsubiri aliyetarajiwa kuzaliwa kwa hamu kubwa. Hatimaye Sara alijifungua mtoto wa kike ambaye walimwita Mame Bakari. Nyumbani kulijaa furaha na sherehe. Hata hivyo, furaha ya Sara haikuwa imekamilika kwani nia yake ilikuwa kumwadhibu baba ya mtoto wake. Alitamani siku hii ingefika. Siku moja akiwa katika mawazo yaya haya, alisikia ghasia na kelele huko nje. Sauti zilisikika zikikata kauli kuwa wamuue mbakaji yule kabla ya polisi kufika. Sara alipochungulia alipata ni jitu lile lile lililombaka. Lilimiminiwa matufali hadi likafa.

### 2.2.5 Namchukia Babangu

Hadithi hii imeandikwa na Iribemwangi P. ambaye ana uzoefu mkubwa katika ufundishaji wa Kiswahili na utunzi wa kazi za fasihi. Mwandishi huyu ana tajriba katika lugha ya Kiswahili kama mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Amewahi kufundisha lugha hii pia kwa wageni katika State University of Zanzibar. Pia, alifanya kazi na Baraza la mitihani nchini Kenya katika sekta ya uandishi. Kwa sasa, Iribe Mwangi ni Professa katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Hadithi yake “Namchukia Babangu” imo katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007).

Mwandishi wa hadithi hii anatueleza kuhusu familia ya mzee Mkata M’mali. Mzee huyu alikuwa mkwasi wa pesa, mifugo na mazao. Kila mwaka alipokea tuzo kwa kuwa mteja wa muda mrefu na mwema katika benki aliyohifadhia pesa zake. Akaunti yake ilikuwa na mamia ya mamilioni ya pesa.

Licha ya utajiri huu, familia yake iliishi maisha ya kubahatisha. Walivaa nguo za mararu na kununuliwa viatu kwao ni baada ya kuhitimu shule ya msingi na kujiunga na shule ya sekondari. Watoto wake hawakupata elimu ilivyostahiliwa kwa sababu mzee huyu hakutaka kuwalipia karo wala kuwapeleka kwenye shule bora. Mwanawe Mafutu alipopita mtihani na kualikwa kujiunga na shule ya kitaifa ya Muungano, alikataa katakata kumlipia karo ya shule hiyo na kumwambia ajiunge na shule ya kutwa ya

Kajinga ambayo ilikuwa umbali wa maili nane kutoka kwake iwapo angetaka kusoma. Mafutu alianza masomo ila hali ilikuwa ngumu kwake. Alimuomba babake amnunulie baiskeli ya kumfikisha shuleni lakini ombi lake lilikataliwa kwa kuambiwa kuwa alikuwa ameyashiba masomo. Hasira zilimpanda mwana huyu na keshoye akapatikana chumbani mwake akiwa mfu kutokana na kujinyonga.

Nduguye mdogo, aliapa kutojiunga na shule ya upili kutokana na yale aliyaona yakitendeka kwa nduguye Mafutu. Alitoroka nyumbani siku iyo hiyo kwa kuiba shilingi mia tano kutoka kwa kibeti cha baba yake na kwenda jiji kuu na kuwa mmoja wa watoto wa mtaani. Baada ya miezi sita, aliwaita dada zake nao pia wakatoroka nyumbani na kwenda kuishi na ndugu yao mjini. Baada ya kutoroka kwa watoto wote, mama yao alipigwa na jitimai na hatimaye kuaga dunia.

Huko jijini, dada mmoja aliyeitwa Kichomi alianza kujirembesha na kuwawinda wanaume ili apate chake. Alikodisha nyumba yake katika mtaa tofauti. Hata hivyo, ilisemekana kuwa alikula tunda lenye dudu baya na kujifia. Dada mdogo alichukuliwa na wazungu ambao walimtunza vyema na kwenda naye ng'ambo. Kijana aliyewatorosha wenzake naye alinufaika na mradi wa kuwasaidia watoto waliorandaranda mtaani na kupelekwa kupata mafunzo ya kuwawezesha kutoa huduma kwa taifa. Alijifunza uhandisi na kupata kazi katika shirika la serikali la National Water Authority. Kisha alijiunga na shirika moja la kimataifa kama mhandisi mkuu wa kanda ya Afrika ya Mashariki na Kati.

Huko nyumbani, baada ya kifo cha mama mzazi, Mzee M'mali alioa mke mwingine ambaye alikuwa tayari na watoto watano, watatu wa kiume na wawili wa kike. Uvumi ulienea kuwa babake wavulana alikuwa tofauti na yule wa wasichana. Mzee huyu na mkewe wa pili walipata watoto mapacha lakini watoto hawa waliaga dunia kutokana na ugonjwa usiojulikana. Baba, mama na watoto wote watano walipatwa na ugonjwa ule ule wasioujua. Walipitana hewani kwenda na kutoka ng'ambo kutafuta matibabu ya ugonjwa huu usiojulikana. Benki aliyohifadhi pesa zake mzee M'mali ilimchukia kwa hali yake ya kutoa pesa kwa wingi.

Siku moja, rafikiye Kichomi alimweleza nduguye jinsi mtoto huyu alivyoapa kulipiza kisasi kwa baba yake. Alipolila tunda baya, alilisambaza kwa familia mpya ya mzee huyu na wote kuangamia. Alianza na mvulana mmoja wa mama wa kambo. Mvulana huyu naye kapeleka kwa dada zake ambao hawakuwa wa baba mmoja naye. Mzee M'mali kwa upande mwingine aliwanyemelea wasichana wale kwa kudai kuwa paka mzee hunywa maziwa ili kujituliza. Hivyo ndivyo ugonjwa uliowasumbua wote ulivyosambaa pale kwa mzee M'mali na familia yake mpya.

### 2.2.6 Shimo la Maisha

Rayya Timammy ni mwandishi wa hadithi hii iliyochapishwa katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007). Timammy ni Mkenya aliyezaliwa mwaka 1965 huko Lamu. Alisomea shule zifuatazo; shule ya msingi ya Lamu, shule ya upili ya Aga Khan na ile ya wasichana ya Coast Mombasa. Alijiunga na chuo kikuu cha Kenyatta kwa masomo ya shahada. Alisoma shahada ya uzamili katika isimu na lugha nyingine za Kiafrika katika chuo kikuu cha Nairobi na hatimaye shahada ya uzamifu katika chuo hicho. Kwa sasa mwandishi huyu ni mhadhiri mkuu katika idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwandishi huyu ameziandika hadithi fupi nyingine kama vile "Uteuzi wa Moyoni", "Umezikumbuka Zabibu", "Kikojozi", "Mifereji ya Machozi", "Haki Yangu Naidai", "Thamani ya Mwanamke" na "Siri ya Mama". Amewasimamia wanafunzi wengi katika uandishi wa tasnifu za uzamili na uzamifu. Amehudhuria kongamano nyingi na kuwasilisha makala mbalimbali.

Shimo la maisha ni hadithi inayomhusu Hamisi na dada yake. Watoto hawa walikuwa mayatima baada ya wazazi wao kuaga dunia na kuachwa mikononi mwa baba mdogo. Baba mdogo aliwatunza vyema kadri ya uwezo wake na pia kuwaelimisha. Hata hivyo, Hamisi alipokamilisha kidato cha nne, babake mdogo alistaafu baada ya kufikisha umri wa miaka hamsini na mitano na hakuwa na akiba yoyote. Baba huyu hakuweza tena kuwasaidia watoto wa nduguye na siku moja aliamua kurudi shambani na akapotelea huko bila kumwarifu yeyote. Dadake Hamisi aliingia katika biashara ya kuuza nguo za mitumba ili amsaidie nduguye kuendeleza masomo. Hamisi alianza muhula wa kwanza katika chuo kikuu vyema. Katika muhula wa pili, dada yake alianza kuugua, nguvu

zikamwishia na biashara ikaanza kuzorota. Msichana huyu alipokuwa anauza nguo za mitumba aligundua kuwa biashara ile haikuweza kukidhi mahitaji yao yote na hivyo ikambidi kujiuza yeye mwenyewe kama mtumba. Ni katika biashara hii ya kujiuza ambapo alijipata taabani kwa kupatwa na ugonjwa wa UKIMWI.

Sasa ilikuwa ni jukumu la nduguye kumkimu. Waliishi katika maeneo maovu kabisa mjini yaliyoitwa Mashimoni kulikokuwa na vyoo vya kuelea. Huku, cha kutia kinywani kilikuwa tatizo kupatikana. Hamisi alitoka katika bweni la chuo kikuu kutokana na gharama kubwa ya kulipia na kuishi Mashimoni ili kumtunza dadake na kwenda chuoni kusoma tu. Alitafuta kazi ya usiku ya kuwakimu ili mchana aweze kuhudhuria mihadhara. Hamisi alitaabika sana katika maisha haya ya elimu na kumtunza dada mpendwa. Mitihani ya muhula wa pili ilimpata akiwa katika hali ya kutopata mwanya wa kusoma. Siku ambayo matokeo ya mtihani huu yalitarajiwa, alirudi nyumbani mapema na kwa bahati mbaya alimpata dada yake kaaga dunia. Jambo hili lilimsumbua sana na kukosa utulivu akilini. Alipokwenda chuoni kutazama matokeo ya mtihani wake, alipata kafeli katika mitihani yote. Alipata barua ya kumfahamisha kuwa asingeendelea na masomo mle kulingana na sheria za chuo kikuu kuhusu mwanafunzi kufeli mitihani yote. Hamisi alituma barua kadha chuoni ili wampe nafasi ya kujitetea. Mwishowe, alipokea barua ya kumweleza ahudhurie kikao cha kujitetea.

### 2.2.7 Malimwengu

Hadithi fupi ya Malimwengu imeandikwa na Mumbo Kenga katika diwani ya *Alidhani Kapata na hadithi nyingine* (2007). Mumbo ni mwalimu, mtaalamu wa Kiswahili na mwandishi. Amefundisha katika shule za upili kwa muda mrefu. Amekuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret kwa muda. Ameziandika kazi mbalimbali za Kiswahili zikiwemo kitabu cha Johari ya Kiswahili (Kidato cha kwanza hadi cha nne), Mwongozo wa Riwaya ya Walenisi miongoni mwa kazi nyingine.

Lozi ni mhusika mkuu katika hadithi hii. Wazazi wake walikuwa wamefariki na akaachwa mikononi mwa shangazi yake Mashaka. Nyanya yake alikuwa hai na aliishi katika eneo lilo hilo na Mashaka. Baada ya kufariki kwa wazazi wake, Lozi alipitia maisha magumu mikononi mwa shangazi Mashaka. Mtoto huyu alifanyishwa kazi nyingi, kunyimwa chakula, kutusiwa na hata kunyimwa nafasi ya kutangamana na

wanawe Mashaka. Isitoshe, alikatiza masomo yake ya shule ya msingi na kuwa kijakazi wa shangazi Mashaka licha ya kuwa na ndoto ya kusoma hadi kufikia chuo kikuu.

Siku moja msichana huyu alikuwa taabani kutokana na njaa kubwa aliyokuwa nayo. Alipatikana chini ya mnazi alikokuwa akijaribu kufikia nazi lakini kutokana na unyonge alianguka na kupoteza fahamu. Nyanya yake alimpata pale na baada ya kumhudumia kiasi aliweza kumweleza kuwa alikuwa anahisi njaa. Bibi huyu alimwandalia mkate wa ndizi, maziwa lala na kumkorogea unga kwenye maji baridi (thumbu). Alipokuwa akila, shangazi Mashaka alifika na kumrushia maneno kuwa alikuwa mvivu kabisa isipokuwa uvivu wa kula tu. Alikigonga kibuyu kilichokuwa na maziwa lala na yote yakamwagika. Hapa ndipo Bibi alipandwa na hasira na kumuomba Mashaka kumwacha Lozi. Lozi aliishi sasa na Bibi na maisha ya kelele na matusi yakamwondokea. Aliendelea kumsaidia shangazi Mashaka kama desturi iwapo wakati mwingine alikatazwa kufanya kazi zile ili asitangamane na watoto wa Mashaka. Basi alifurahia kufanya kazi na Bibi ili kupata hela za kuwasaidia kununua chakula. Muda ulivyosonga, Lozi alitaka kufanya kazi ya kujitegemea na kumsaidia Bibi ambaye alikuwa kazeeka. Pia, alitaka kwenda mbali na mateso ya shangazi Mashaka. Lozi alipomwarifu Bibi kuhusu mpango wake na kumweleza kuwa rafiki yake Furaha alikuwa anaishi mjini na angemsaidia, alikubali na kumuomba amfahamishe shangazi ndipo aende.

Furaha alikuwa ameanza kazi katika Benki ya Biashara mjini  Maunguja. Basi, Lozi alipofika huko alipata kazi mara moja kwani Furaha alikuwa amefanya mipango yote. Lozi alianza kibarua cha kukusanya na kupanga nguo katika kiwanda kimoja cha kushona na kuuza nguo ng’ambo. Baadaye, alifunzwa kukata na kuunganisha nguo na kuwa fundi kamili wa cherahani. Siku zote hizi, Lozi alikuwa akiishi na Furaha. Alijihisi sasa mtaji wake ungetosha kukodi nyumba na akamwomba Furaha kuondoka. Furaha hakufurahishwa na msimamo huu lakini ilimbidi amruhusu. Wasichana hawa waliendelea kutembeleana na kila mwisho wa mwezi Lozi alienda nyumbani kuwajulia hali Bibi na shangazi na kuwapelekea chakula na zawadi. Jambo moja ambalo Furaha hakuwahi kulielewa kumhusu Lozi ni kuwa nyumba aliyoipanga ilikuwa ya kiwango ambacho Furaha na mshahara wake wa benki asingeweza kuilipia seuze fundi wa cherahani. Maisha ya Lozi yalikuwa yamebadilika ghafla alipohamia pale na kuwa ya

hali ya juu. Kumbe msichana huyu alikuwa ameanza uhusiano wa kimahaba na wanaume matajiri ambao walimpa maisha ya starehe.

Mwisho wa mwezi mmoja ulipowadia Furaha alimwendea Lozi ili waandamane hadi nyumbani. Alishangaa kumpata nje amejikunyata na kulia. Vitu vyake vilikuwa vimetapakaa kila mahali. Mkurugenzi mkuu katika kibanda alikofanya kazi Lozi alitoka nje ya chumba kile na kwa hasira kamwambia Furaha amchukue kahaba wake kwani alikuwa amemuaibisha. Lozi alikuwa amepigwa kalamu kazini na kufukuzwa kwa nyumba ile kutokana na tabia yake ya ukahaba. Isitoshe, alikuwa mjamzito. Furaha alifanya mpango na rafiki yake akafika kwa gari na kumsaidia kumwahamishia Lozi kwa nyumba yake. Furaha alimpokea vyema na kumfanya ayaone maisha rahisi. Bibi alipopata ujumbe, alifunga safari hadi mjini kumjulia hali mjukuu wake. Alipofika, mara moja alipatiwa majukumu ya ukunga na kukipokea kitukuu chake salama na kuendelea kutoa mafunzo ya ulezi. Baadaye, Lozi alipata kazi katika kiwanda cha kutengeneza mablanketi mjini mumo humo na sasa aliapa kutojiingiza katika masuala ya mahaba na matajiri.

**2.2.8 Safari ya Maangamizi**

Hii ni hadithi ya Julius Gichamba katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007). Huyu ni mwandishi chipukizi wa kazi za fasihi. Ni msomi, mwandishi na mhariri. Amekuwa akihariri miswada ya Kiswahili kwa makampuni mbalimbali ya uchapishaji jijini Nairobi.

Pendo alikuwa mtoto wa pili na msichana wa pekee katika familia ya mzee Majuto. Katika masomo yake, mtoto huyu alijikakamua vilivyo kupitia maneno ya ushauri kutoka kwa wazazi wake. Alikuwa msichana wa kwanza kutoka kijiji cha Sechu kuhitimu na kujiunga na chuo kikuu cha umma. Hivyo, wanakijiji walikuwa na matumaini makubwa kwake na kumwona kama balozi wao. Matumaini yao yalikuwa yamekatika ghafla waliposikia kuhusu kifo chake.

Siku ya mazishi ilipofika, umati wa watu ulifika kijijini pale. Wanafunzi wa chuo kikuu cha KwenuKwetu alikokuwa anasomea Pendo walifika kwa wingi pia. Ibada ilipoendelezwa na kiongozi wa ibada ile kuuliza iwapo kulikuwa na mtu aliyekuwa na

jambo la kusema, Faridi, rafiki wa karibu wa Pendo alitokea na kijikaratasi mkononi. Alieleza jinsi alipokezwa kijikaratasi kile na Pendo mwenyewe alipomtembelea pale hospitalini siku chache kabla ya kufariki kwake. Pale, Pendo alikuwa ameeleza umma kujihadharisha na maovu ya dunia. Alieleza kuwa alikuwa msichana mwenye heshima zake na alifanya kila juhudi kuhifadhi ubikira wake. Hata hivyo, akiwa mwaka wa kwanza katika chuo kikuu alitendewa unyama na wanaume watano ambao walimbaka mchana wakiwa wamevalia vinyago nyusoni na kumwacha katika hali mahututi. Hata baada ya matibabu, alibaki na athari kubwa ya kisaikolojia kwani alikuwa ameharibiwa maisha yake. Miezi ilivyopita, afya yake ilianza kuzorota na daktari akaagiza apimwe damu. Hapa ndipo alipatikana na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi. Alitamani kufa lakini akaona hawezi kufa peke yake na kuamua kulipiza kisasi na kuwafunza wanaume adabu. Mchana alikuwa mwanafunzi stadi na usiku alikuwa katika harakati za kulipiza kisasi. Aliwanasa wengi bila kujali chochote. Wanafunzi wa shule ya upili, wa vyuo vikuu, madaktari, viongozi wa kisiasa, wahadhiri, walimu, watalii kutoka nchi za mbali, viongozi wa kidini, polisi, walevi, wavuvi, wavuta rukwama, wote hawa aliwaangamiza. Mazishi yale yalikamilika kwa vilio kwani waombolezaji wengi waliokuja kumzika walikuwa wameramba asali, akiwemo kiongozi wa dini, wanafunzi wa chuo kikuu na wengineo.

### 2.2.9 Shetani Hana Hatia

Bitugi Matundura ni mwandishi wa hadithi hii inayopatikana katika diwani ya *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine.* Matundura alizaliwa nchini Kenya mnamo mwaka 1973. Alikulia Kericho na kujiunga na shule ya msingi ya Kipketer na baadaye shule ya upili ya Starehe Boys’ centre. Alijiunga na chuo kikuu cha Moi kwa masomo ya shahada. Alifanya kazi kama mhariri katika kituo cha KBC kwa muda mfupi kabla ya kujiunga na chuo kikuu cha Nairobi kwa masomo ya uzamili katika masomo ya Kiswahili. Kwa sasa ni mhadhiri katika chuo kikuu cha Chuka.

Matundura ni mwandishi wa kazi za fasihi zikiwemo vitabu vya hadithi na hadithi fupi. Ni mwandishi aliyetambulika hasa katika uandishi wa fasihi ya watoto.Ameviandika vitabu vya hadithi kama vile *Sitaki Iwe Siri, Mbwa na Sungura, Mamba Mnafiki, Mtoboa Siri* na vinginevyo. Pia, ni mwandishi wa hadithi fupi kama “Mrithi Nini

Wanangu?” na “Giza la Kumi Kumi”. Isitoshe, ameiandika miswada mbalimbali ya Kiswahili. Kupitia uandishi huu, ametambua matatizo yanayowakumba watoto.

Shetani Hana Hatia ni hadithi fupi inayomhusu mtoto Toto, mtoto wa chekechea ambaye alibakwa na ami yake alipokuwa ametoka kumchukua shuleni. Ami yake Toto aliyeitwa Pakashume alikuwa anafanya kazi kwa kaka yake kama shambaboi. Kaka yake aliona bora amwajiri katika kazi hiyo kwa sababu hakung’amua chochote masomoni na alitaka kumsaidia kwa vyovyote ili aweze kujikimu. Kwa vile visa vya ubakaji wa watoto vilikuwa vimekithiri maeneo walimoishi, wazazi wake Toto walimpa Pakashume jukumu la kwenda shuleni kumchukua mwanao.

Siku moja, Pakashume alimwendea mtoto huyu shuleni, akambebea mkoba wake na kumshika mkono kumwongoza kwenye njia ya kurudi nyumbani. Walipofika karibu na kichaka, Pakashume aliingiwa na uayawani na kumgeukia mtoto huyu wa chekechea asiyejua chochote kuhusu mapenzi. Mtoto huyu alilia kwa sauti akimwita mamake lakini mama alikuwa mbali mjini. Kwa bahati nzuri, wapita njia walisikia sauti ya mtoto huyu ikitoka kichakani na wakafika huko mara moja. Walimpata Toto akiwa hoi huku Pakashume akiwa katika harakati za kuvaa suruali yake ili atoroke. Alijaribu kutoroka lakini aliangushwa na gogo lililokuwa njiani na kuanguka. Waliomtimua walimfikia na kumwadhibu kwa kumchapa vibao. Isitoshe, walimvua suruali na kumkata viungo vilivyomchochea kumbaka mpwa wake. Hapo ndipo polisi wawili walifika na kumwokoa asitiwe tairi. Pakashume alizirai na alipopata fahamu, alijikuta hospitalini akiwa na maumivu makali. Alipodadisiwa na daktari kuhusu kilichomfanya kufanya kitendo kile alimlaumu shetani ila daktari alisisitiza kuwa shetani hana hatia. Pakashume alionekana kujutia kitendo chake cha unyama kwa mpwa wake.

### 2.3 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa waandishi wa kazi teule ulishughulikiwa. Pia, mtafiti alitoa muhtasari wa hadithi fupi teule. Sura hii ilikuwa nguzo muhimu katika kuzishughulikia sura zilizofuata. Baada ya kumtambua mwandishi wa hadithi fupi teule na hadithi teule, sura inayofuata iliangazia msimamo wa waandishi wa kazi teule kuhusu visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

# SURA YA TATU

# VISABABISHI VYA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI

## 3.1 Utangulizi

Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni suala nyeti ambalo limewasumbua wanajamii kwa muda. Hii ni kwa mujibu wa ripoti zinazotolewa mara kwa mara na mashirika mbalimbali na pia vyombo vya habari. Hali hii imechangiwa na visababishi mbalimbali. Kwa mfano, Kiarie (2015) alibaini kuwa mimba za mapema zilisababishwa na tamaduni za watu, msukumo wa wanarika na matumizi mabaya ya mtandao wa kijamii. Ripoti ya Baraza la Makanisa Nchini Kenya (NCCK, 2019) ilionyesha kuwa mojawapo ya kisababishi cha hali hii ni ulegevu wa nidhamu katika jamii. Ulegevu huu umechangia watoto kushiriki mahaba kiholela na wengine kuwa waathiriwa wa mimba za mapema. Takwimu za Baraza la Kitaifa Kuhusu Idadi ya watu (NCPC, 2020) pia zilionyesha kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema zilichangiwa na ufukara ulioko kwenye jamii, ubakaji dhidi ya watoto na ndoa za mapema. Katika sura hii, mtafiti aliongozwa na madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ya kuchunguza mambo mbalimbali ambayo yalichangia uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

## 3.2 Visababishi vya Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Utotoni

Kisababishi ni mtu au kitu ambacho hufanya kitendo fulani kitendeke. Kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni mtu au jambo ambalo linamfanya mtoto kuwa katika hali hii. Watoto ni waathiriwa wa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Waandishi wa fasihi huwa wamesukumwa na jambo fulani lililomo katika jamii ili kufanya utunzi wao. Hii ina maana kuwa uandishi wa kifasihi huwa haumo katika ombwe tupu. Waandishi wa hadithi fupi teule wanaeleza mambo ambayo husababisha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika jamii kama yafuatayo:

### 3.2.1 Ubakaji

Kubaka ni kushiriki ngono na mtu bila idhini yake kwa kutumia nguvu. Huu ni uhusiano wa kimahaba bila hiari ya mtendewa. Suala la ubakaji limekithiri nchini Kenya na kuwaathiri watoto wengi. Hii ni kwa mujibu wa ripoti zinazotolewa na vyombo vya habari mara kwa mara. Washukiwa wa kitendo hiki wamekuwa watu wazima wakiwemo jamaa, marafiki na walimu wanaofaa kuwalinda watoto kutokana na

dhuluma ya aina hii. Ojamaa (2020) alieleza kuhusu mwalimu aliyeripotiwa kumnajisi mwanafunzi mwenye umri wa miaka kumi na mitano katika kaunti ya Bungoma. Wanaume watatu wenye umri wa miaka kati ya 18 na 24 waliripotiwa kuwanajisi watoto wenye umri wa miaka minane, kumi na minne na kumi na saba mtawalio katika kaunti ya Kakamega kama ilivyoripotiwa na Ominde na Chepkemboi (2020). Fasihi ya Kiswahili pia imetumika kuliangazia jambo hili. Waandishi mbalimbali wa kazi teuli wamedhihirisha kuwa ubakaji ni mojawapo ya kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kwa mfano:

Mwandishi Mohammed Ghassany katika hadithi yake "Mame Bakari" amedhihirisha kisababishi hiki katika dondoo hili:

> "Leo ndiyo huyu hapa Sara, mja mzito wa miezi miwili u nusu. Ulikuwa ujauzito wa Jumatano ile. Ujauzito wa kubakwa na kulazimishwa.Wa kuvunjiwa ujanajike na utu wake. Wa kuharibiwa maisha yake" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 47)

Katika dondoo lililonukuliwa, Sara alikuwa mwathiriwa wa kitendo cha ubakaji. Sara alibakwa usiku mmoja wa siku ya Jumatano akiwa anatoka katika masomo ya ziada. Alipokuwa njiani kuelekea nyumbani ndiko alikotendewa unyama huu na jitu asilolijua. Inafahamika kuwa jitu hili lilikuwa na tabia ya kuwabaka watoto katika eneo hilo. Kwa kuwa Sara alikuwa anawaogopa wazazi wake kwani aliwaona wakali sana (hasa baba yake), alipofika nyumbani hakumweleza yeyote kilichotendeka. Badala yake, alikoga na kujikomelea chumbani mwake na kulia. Baada ya muda, Sara aligundua kuwa alikuwa mja mzito, ujauzito alioutunga usiku ule aliobakwa. Kitendo hiki kilimfanya Sara kushiriki ngono akiwa mtoto na pia kutunga mimba utotoni.

Mtoto huyu alipojipata kuwa alikuwa mja mzito, alikumbwa na mawazo mengi. Alijiuliza maswali mengi kwa nini alitendewa kitendo kile. Alitoa wazo kuwa pengine alitendewa vile kwa kuwa yeye ni mwanamke kwani mwanamke huonekana kama kiumbe duni na hivyo suala la ubakaji huenda lisichukuliwe na uzito wowote. Mhusika Sara anaeleza kuwa angethubutu kuwaambia wazazi na jamaa zake kuhusu kubakwa kwake, basi angepokea matusi si haba na kufukuzwa nyumbani kwani kosa la ubakaji ni la mwanamke kama ilivyo kwenye nukuu;

> “Kila siku linapotokezea jambo la mwanamke kubakwa basi mwanamume hana kosa. Mwanamke ndiye shetani” (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 48)

Hali ya watoto kubakwa kwa mujibu wa dondoo hili inatokana na mtazamo duni ambao jamii inayo kumhusu mwanamke. Jamii inamtukuza mwanamume hata kwa vitendo viovu kama hivi vya ubakaji.

Kwa mujibu wa Bitugi Matundura katika hadithi ya “Shetani hana hatia” kwenye diwani ya *Kurudi nyumbani na hadithi nyingine*, anaelezea yafuatayo:

> Kando na ushambaboi, Pakashume alitwikwa jukumu la kwenda shuleni kumchukua binti ya kaka yake aliyeitwa Toto- yaani mpwa wake kutoka shule ya chekechea iliyokuwa karibu na nyumbani. Alipewa jukumu hili kimaksudi kwa sababu ya wasiwasi wa wazazi kuhusu usalama wa Toto.Visa vya ubakaji wa watoto vilikuwa vimekithiri katika mtaa wa Bwagazana. Kutokana na ripoti za vyombo vya habari za mara kwa mara ilielekea kwamba hali ilikuwa vivyo hivyo katika nchi nzima *(Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 60)

Dondoo hili linaeleza hali ya ubakaji wa watoto ilivyokuwa katika mtaa wa Bwagazana na pia kwenye nchi mzima. Jambo hili lilisababisha ukosefu wa usalama. Pakashume ambaye alikuwa shambaboi katika nyumba ya nduguye alitwikwa jukumu la kumwendea mwanao Toto kutoka shule ili kuzuia asipatwe na janga hili. Mwandishi wa kazi hii anaendelea kueleza;

> “Walipofika karibu na kichaka, Pakashume aliingiwa na wazimu ghafula. Akapandwa na shetani. Hisia za kinyama zikamtawala. Akamgeukia ghafula malaika yule asiyejua chochote kuhusu mapenzi” (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61)

Nukuu hii inaonyesha jinsi Pakashume alivyombaka Toto ambaye alikuwa mtoto wa chekechea alipokuwa akitoka kumchukua shuleni. Siku moja, Pakashume alimwendea Toto kama kawaida. Walipokuwa njiani mahali kulikuwa na kichaka, akili ya kinyama ilimwingia Pakashume na kumrukia malaika huyu asiyejua maana ya mapenzi. Ni wazi kuwa kitendo cha ubakaji kinaweza kutekelezwa na mtu yeyote wakiwemo jamaa kama vile Toto alivyobakwa na amu yake Pakashume. Ubakaji wa mtoto Toto ulimsababishia uhusiano wa kimahaba akiwa katika darasa la chekechea.

Katika hadithi ya “Safari ya Maangamizi”, Pendo ni mwathiriwa wa tendo la ubakaji. Nikinukuu:

> Nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza katika chuo kikuu, nilitendewa unyama na wanaume watano. Walinibaka mchana mchana na kuniacha katika hali mahututi...Walionitendea kitendo hiki sikuweza kuwatambua kwani walikuwa wamevalia vinyago kwenye nyuso zao. (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 168)

Nukuu hii inamrejelea msichana Pendo ambaye kufikia siku ya kitendo kubakwa alikuwa bikira. Alibakwa mchana mmoja na wanaume watano ambao walikuwa wamevalia vinyago usoni ili wasiweze kutambulika. Baada ya kutendewa unyama huo alisononeka sana moyoni na hakumwambia yeyote aliyoyapitia. Hatimaye alipatikana na ugonjwa wa UKIMWI uliotokana na kitendo kile. Hali yake ilizidi kudhoofika na alipokuwa hospitalini rafiki yake Farida alienda kumjulia hali. Alimkabidhi wosia ambao angeusoma katika siku ya mazishi yake kuhusu kilichosababisha kifo chake na maisha yake chuoni. Kazi hii inadhihirisha chanzo cha Pendo kushiriki kwenye mahaba kama ubakaji wa kulazimishwa.

Katika hadithi ya “Mwana wa Darubini,” Kananda alinajisiwa na mwajiri wake Mwatela. Hapa ni nukuu:

> Siku moja, Maria aliwatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji. Jioni ya siku hiyo ulevi wa Mwatela ulimtuma kumtia doa Kananda. Kananda alifadhaika sana lakini akaona heri anyamaze. Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha! Baada ya miezi miwili Kananda alibaini kuwa alikuwa na kijusi tumboni. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* 2007,Uk 99)

Kwa mujibu wa kazi hii teule, ubakaji unasababisha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kwa watoto. Hii ni kupitia kunajisiwa na waajiri ambao wanawaajiri watoto. Kananda alikuwa mtoto mdogo wa umri wa shule ambaye hakuwa shuleni kutokana na umaskini wa wazazi wake. Alipata kazi kwa Mwatela kama kijakazi ili kuwasaidia wazazi wake kujikimu. Siku moja Maria (bibiye Mwatela) alisafiri kuwatembelea wazazi wake mbali na jiji. Mwatela alimnajisi Kananda kitendo ambacho kilimfanya msichana huyu kuwa mja mzito angali mdogo. Hili ni dhihirisho la baadhi ya dhuluma ambazo waajiriwa watoto hukumbana nazo mikononi mwa waajiri wao.

Kutokana na dondoo hizi, imebainika kwamba watoto hujipata kushiriki mahaba utotoni kutokana na ubakaji. Ubakaji huu huwafanya baadhi yao kuwa wajawazito katika umri huo mdogo. Suala la ubakaji linawekwa wazi ili dhuluma hii dhidi ya watoto iweze kushughulikiwa kwa kuitafutia suluhu mwafaka. Pia, ijulikane kuwa watoto wengine hunajisiwa na kunyamazia kitendo hiki kwa sababu ya kukosa mtu wa karibu ambaye wanaweza kumweleza yaliyotokea. Kwa hivyo, wakati umefika kwa familia na jamaa kuwa rafiki wa karibu wa watoto wao ili kuwasaidia watoto moja kwa moja wanapokumbana na jambo kama hili na kutoa ripoti kwa vyombo vya usalama. Ushirikiano huu ukikosekana katika jamii, kuna uwezekano wa kuwahatarisha watoto kupitia ubakaji.

### 3.2.2 Ukali na Ukatili wa Wazazi na Walezi

Uhusiano mwema na uelewano kati ya mzazi na mwana ni jambo muhimu katika maisha na ujenzi wa familia. Wakati mwingine wazazi wanaweza kuwa wakali hadi kiwango cha kuogopwa na watoto. Katika hali hii, watoto hushindwa kuwaeleza mambo wanayoyapitia ambayo pengine wanaweza kuwa na uwezo wa kuyatatua. Wazazi pia wanapokuwa na mtazamo duni kumhusu mtoto wa kike kwa kuongozwa na tamaduni potovu huwaathiri watoto wale. Hali hii huchangia watoto kujihusisha na mahaba ambayo huweza kusababisha mimba za utotoni.

Katika hadithi ya "Mame Bakari" mwandishi amebainisha kisababishi cha mimba ya mapema kama inavyojitokeza katika kifungu kifuatacho:

> Angepasuka kwa ukali tu. 'Taadabu! Kisirani mkubwa we! Wende ukafanye uchafu wako huko, halafu utujie na uwongo wako usio kichwa wala miguu. Ati umebakwa! Nani akubake wewe? Wapi utakapobakwa mji huu pasiwe na mtu wa kukuombea? Bado mtoto wewe unatarajia mimi mtu mzima na adabu zangu nihadaike na balaa yako?' (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 48).

Kwa mujibu wa kifungu hiki, inabainika kwamba mojawapo ya visababishi vya mimba za mapema ni ukali na ukatili wa wazazi hata pale mtoto ametendewa kitendo kiovu kama vile cha kubakwa. Ukali na ukatili ambao Sara alimhusisha baba yake nao ulimfanya kutokiripoti kitendo alichotendewa akitoka katika masomo ya ziada. Sara alibakwa usiku mmoja alipokuwa akitoka katika masomo ya ziada. Anaeleza kuwa baba yake hangetaka kuelewa kweli kuwa amebakwa bali angemfokia kwa ukali. Isitoshe, Sara aliona kuwa angefukuzwa nyumbani bila huruma kwani hata mama yake

mwenyewe hangeweza kumtetea kama asivyoweza kuitetea nafsi yake mbele ya mumewe. Alikuwa na taswira ambavyo angefukuzwa shuleni kwa kuambiwa kuwa shule ni ya wasichana na wala si ya akina mama alipobainika kuwa ni mjamzito. Aliona kutengwa katika maisha yake na wote waliotarajiwa kumsaidia. Hivyo, Sara aliamua kunyamazia kitendo kile. Alipofika nyumbani alikoga na kujifungia chumbani akilia. Mtoto huyu aliiona jamii yake kuwa yenye taasubi ya kiume ambapo suala la ubakaji lingesukumiwa mwanamke kuwa mwenye makosa na kumwona mwanamume kama kiumbe asiye na doa. Kwa mfano:

> “Kila siku linapotokezea jambo la mwanamke kubakwa basi mwanamume hana kosa. Mwanamke ndiye shetani” (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 48).

Nukuu hili linadhihirisha jinsi jamii ilivyomlaumu mwanamke na kumtukuza mwanaume hata kwa matendo maovu kama ya ubakaji. Kosa lilielekezwa kwa mwanamke na kumuona mwanamume kama kiumbe asiye na hatia.

Katika hadithi ya “Malimwengu” kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kinabainika kupitia mhusika Lozi. Nikinukuu:

> Lozi alikuwa na ndoto ya kusoma hadi kufikia chuo kikuu, lakini wazazi wake walipofariki na kuachwa mikononi mwa shangazi Mashaka, ndoto yake iliyeyuka kama barafu hasa wakati alipokatishwa masomo ya shule ya msingi na akawa kijakazi wa shangazi Mashaka. Sasa alijihisi kuwa alihitaji kufanya kazi ili aweze kujitegemea na amsaidie Bibi kuendeleza maisha hususan katika siku hizi zake za mwisho na pia aweze kujiepusha na mateso ya shangazi Mashaka. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 30)

Kulingana na kifungu hiki, Lozi alikuwa mtoto yatima baada ya kufiwa na wazazi wake. Alibaki kwa shangazi Mashaka kama mlezi wake. Aliachia masomo katika shule ya msingi ili aendelee kufanya kazi kwa shangazi yake aliyemlea kwa mateso mengi kama vile kumnyima chakula, kumfanyisha kazi nyingi na ngumu na pia kumnyima utangamano na wanawe. Lozi alichoka na mateso haya na akaamua kuenda kutafuta kazi mjini ili kujikimu na kumsaidia Bibi (nyanya) ambaye alikuwa sasa mzee na mtetezi wa haki zake.

Lozi alitaka kutoka pale nyumbani ili kujiepushana na ukatili huu wa shangazi yake. Alipofika mjini kwa usaidizi wa rafikiye Furaha aliyekuwa anafanya kazi katika Benki

ya Biashara, alipata kibarua cha kukusanya na kupanga nguo katika kiwanda cha kushona na kuuza nguo ng'ambo. Waliishi na Furaha katika chumba kimoja hadi pale aliamua kuenda kujikodishia chumba chake ambacho kilimshangaza Furaha kwani hangeweza kukilipia na mshahara wake wa benki. Ukweli wake ulijulikana pale siku moja Furaha alipomwendea mwisho wa mwezi waende nyumbani kama kawaida yao. Alimpata kajikunyata nje huku vitu vyake vimetapakaa kila mahali. Alikuwa analia kwi kwi kwi. Kisha mtu alitoka ndani ya nyumba. Hapa ni nukuu;

> Sura iliyotokea ilikuwa ya Mkurugenzi Mkuu wa kile kiwanda alikofanya kazi Lozi. Yule ndiye mtu Furaha aliyezungumza naye hadi akapata kazi. Bwana Mark Pacha, kwa jina. Furaha alimsabahi Pacha kwa heshima na hata kabla ya kudadisi kulikuwani, Pacha alianza kufoka,
> "Mchukue huyu kahaba wakoupelekee watu wengine. Mimi ninamsaidia, naye kazi yake kuniaibisha." (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 32)

Dondoo hili linaonyesha vile Lozi alitimuliwa kazini baada ya kugundulika kuwa alikuwa amegeuka kuwa kahaba kwa kujihusisha mahaba na wanaume matajiri. Isitoshe, Lozi alikuwa pia mjamzito. Ujauzito wa Lozi ulisababishwa na kuacha shule angali mdogo kitendo kilichochangiwa na ukatili na mateso ya shangazi Mashaka. Alijihusisha na mahaba ili aweze kupata kipato cha kujikimu mjini. Hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa watoto ambao wanafaa kuwa shuleni wanakuwa huko licha ya changamoto zozote za kimaisha. Elimu ya mayatima ishughulikiwe kikamilifu hadi watimize ndoto zao.

### 3.2.3 Mazingira na Majira Mabaya

Mazingira ni mahali ambapo shughuli fulani hufanyika. Mazingira wazi ni muhimu na salama kwa maisha ya binadamu ikilinganishwa na mahali yaliyo fiche ambayo yanaweza kuchangia maovu katika jamii. Mazingira hayo hatari ni mabondeni, vichakani, mwituni, vibandani, kwenye mahame na vichorochoroni. Majira kwa upande mwingine ni saa maalum kama asubuhi, adhuhuri, alasiri, jioni, usiku na alfajiri. Usiku huwa ni majira ambayo shughuli nyingi zimekomeshwa na watu wachache wanapatikana nje. Usalama katika majira haya si mwema mno ikilinganishwa na mchana. Mazingira fiche na majira ya usiku yamechangia maovu katika jamii yakiwemo uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Matheka (2018) alionyesha maeneo ambako wanafunzi hupata mimba kwa wingi kwa kubaini kuwa visa vingi

hutokea katika maeneo ya mashambani ambako wakaazi ni maskini Waandishi wa hadithi fupi teule wana haya ya kusema kuhusu mazingira na majira mabaya:

Katika hadithi ya "Mame Bakari" mwandishi anaangazia majira ya usiku yalivyochangia uhusiano wa kimahaba na mimba ya mapema. Kwa mfano:

> "Ilikuwa ni Jumatano moja ya bahati mbaya kwake. Majira ya saa tatu unusu usiku. Alikuwa akirudi darasa la ziada." (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 47)

Nukuu hili linamrejelea mhusika Sara ambaye alikuwa akitoka masomo ya ziada mnamo saa tatu unusu usiku. Kutokana na kuwa njiani pekee yake katika majira yale, yafuatayo yalitokea:

> "Leo ndiyo huyu hapa Sara, mja mzito wa miezi miwili u nusu. Ulikuwa ujauzito wa Jumatano ile. Ujauzito wa kubakwa na kulazimishwa.Wa kuvunjiwa ujanajike na utu wake. Wa kuharibiwa maisha yake" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 47)

Kwa mujibu wa dondoo hizi Sara alihusishwa kimahaba kwa kubakwa alipokuwa akitembea majira ya usiku na kusababishiwa kuwa mjamzito. Mtoto huyu alikuwa njiani saa tatu usiku akitoka masomo ya ziada bila ulinzi wowote. Usiku huwa wakati ambao si bora kwa mtoto kutembea pekee yake bila ya ulinzi mwema kutoka kwa wazazi au mtu anayeaminika. Tukio hili linatupa funzo kuwalinda watoto wa kike kwa kuwapa ulinzi unaostahili hasa nyakati za usiku.

Mwandishi wa hadithi ya "Shetani hana Hatia" anadhihirisha jinsi uhusiano wa kimahaba utotoni unavyosababishwa na mazingira mabaya. Kwa mfano:

> "Walipofika karibu na kichaka, Pakashume aliingiwa na wazimu fulani. Akapandwa na shetani. Hisia za kinyama zikamtawala. Akamgeukia ghafula malaika yule asiyejua chochote kuhusu mapenzi." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61).

Dondoo hili linamrejelea Pakashume ambaye alimbaka mpwa wake Toto alipokuwa anatoka kumchukua kutoka shule ya chekechea iliyokuwa karibu na kwao. Pakashume aliingiwa na unyama fulani walipofika karibu na kichaka. Kichaka ni mahali penye miti mingi na hivyo kuwa na mandhari ya kisiri. Pakashume alipofika mahali pa kichaka alipaona pangemfaa kutekeleza kitendo chake pasi kuonekana. Hapo ndipo alimgeukia mpwa wake na kumbaka.

Isitoshe, mwandishi Alifa Chokocho katika hadithi ya "Shogake Dada ana Ndevu" amezungumzia suala hili la mandhari. Safia mwanawe Bwana Masudi na Bi Hamida alikuwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Aliwaomba wazazi wake nafasi ya kumleta rafiki yake wa kiume aliyeitwa Kimwana wadurusu pamoja kwa ajili ya kujiweka tayari kwa mtihani wa kujiunga na kidato cha kwanza. Safia alipewa nafasi hii bila pingamizi yoyote. Watoto hawa walipata mwanya bora wa kufanya mambo yao kisiri kama kujihusisha kimahaba bila kuonekana wala kufikirika na yeyote. Kutokana na jinsi wazazi wake Safia walivyomwamini mwanao na rafiki yake, waliwapa hata ruhusa ya kudurusia kwenye chumba cha Safia. Waliwaomba kufunga mlango mara tu waingiapo ili dada yake Lulua asiye akawasumbua. Wazazi pia hawakutaka kuwashughulisha walipokuwa kwenye majadiliano yao. Hali ilikuwa hivi:

> Si mama, baba au Lulua, kile kidugu chake Safia, wanaoingia chumbani wawili Safia na Kimwana wanapokuwa na kazi yao humo. Hawaingii humo kwani hawataki kuwashughulisha au kuyakata majadiliano ya masomo yao. Basi hatimaye walimwambia Safia wafunge mlango wao kwa ndani, maana mara kadhaa Lulua alitaka kuingia ndani humo kuwasumbua bure. Naam, mlango ulifungwa kila siku, kila Kimwana alipokuja kudurusu na mwenzake Safia. (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* 2016, Uk 32)

Dondoo hili linadhihirisha vile mandhari ya kujifungia mle chumbani kwa watoto hawa wa jinsia tofauti ulivyowafanya kuyatumia kushiriki mahaba jambo ambalo lilichangia pia mimba ya utotoni. Siku moja Lulua anawasimulia wazazi wake kuwa kuna siku hawakuwa nyumbani na walikuwa wakicheza mchezo wa kujificha na rafiki yake na akakosa mahali bora pa kujificha asionekane. Aliamua kwenda kujificha chumbani mwa Safia ambako Safia na Kimwana walikuwa wakisomea. Aliona ajaribu kufungua mlango wa chumba hiki na kumbe mlango ulikuwa haujafungwa. Aliwapata kalala kitandani na kumwona shogake dada akiwa na ndevu. (Uk 34-35)

Hapa ni wazi kuwa watoto hawa walikuwa na uhusiano wa kimahaba yaliyochangiwa na mandhari fiche ya kujifungia chumbani licha ya kuwa wa jinsia tofauti. Mandhari kama haya yanafaa kukomeshwa na wazazi na walezi kwa kuwapa watoto mawaidha mwafaka. Watoto wanafaa kuelekezwa namna ya kuhusiana na watoto wa jinsia tofauti ili kuzuia madhara kama ya kujihusisha mahaba wangali wadogo. Pia, athari za mandhari yasiyo wazi zinafaa kutolewa waziwazi.

Majanga yanayosababishwa na watoto kujipata katika mahali pa siri pia yamefafanuliwa katika hadithi ya "Kanda la Usufi". Sela alikuwa mwanafunzi wa kidato cha pili. Alianza uhusiano wa kimahaba na Chris Masazu ambaye pia alikuwa mwanafunzi katika shule jirani. Uhusiano huu ulianza katika tamasha za muziki na drama pale shuleni mwa akina Sela. Baada ya siku hiyo, Sela na Masazu walianza mawasiliano kupitia barua na kupanga mikutano ya kisiri wakati wa likizo na katika mikutano ya shule walipopata nafasi. Kwa mfano:

> "Sela na Masazu walifanya mazoea ya kuandikiana barua. Barua zile ziliwasilisha ahadi za kweli na uongo. Barua zile zikawasilisha pia maagano. Mikutano ya faragha ya wapenzi hawa ikafanywa wakati wa likizo za shule na tamasha za shule; nafasi ilipojitokeza." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61).

Kwa mujibu wa dondoo hili, mwandishi anaeleza kuhusu mikutano ya kisiri iliyofanyika na watoto hawa wawili wa jinsia tofauti wakati wa likizo. Katika mandhari haya yalimsababishia Sela kupewa ahadi za uongo na hatimaye yafuatayo yakadhihirika:

> "Muhula wa tatu wa kidato cha pili ulipoanza Sela alijiunga na wanafunzi wengine. Mwezi wa kwanza wa muhula uliisha. Ulipoisha akathibitikiwa na kile alichohofia katika uhusiano wake na Masazu. Kijusi kilikuwa kimetungika! Hapakuwa na nafasi ya kugeuza mambo." Uk 61

Kwa mujibu wa kifungu hiki, mikutano ya mandhari ya siri kati ya Masazu na Sela ilichangia watoto hawa kuhusika katika uhusiano wa kimahaba wangali wanafunzi. Baadaye, uhusiano huu ulisababisha ujauzito utotoni. Hii inabaini kuwa mandhari ya siri ni kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

### 3.2.4 Kutowajibika kwa Wazazi na Walezi

Mayieka (2015) anaeleza kuwa jamii inafaa kuwajibika ili kuweza kuwaelekeza vijana. Kwa hivyo, ni jukumu la wazazi kuwajibikia malezi ya wanao ili kukuza kizazi chenye afya na maadili mema. Watoto wanapokosa mwelekeo mwafaka kutoka kwa wazazi wao huweza kupotoka maishani. Kila mzazi humtakia mwanawe mema na wema huu unafaa kuonyeshwa kutokana na njia bora za ulezi. Hata hivyo, kuna wazazi ambao huwaona wanao kama watu wazima ambao wanajua kila kitu na kuweza kujiamulia mwelekeo bora maishani mwao bila hata kuongozwa. Kwa mfano:

> " Leo, kama siku zote, walimzungumzia binti yao Safia. Kusema kweli, si kumzungumzia tu bali kuchukua fursa ya kumsifu sifa zilizopindukia mipaka, kama vile binti yao si binadamu wa kawaida bali ni malaika wa Mungu" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 29)

Nukuu hili linamrejelea mhusika Safia katika hadithi ya "Shogake dada ana ndevu" ambaye alikosa kuelekezwa vyema na wazazi wake. Badala ya kumfuzwa mwelekeo bora, wazazi wake Safia walimuona kuwa malaika asiye na doa lolote na asiyekuwa na haja ya kulindwa kwani alikuwa na uwezo wa kujilinda mwenyewe. Waliyaamini maneno na matendo yake bila ya hofu kwani walimwona bora kuliko watoto wengine. Walimwamini Kimwana ambaye alikuwa rafiki wa kiume wa Safia na kudhani kuwa alikuwa na tabia njema sawa na mwanao.

Kimwana alikuwa rafikiye Safia wa kiume ambaye walisoma naye darasa moja. Safia alipowauliza wazazi wake ruhusa ya kumleta Kimwana nyumbani wadurusu pamoja walikubali tena kwa haraka kwani walidhani kuwa alikuwa na tabia njema sawa na mwanao. Kulikuwa na lifuatalo la kusema:

> Hilo halikuwa tatizo hata chembe kwa wazazi wake Safia. Acha aje Kimwana-walimwambia, maana hapana cha kuogopa. Safia halindwi, hujilinda yeye mwenyewe. Hujilinda ndani sikwambii nje. Uk 31

Hili ni nukuu linaloonyesha jinsi wazazi wake Safia walivyomwitikia Kimwana kuja kudurusu na mwanao bila kuwaongoza kwa lolote. Walimwona mwanao kuwa asiyehitaji welekezi wowote kwa kuwa angejilinda mwenyewe. Waliwapa watoto hawa idhini ya kukitumia chumba cha Safia kwa masomo yao huku wamefunga mlango wasisumbuliwe na ndugu mdogo wa Safia. Watoto hawa walitumia uaminifu huo wa wazazi wa Safia kujihusisha mahaba chumbani mle. Hatimaye Safia alikuwa mwathiriwa wa mimba ya mapema. Hali hii ilichangiwa na kutowajibika kwa wazazi wa Safia katika kumwelekeza mwanao Safia na jinsi ya kuhusiana na watoto wenzake wa jinsia ya kiume.

Wazazi wake Sara katika hadithi ya "Mame Bakari" walikosa kuwajibika ipasavyo kumlinda mwanao. Sara alitoka katika masomo ya ziada ya usiku pekee yake bila ya ulinzi wowote. Alipokuwa njiani , alibakwa na janadume ambalo lilimharibia ujana na utu wake. Sara aliogopa kuwaambia wazazi wake yaliyotokea kwani aliona kuwa angewaarifu basi lawama zote zingewekwa upande wake. Alifika nyumbani akaoga na

kujifungia chumbani huku akilia na kujidunisha. Hata hivyo ujauzito ulikuwa umetungika. Katika hadithi hii uhusiano wa kimahaba na mimba utotoni ulisababishwa na ukosefu wa wazazi wake Sara kuwajibika katika kumlinda mwanao katika yale majira ya usiku.

Katika hadithi "Namchukia Babangu", Mzee Mkata M'mali hakuwajibika katika malezi bora ya wanawe licha ya kuwa tajiri wa kutajika. Alikataa kuyakidhi mahitaji ya kimsingi ya wanawe jambo lililosababisha mwanawe mmoja kujitia kitanzi na wengine kutorokea jijini kuwa watoto wa mtaani. Mkewe aliaga dunia kutokana na msukumo wa mawazo. Baadaye, alioa mke wa pili. Mwanamke huyu aliolewa na mzee M'mali akiwa na wasichana wawili na wavulana watatu. Watoto wa kike walikuwa wa baba tofauti na yule wa wale wa kiume. Badala ya mzee M'mali kuwaelekeza kama wanawe, alitumia pesa zake kuwa na uhusiano wa kimahaba na wasichana hawa. Kwa mfano:

> "Naye mzee Mkata aliwaendea mabinti wale (hawakuwa wanawe halisi, alijituliza) na kutumia pesa yake akaweza pia kucheza ngoma goya nao (nani alisema kwamba simba mzee asile nyama au paka mzee asinywe maziwa? Alinung'unika mara kwa mara)." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 117)

Dondoo hili linaonyesha jinsi Mzee M'mali alikosa kuwa kielelezo chema kwa wanawe na kuwaadilisha ifaavyo. Hata hivyo, suala la kushiriki mapenzi nao ni la kukosa heshima na kushindwa kuwajibika kama mzazi. Hoja hii inaeleza vile wazazi wengine wanashindwa kuwajibikia malezi bora ya wanao na kuwa chanzo cha kuwadhulumu watoto hao hasa kimapenzi. Pia, ni dondoo linalodhihirisha namna watoto wanavyoshirikishwa kimahaba na watu wa karibu nao wakiwemo wazazi.

### 3.2.5 Shinikizo la Wanarika

Wanarika ni watu ambao wanakaribiana kiumri na kufanya mambo mengi kwa pamoja. Urafiki mbaya baina ya marika ni hatari miongoni mwa watoto. Kiarie (2015) anaeleza shinikizo la wanarika kama kisababishi cha watoto wengi kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba katika eneo bunge la Imenti Kaskazini kwenye kaunti ya Meru, Kenya. Anaeleza kuwa ni katika makundi ya wanarika ambapo watoto hawa hupata nafasi ya kujieleza na kujitambulisha kwa wenzao na kuiga tabia zao ili wasitengwe na wenzao hao. Waandishi wa hadithi fupi teule wanaonyesha jinsi watoto hujiingiza

katika uhusiano wa kimahaba kutokana na msukumo wa watoto wengine wanaoshirikiana nao.

Mwandishi wa hadithi "Kanda la Usufi" anaonyesha kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa kuandika:

> "Hakuwa amepokea barua nyingine kutoka kwa mvulana yeyote. Alikuwa tu akiwasikia wanafunzi wenzake wakizungumzia barua walizotumiwa na marafiki zao wavulana wa shule nyingine. Sasa alikuwa ameipokea barua iliyokuwa imepuliziwa marashi. Aliitunza barua ile kama uhai..." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 61)

Hili ni dondoo linalomrejelea Sela ambaye alikuwa mwanafunzi katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo. Mtoto huyu alikuwa hajui maana ya mapenzi hadi pale aliwasikia wanafunzi wenzake wakizungumzia barua za kimapenzi walizotumiwa na marafiki wa kiume. Siku moja ya tamasha za muziki na drama shuleni mwao, alipatana na mwanafunzi Chris Masazu wa shule ya wavulana ya Lenga Juu. Kutokana na msukumo ambao Sela alipata kutoka kwa wanafunzi wenzake, aliingia kwenye mtego wa Masazu bila kujipa nafasi ya kufikiria na kujizungumzia. Papo hapo, Sela alimpata mpenzi. Alipata pia nafasi ya kupokea barua kutoka kwa mvulana. Sela na Masazu sasa walianza mawasiliano ya barua na wakati wa likizo walipanga mikutano ya faragha. Walipokutana katika mikutano hii yao ya faragha wakati wa likizo, walijihusisha na mahaba na Sela alitambua kuwa alikuwa mjamzito.

Kulingana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa watoto wanaokaribiana kiumri na kutangamana kwa namna moja au nyingine kwa mfano katika mandhari ya shuleni wanaweza kuathiriana. Athari hizi zaweza kuwa ushauri mbaya na kuiga mambo maovu yakiwemo yale ya kujihusisha na mahaba wangali shuleni kama alivyofanya Sela. Watoto wanafaa kuelezwa athari ambazo zinaweza kuletwa na wanarika. Pia, waongozwe namna ya kujiepusha nazo.

### 3.2.6 Matumizi Mabaya ya Likizo

Likizo ni mapumziko anayopewa mtu baada ya kipindi fulani cha kuwa anahudumu au anafanya jambo fulani. Wanafunzi hupewa mapumziko haya baada ya kila muhula ili kupata mwanya wa kupumzisha akili zao kabla ya kuanza muhula mpya. Hata hivyo,

kuna wanafunzi ambao huwa hawajui maana ya likizo na badala ya kupumzisha akili zao hujiingiza katika shughuli ambazo hazina manufaa maishani mwao kwa wakati huo. Shughuli hizi ni pamoja na kujihusisha na mahaba utotoni. Kwa mfano nchini Kenya, likizo ndefu iliyotolewa kwa wanafunzi baada ya kuzuka kwa janga la korona ilisababisha watoto wengi kujiingiza katika mahaba. Wengi wao walijipata wahanga wa mimba za utotoni. Waandishi wa hadithi fupi teule wameangazia matumizi mabaya ya likizo kama kisababishi cha uhusiano wa kimahaba miongoni mwa watoto jambo linalosababisha pia mimba za mapema.

Rhoda Nyaga ambaye ni mwandishi wa hadithi "Kanda la Usufi" ni mmoja wa waandishi walioshughulikia kisababishi hiki cha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Anasema:

> "Mikutano ya faragha ya wapenzi hawa ikafanywa wakati wa likizo za shule na tamasha za shule; nafasi ilipojitokeza." (*Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*, 2007, Uk 61).

Nukuu hili linamhusu Sela ambaye alikuwa mwanafunzi wa kidato cha pili alivyojihusisha na mapenzi na Chris Masazu mwanafunzi wa shule jirani kupitia mikutano ya kisiri wakati wa likizo. Mikutano hii ilisababisha sio tu uhusiano wa kimahaba bali pia mimba ya mapema kwani baada ya muda Sela alikuwa mjamzito, (Uk 61).

Wanafunzi hawa hawakutumia likizo zao vyema na matokeo yasiyotarajiwa yalipatikana wakati usiofaa yaani wangali shuleni. Kutokana na haya, ni vyema wazazi na walezi wafuatilie mitindo ya wanao pale nyumbani wakati wa likizo hili kuepukana na visa vya watoto kujihusisha na mahaba wakati huu. Pia, watoto wanapokuwa shuleni na nyumbani washirikishwe katika shughuli zitakazowafanya kutopata muda wa kurandaranda popote wala kuwa na mikutano hii ya kisiri.

### 3.2.7 Ukiukaji wa Maadili

Maadili ni muhimu katika kuielekeza jamii yoyote au kundi la watu kwani yanapokosekana wanajamii hukosa mwelekeo. Shule pia huwa na maadili yake ambayo sharti yazingatiwe na wanafunzi wote wa shule husika. Ukiukaji wa maadili ni kisababishi cha watoto wengine kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba jambo ambalo limesababisha mimba za utotoni wakiwa wanafunzi. Waandishi wa hadithi fupi teule

wamejadili ukiukaji wa maadili kama mojawapo ya kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kama ifuatavyo:

> "Shule ya bweni ya wasichana ya Askofu Timotheo kwa kawaida ilikuwa na utuvu wa ajabu. Wasichana walitarajiwa kuendeleza shughuli zao kwa utulivu na ustaarabu huku wakizingatia maadili ya hali ya juu" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007,Uk 59)

Hili ni nukuu linalodhihirisha hali ilivyotarajiwa kuwa katika shule ya upili ya wasichana ya Askofu Timotheo alimosomea mhusika Sela. Shule hii ilikuwa na uzingativu wa maadili ya hali ya juu. Hata hivyo, tunawaona wanafunzi wakijiingiza katika uhusiano wa kimahaba wangali shuleni humo jambo ambalo linawasababishia mimba wangali shuleni na kufukuzwa shuleni humo kutokana na ukuikaji wa maadili ya shule. Sera ni mmoja wa wanafunzi ambao hawakuzingatia maadili ya shule hii. Anakuwa na uhusiano wa kimahaba na Masazu ambaye pia ni mwanafunzi katika shule ya wavulana ya Lenga Juu. Muhula wa kwanza katika kidato cha tatu, Sera hakuweza kuendeleza masomo yake katika shule ya Askofu Timotheo. Hii ni kwa sababu katika ukaguza wa ujauzito wa kila muhula kama ilivyokuwa desturi kwenye shule hii ulipata matokeo kuwa yeye na wasichana wengine wawili walikuwa waja wazito. Jambo hili lilichangia kuombwa kuondoka shuleni humo kutokana na hali zao za kuyakiuka maadili ya shule hiyo.

Mwalimu mkuu wa shule hii alipoipata ripoti kuwa wanafunzi watatu walikuwa waja wazito aliwaalika wazazi wao shuleni kuwafahamisha na kuwaelekeza. Katika maelezo yake aliwaambia wazazi yafuatayo:

> "Ingawa sisi hufanya tuwezavyo kuwalinda wanetu, mara nyingi tabia zao hutupiga chenga..." Uk 62

Maneno haya ya mwalimu mkuu yanaonyesha kuwa iwapo kuna maadili yaliyowekwa shuleni au hata katika jamii, kuna wale ambao hawajazingatii. Kwa mujibu wa kazi hii teule, ukiukaji wa maadili katika jamii husababisha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Katika hadithi fupi ya "Namchukia Babangu", mhusika mzee Mkata M'mali aliyakiuka maadili ya jamii. Alikuwa tajiri mtajika katika eneo lake. Hata hivyo alikataa kuwajibikia malezi ya wanawe jambo lililowafanya kutorokea mjini. Mkewe aliaga

dunia kutokana na msukumo wa mawazo watoto wote walipotoka nyumbani. Mzee huyu alioa mke wa pili ambaye alikuwa ameolewa mara kadha. Mwanamke huyu alikuwa na watoto watano, wasichana wawili na wavulana watatu ambapo wasichana hawa walikuwa wa baba tofauti na yule wa wavulana. Mzee M'mali alianza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wasichana hawa kwa nia ya kujiridhisha kingono. Maelezo haya yanaonyesha jinsi mzee M'mali alivyoyakiuka maadili ya jamii na kuwahusisha wanawe kwenye mahaba utotoni.

Katika hadithi hii hii, Kichomi alikuwa mmoja wa watoto wa mzee M'mali aliyetorokea mjini kutokana na ukosefu wa uwajibikaji wa babake. Alipoenda mjini, alianza uhusiano wa kimahaba na wanaume ili aweze kujikimu. Baadaye, mtoto huyu aliambukizwa virusi vya ukimwi. Aliposikia kuwa baba yake alikuwa ameoa mke mwingine, aliamua kulipiza kisasi dhidi ya kitendo hiki. Alianza uhusiano wa kimahaba na wanawe wa mke wa pili wa baba yake kwa nia ya kumuangamiza mzee M'mali na familia yake. Alifahamu kuwa baba yake alikuwa na uhusiano wa kimahaba na wasichana wa mke wa pili na pia wasichana wale walikuwa na uhusiano wa kimahaba na ndugu zao wa kiume. Kwa mfano:

> " Kichomi alielewa mengi kuhusu nyumba ya mzee M'mali. Kwa kuwa ilisemwa kuwa wana wa Bi. Mfuata hawakuwa ndugu halisi, na wao walikuwa wameyasikia hayo mara chungu nzima, hawakuona haja ya kunyimana chochote kile, hata kucheza ngoma goya" (Uk 117)

Kifungu hiki kinadhihirisha namna Kichomi mwanawe Mzee M'mali alivyoyakiuka maadili ya jamii kwa kijihusisha mahaba na watoto wa mama yake wa kambo kwa nia ya kulipiza kisasi. Hii ni dhahiri kuwa uhusiano wa kimahaba wa Sela, M'mali na Kichomi unasababishwa na ukiukaji wa maadili.

### 3.2.8 Ulipizaji Kisasi

Watu mbalimbali huwa na sababu tofauti za kutaka kulipiza kisasi. Hali hii hutokana na uchungu ulioko moyoni kutokana na kutendewa kitendo kisichofaa. Vitendo hivi ni kama kudhulumiwa na kunyimwa haki. Kuna sababu mbalimbali zilizochangia watoto kulipiza kisasi kwa njia ya kujihusisha katika mahaba katika kazi teule. Waandishi wa hadithi fupi teule wana haya ya kusema:

> Sawa, alimchukia sana marehemu Mzee M'mali na kila siku aliapa kuwa angelipiza kisasi, siku moja n'takuja kulifunza jizee hilo

> kilichomnyonyoa kanga manyoya, aliapa. Ikawa hivyo siku baada ya siku (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 117)

Maneno yaliyonukuliwa yanamrejelea mtoto Kichomi katika hadithi ya “Namchukia Babangu” ambaye alikuwa na roho ya kulipiza kisasi kwa baba yake mzee M’mali. Mzee huyu alikuwa mkwasi wa kusifika wa pesa, mifugo na mazao. Hata hivyo aliwalea wanawe kwa maisha ya kimaskini. Kwa mfano wanawe walinunuliwa viatu walipokuwa wanajiunga na shule ya upili. Nduguye Kichomi aliyeitwa Mafutu alipelekwa shule ya upili ya kutwa iliyokuwa umbali wa kilomita kumi ambazo alitarajiwa kutembea kila siku. Hii ni kwa sababu baba yake hakutaka kuharibu pesa zake kumpeleka shule ya kitaifa aliyoalikwa. Alipochoka na kutembea na kuomba baba amununulie baiskeli alikataa kata kata. Mwishowe mtoto huyu alijitia kitanzi. Ndugu zake waliofia haya kutendeka kwao na kutorokea mjini. Basi Kichomi alipofika mjini, aliamua kutafuta chake. Alijiingiza katika uhusiano wa kimahaba na wanaume ili aweze kujikimu. Hatimaye, mtoto huyu aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Siku moja rafikiye Rahma alisimulia hadithi ya Kichomi kwa nduguye ambapo alimweleza jinsi Kichomi alivyomchukia baba yake na kila mara kuapa kulipiza kisasi.

Kichomi alipoambukizwa ugonjwa wa UKIMWI, aliusambaza kwa familia ya baba yake mpya kwa kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi na Mosi, mwanawe mama wa kambo. Mosi kwa upande wake aliupeleka kwa dada zake wa kambo. Dada hawa nao walimsambazia baba wa kambo mzee M’mali ambaye alikuwa na uhusiano wa kimahaba na binti hawa. Kulipiza kisasi kwa Kichomi kuliiangamiza familia mpya ya mzee M’mali kama alivyoapa mara kwa mara kulipiza kisasi.

Katika hadithi ya “Safari ya Maangamizi”, kuna nukuu lililodondolewa kwenye wosia uliosomwa katika mazishi ya Pendo na rafikiye Farida. Ni nukuu linaloeleza jinsi Pendo alipata kushiriki mahaba utotoni kwa kubakwa na wanaume watano mchana mmoja. Hapa ni nukuu hilo:

> “Kumbe licha ya kunibikiri vile vinyangarika vilikuwa vimeniambukiza virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwi? Lo! Nilitamani kufa mara moja. Nilitaka kujitia kitanzi. Lakini nikawaza, nikaona sifi peke yangu. Sharti nilipize kisasi. Nitawafunza adabu wana wa Adamu. Mchana nilikuwa mwanafunzi stadi ilhali usiku nilikuwa katika mstari wa mbele kuona kuwa jamaa wanafagiliwa. Nia yangu haikuwa kupata tija. La hasha! Ilikuwa ni kuwaogesha, kuwanawisha na kuwazamisha wana wa

> Adamu kwenye bahari ambayo tayari walikuwa wameichafua wao wenyewe. (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 169)

Kabla ya yaliyotendeka kwenye nukuu hili mtoto huyu alikuwa bikira. Kule kuvunjiwa ujanajike wake na heshima kulimtia uchungu mwingi moyoni. Isitoshe, baada ya muda Pendo alidhihirishiwa na daktari kuwa walikuwa wamemuambukiza ugonjwa wa ukimwi. Pendo aliona heri kujitia kitanzi na kuondoka duniani. Hata hivyo, alighairi nia yake na kuapa kutokufa peke yake. Aliamua kulipiza kisasi kwa wanaume wote kwani hakuwa na uwezo wa kuwatambua waliomtendea unyama ule kwani walikuwa wamevalia vinyago usoni wasitambulike. Hivi ndivyo alivyofanya Pendo na kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba bila ubaguzi wowote wa kiumri na kitabaka kwa nia ya kuwaangamizi wengi awezavyo. Alishiriki mahaba na wanaume wengi alivyoweza wakiwemo wanafunzi wa shule za upili ambao pia ni watoto. Umbo lake la kutamanika liliwafanya wengi kuomba urafiki naye. Hakuwakatalia. Alikuwa katika safari ya kuwaangamiza. Kwa mfano:

> "Wanafunzi wa shule za upili, wa vyuo vikuu, madaktari, viongozi wa kisiasa, wahadhiri, walimu, watalii kutoka nchini za mbali, viongozi wa kidini, polisi, walevi, wavuta rukwama...wote hawa sasa wanasubiri kutumbukizwa kaburini. Wachimba kaburi mna kazi kubwa!" (Uk 171).

Maelezo haya yanatoa orodha ya watu wa tabaka mbalimbali ambao walikuwa wameangamia kutokana na kujihusisha kimahaba na Pendo ambaye alikuwa katika harakati ya kulipiza kisasi dhidi ya wanaume. Kwa mujibu wa dondoo hizi, kulipiza kisasi ni mojawapo ya kisababishi cha uhusiano wa kimahaba. Katika hadithi hizi mbili, waandishi wanaeleza jinsi watoto walivyoshiriki mahaba kwa lengo la kulipiza kisasi dhidi ya uovu waliotendewa maishani. Uovu huu unatendwa na wazazi na wanajamii wengine. Uamuzi huu wa kulipiza kisasi unawaangamiza waliolengwa kuadhibiwa na wasiokuweko. Hivyo, madhara yake ni mengi. Maovu yanayosababisha kulipiza kisasi ni pamoja na yale ya kubakwa na kuhusishwa mahaba katika umri mdogo kutokana na kutowajibika kwa wazazi.

### 3.2.9 Kukidhi Mahitaji ya Kila Siku

Waandishi wa hadithi fupi teule wanadhihirisha haya katika kazi zao. Baadhi ya watoto hujiingiza katika ukahaba kutokana na umaskini huku wengine wakitelekezwa na wazazi wao wanaojimudu kiuchumi. Mfano:

Kichomi katika hadithi "Namchukia babangu" alijiingiza katika uhusiano wa kimahaba ili aweze kujikimu. Nikinukuu:

> Nako jijini, dadangu mmoja aliyeitwa Kichomi alianza kukoga vizuri na kuwawinda wanaume na hatimaye akapata chake. Alikodi nyumba katika mtaa wa Majengo. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 114)

Msimulizi wa hadithi hii anasimulia jinsi dadake Kichomi alivyotorokea jijini kuwa mtoto wa mtaani baada ya baba yake mzee M'mali kukataa kutekeleza majukumu yake kama baba na kuwalea maisha ya kimaskini licha ya kuwa tajiri mtajika. Baadaye kule mjini, Kichomi alianza kuwawinda wanaume ili aweze kutafuta kipato cha kumkidhia mahitaji.

Kwa mujibu wa nukuu hili, Kichomi alishiriki mahaba angali mtoto kwa nia ya kujikidhia mahitaji yake. Hivyo, mahitaji ya kimsingi ni mojawapo ya kisababishi cha uhusiano wa kimahaba utotoni.

Hamisi na dada yake walikuwa wamefiwa na wazazi na kuachwa mikononi mwa baba mdogo. Baada ya kustaafu, baba mdogo hangeweza kuwatimizia mahitaji yao ya yale ya familia yake. Alitorokea kijijini na watoto hawa wakaachwa pale mjini. Watoto hawa walitafuta namna zote za kujikimu kama ifuatavyo:

> "Katika kule kuuza, aliuza zaidi ya nguo za mitumba kwa kuwa biashara ile haikuweza kukamilisha mahitaji yao yote, ikambidi yeye mwenyewe kuwa mtumba. Katika biashara hiyo alijipata taabani na ugonjwa wa ukimwi." (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 77)

Mfano huu unamhusu dada yake Hamisi ambaye aliamua kuacha shule ili kumwacha nduguye aendelee na masomo na pia kutafuta kipato cha kujikimu yeye na nduguye. Alianza kuuza nguo za mitumba. Alipoona kuwa biashara aliyokuwa nayo ya kuuza nguo za mitumba haikuweza kukamilisha mahitaji yake na ya nduguye Hamisi, alijiuza yeye kama mtumba. Hii ina maana kuwa alianza kujihusisha na uhusiano wa kimahaba na wanaume ili aweze kujikimu pamoja na kumkimu nduguye Hamisi.

Mwandishi wa hadithi ya "Malimwengu" anakieleza kisababishi hiki pia. Lozi alikuwa yatima aliyeachwa mikononi mwa shangazi Mashaka. Kwanza, Lozi aliitupilia ndoto yake mbali alipoachishwa masomo katika shule ya msingi. Alifanyishwa kazi nyingi pale kwa shangazi. Siku moja mtoto huyu aliamua kwenda mjini kutafuta riziki ili

kujikimu mwenyewe na kumkimu nyanya yake aliyekuwa amezeeka. Pia, alitaka kuyaepuka mateso ya shangazi Mashaka. Rafikiye Furaha alimsaidia kufika mjini na kupata kazi ya kupanga nguo katika kampuni ya kushona na kuuza nguo ng'ambo. Hata hivyo, aliamua kuongeza kipato chake kwa kushiriki mapenzi na wanaume matajiri. Mwishowe, mtoto huyu alikuwa mjamzito jambo lililomfanya kuachishwa kazi, (Uk 32).

Hadithi hizi zinadhihirisha kuwa watoto huanza uhusiano wa kimahaba kwa sababu ya kukidhi mahitaji ya kimsingi kama vile mavazi, chakula na makaazi. Hivyo ni wazi kuwa kulingana na waandishi wa hadithi fupi teule, uhusiano wa kimahaba wa Kichomi, dada yake Hamisi na Lozi ulisababishwa na haja ya kujikimu maishani.

### 3.2.10 Uyatima

Kulingana na waandishi wa hadithi fupi teule zilizohakikiwa katika utafiti huu, uyatima unaweza kusababisha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Katika hadithi ya "Malimwengu," Lozi alikuwa yatima ambaye alikuwa mikononi mwa shangazi Mashaka. Mtoto huyu aliachishwa masomo katika shule ya msingi na kuwa kijakazi kwa shangazi Mashaka. Alifanya kazi nyingi pale nyumbani mwa shangazi. Hata hivyo, mateso mengi yalimwandama yakiwemo matusi, kunyimwa chakula na kunyimwa nafasi ya kutangamana na watoto wake shangazi Mashaka. Nikinukuu:

> Lozi alikuwa na ndoto ya kusoma hadi kufika Chuo Kikuu lakini wazazi wake walipofariki na kuachwa mikononi mwa shangazi Mashaka, ndoto yake iliyeyuka kama barafu hasa wakati alipokatishwa masomo ya shule ya msingi na akawa kijakazi wa shangazi Mashaka. Sasa alijihisi kuwa alihitaji kufanya kazi ili aweze kujitegemea na amsaidie Bibi kuendeleza maisha hususan katika hizi siku zake za mwisho na pia aweze kujiepusha na mateso ya shangazi Mashaka. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 30)

Nukuu hili linaeleza maisha ya Lozi yalivyokuwa baada ya kufariki kwa wazazi wake. Kutokana na mateso aliyoyapitia kwa mlezi wake, Lozi alienda kufuta kazi ya kujitegemea mjini kwa usaidizi wa rafiki yake Furaha. Huko mjini ndiko alijihusisha na uhusiano wa kimahaba na wanaume matajiri. Ukahaba huu ulimsababishia kufutwa kazi na pia kuwa mjamzito. Hivyo, ni kutokana na hali ya Lozi kuwa yatima ambapo alipitia mateso mengi yaliyomsababishia kuelekea mjini kutafuta kazi ikiwemo kushiriki mahaba kama njia ya kujichumia.

Katika hadithi ya “Shimo la Maisha” Hamisi na dadake walikuwa mayatima. Walitunzwa vyema na baba mdogo hadi pale alistaafu na kukosa uwezo wa kuwasaidia tena. Baba mdogo alirudi shambani nao wakabaki mjini kwa kujitegemea. Dadake Hamisi alichukua jukumu la ulezi na kuanza biashara ya kuuza nguo za mitumbo ili kuyamudu mahitaji yao. Alipogundua kuwa biashara ile haikuweza kuyakimu mahitaji yao ipasavyo, aliamua kujiuza mwenyewe kama mtumba kwa kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba angali mtoto. (Uk **77)**.

### 3.2.11 Uamuzi Mbaya

Uamuzi anaochukua binadamu katika kulitatua jambo fulani maishani huwa muhimu sana. Uamuzi bora huzuia majuto ya baadaye. Wasichana wengi hujiingiza katika masuala ya mapenzi mapema na wengine kuwa wajawazito kutokana na ukosefu wa kufanya maamuzi bora.

Katika hadithi ya “Mame Bakari,” Sara alifanya uamuzi mbaya wa kunyamaza alipobakwa na janadume akitoka masomo ya usiku. Alifika nyumbani na badala ya kuwaharifu wazazi wake kilichotendeka, alifika akakoga na kujifungia chumbani na kulia. Uamuzi huu ulisababisha msononeka mkubwa hasa wakati aligundua alikuwa mja mzito. Sara angesema yaliyompata pengine angesaidika na matibabu ya dharura na uja uzito ungezuilika. Vile vile, angepata mawaidha ambayo yangemsaidia kupunguza mawazo mengi akilini.

> “Kwa nini hakutoa taarifa ya lile lililompata siku ile? Badala yake alipofika nyumbani, alikwenda kukoga na kujikomelea chumbani kulia na kuomboleza” (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 48).

Uamuzi wa Sara ulimfanya akaishi maisha ya kuwaogopa wazazi wake. Uamuzi mbaya ulikuwa kisababishi cha mimba utotoni ambao ungezuiliwa.

Mhusika Kichomi katika hadithi “Namchukia Baba Yangu” alifanya uamuzi usiofaa. Baba yao mzee M’mali alipokosa kuwajibikia malezi bora kwao, wote walitorokea mjini. Kichomi alijiingiza kwenye uhusiano na wanaume ili kujikimu. Uamuzi huu haukuwa bora kwani hangefanya kazi nyingine ambayo ingemsaidia kujikimu na kuepuka kuutumia mwili wake kama njia ya pekee ya kujikimu.

Sela kwa upande wake katika hadithi "Kanda la Usufi" alifanya uamuzi mbaya wa kujiingiza katika uhusiano wa kimahaba angali mwanafunzi wa shule ya upili ya Askofu Timotheo. Alijihusisha na mapenzi na Masazu ambaye pia alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili katika shule ya wavulana ya Lenga Juu. Hatimaye, alipata ujauzito katika kidato cha pili na ikabidi kutimuliwa katika shule hiyo.

Watoto wanafaa kuelekezwa kufanya uamuzi bora maishani. Hili litapungua majuto ya baadaye. Uhusiano wa kimahaba na ujauzito utotoni utakomeshwe pia. Hii ni kwa sababu maelezo ya hapa juu yanashadidia kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema yanaweza kusababishwa na uamuzi mbaya unaofanywa na watoto kama wanavyoeleza waandishi wa hadithi fupi teule.

### 3.2.12 Matumizi ya Pombe na Dawa za Kulevya

Mwende (2020) alifafanua kuwa kuna ongezeko la visa vya mimba za mapema jambo ambalo lilichangiwa na utumiaji wa dawa za kulevya miongoni mwa visababishi vingine. Kwa mujibu wa utafiti huu, ongezeko la matumizi ya pombe na dawa za kulevya limechangia ongezeko la visa vya ushiriki mahaba. Baada ya vileo hivi, wanaume wengi huwa watoro kiasi cha kushiriki mahaba na watoto. Waandishi wa hadithi fupi teule wanalitaja jambo hili kuwa limechangia uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Dondoo hili linashadidia haya:

> Ulevi huu ulimpeleka Bwana Mwatela katika ngazi nyingine. Alianza kumchokoza Kananda kwa kumtaka mapenzi. Ilimlazimu Kananda kumtisha kwa kumwambia, usipoachana na ambo haya nitaacha kazi. Hata hivyo, Kananda alielewa kitisho hiki hangekitekeleza. Hela alizokuwa akizipata ziliwaauni wazazi wake pakubwa.
> Siku moja, Maria aliwatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji. Jioni ya siku hiyo ulevi wa Mwatela ulimtuma kumtia doa Kananda. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 99)

Dondoo hili linamrejelea Mwatela ambaye alimnajisi kijakazi wake aliyeitwa Kananda kutokana na ulevi wake.Kananda alikuwa mfanyakazi pale nyumbani kwa bwana Mwatela. Mtoto huyu alikuwa ameajiriwa pale hili aweze kuwasaidia wazazi wake kujikimu. Wazazi hawa walikuwa maskini kiwango cha kutoweza kumpeleka Kananda shuleni. Basi Kananda alipokuwa pale kwa Mwatela, aligundua kuwa Mwatela alipenda kuchapa mtindi na mara kufika usiku akiwa amelewa chakari. Alikuwa anaanza ugomvi na bibi yake Maria kutokana ulevi huu. Alianza pia kumchokoza Kananda akitaka

washiriki mahaba naye lakini Kananda alikuwa anakataa. Basi siku moja Maria, mkewe Mwatela alipokwenda kuwatembelea wazaziwe mbali na jiji, Mwatela alimnajisi Kananda kama ilivyodhihirika hapa juu. Kunajisiwa huku kulimsababishia mimba ya mapema kama ifuatavyo:

> "Baada ya miezi miwili Kananda alibaini kuwa alikuwa na kijusi tumboni." Uk 99

Kwa mujibu wa mwandishi wa kazi hii, matumizi ya pombe kwa mwajiri wake Kananda yalichangia katika uhusiano wa kimahaba na Kananda. Pia, mimba ya mapema ilitokea kutokana na kunajisiwa huku.

Isitoshe, katika hadithi ya "Shetani hana Hatia" Pakashume alifikirika kuwa alikuwa mtumizi wa dawa za kulevya zilizochangia kumbaka mpwa wake wa chekechea aliyeitwa Toto. Alipombaka mtoto huyu alivamiwa na wapita njia ambao walimwadhibu vikali. Alinusuriwa na polisi wawili wapita njia ambao walimpeleka hospitali kwa matibabu chini ya ulinzi wao mkali. Mle hospitalini nesi waliokuweko walikuwa na kila sababu ya kushangaa na kujiuliza maswali mengi kumuona mwanaume wa kiwango chake kumbaka mtoto mdogo wa chekechea. Hapo ndipo afisa mmoja wa polisi aliingilia mazungumzo yao na kusema:

> "Labda amerukwa na akili kwa sababu ya kutafuna miraa" (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*,2007, Uk 56)

Dondoo hili linashadidia msimamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya dawa za kulevya hasa miraa. Linaonyesha vile matumizi ya miraa yalichangia kuifanya akili kutofanya kazi vifaavyo na hivyo Pakashume kutenda kitendo kisichotarajika cha kumshirikisha mtoto mdogo kwa mahaba. Kupitia dondoo hizi, ni bayana kuwa matumizi ya pombe na dawa za kulevya huchangia watu kuwa na uhusiano wa kimahaba na watoto.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii iliangazia sababu zinazochangia uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa kuna sababu mbalimbali zinazochangia uhusiano wa kimahaba miongoni mwa watoto jambo ambalo linachangia mimba za mapema. Visababishi hivi ni pamoja ni kama kubakwa, ukatili wa wazazi, ukosefu wa uamuzi bora, kutowaadilisha watoto vifaavyo, uyatima, umaskini, matumizi ya dawa za kulevya, kujikimia mahitaji, kulipiza kisasi miongoni mwa visababishi vingine.

Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni suala nyeti kutokana na athari zake kwa wanajamii. Katika sura iliyofuata, mtafiti aliangalia athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kwa mujibu wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichochewa na ongezeko la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni na athari zake katika jamii. Katika sura hii, mtafiti aliongozwa na madhumuni ya pili ya kutathmini athari za uhusiano huu wa kimahaba na mimba za utotoni. Mtafiti alitumia matini zilizoko katika hadithi fupi teule ili kueleza kwa kuongozwa na maoni yake kuhusu athari hizi kwa mujibu wa Tompkins (1980) kuhusu nadharia ya mwitikio wa msomaji. Athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema zikiwemo ujauzito usiotarajiwa, msongo wa mawazo, vifo, unyanyapaa, ndoa za mapema, kutomakinika masomoni, majuto na athari nyinginezo zilijadiliwa kwa mujibu wa hadithi fupi teule za Kiswahili.

## 4.2 Athari za Uhusiano wa Kimahaba na Mimba za Mapema

Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni limekuwa suala sugu kutokana na athari zake kwa wanajamii. Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UN na UNFPA, 2013) inaeleza kuwa watoto wanaoshika mimba chini ya umri wa miaka kumi na minane hukumbana na matatizo mengi. Baadhi ya matatizo haya ni yale ya kiafya kama vile magonjwa ya zinaa, fistula na yale ya kijamii kama kutengwa. Vilevile, Shirika la Kimataifa la Human Right Watch (2016) linaonyesha kuwa asilimia 40 ya wanafunzi hukatiza masomo yao ya sekondari kutokana na ujauzito. Watoto wengine hukumbana na ndoa za mapema hasa pale wanakuwa wahanga wa mimba za utotoni (UNICEF, 2017).

Waandishi wa hadithi fupi teule wamesawiri uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama iliyosababisha madhara mengi.  Miongoni mwa athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni:

### 4.2.1 Ujauzito Utotoni Usiotarajiwa

Uhusiano wa kimahaba utotoni umechangia ongezeko la mimba za mapema miongoni mwa watoto. Mimba hizi huja wakati usiofaa na hivyo kuathiri maisha ya mhusika kwa kiwango kikubwa. Hii ni kwa sababu huwafanya watoto kuwa wazazi wakati ambapo wanafaa kuwa shuleni. Uhusiano wa kimahaba unaochangia mimba za mapema

unaweza kuwa wa hiari au wa kulazimishwa. Si uhusiano wote wa kimahaba huleta mimba kutegemea umri wa mtoto, mabadiliko ya kimwili na pia njia za kujikinga. Hata hivyo, mtoto yeyote anafaa kuepushwa na uhusiano wa kimahaba wa aina yoyote kwani hana uwezo wa kujitolea uamuzi katika umri huu. Kwa mujibu wa Utafiti kuhusu Hali ya Afya katika maeneo mbalimbali nchini (KDHS, 2014), kaunti ya Narok iliongoza kwa idadi ya wasichana waliopata mimba wangali wadogo. Mwaka 2018, kaunti hii ilikuwa na visa 15,000. Isitoshe, kuzuka kwa janga la korona nchini na kufungwa kwa shule mwaka elfu mbili na ishirini kulichangia watoto wengi kuwa waathiriwa wa mimba za mapema. Wengi walijiingiza katika mahaba kwa sababu mbalimbali ambazo zilichangia wengine kuwa waja wazito. Hii ni kwa mujibu wa ripoti mbalimbali zinazotolewa na vyombo vya habari. Mutheu (2020) anaeleza kuhusu hatua ya viongozi ya kuomba vijana kupewa elimu kuhusu maswala ya uzazi ili waweze kujiepusha kupata mimba za mapema.

Rhoda Nyaga ni mwandishi wa hadithi fupi teule ya "Kanda la Usufi" ambaye anaeleza athari hii ya uhusiano wa kimahaba. Nikimnukuu:

> "Muhula wa tatu wa kidato cha pili ulipoanza Sela alijiunga na wanafunzi wengine. Mwezi wa kwanza wa muhula uliisha. Ulipoisha akathibitikiwa na kile alichohofia katika uhusiano wake na Masazu. Kijusa kilikuwa kimetungika! Hapakuwa na nafasi ya kugeuza mambo" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 61).

Nukuu hili linaonyesha yaliyomkumba Sela kutokana na kushiriki mahaba angali shuleni, yaani kupata mimba asiyohitaraji. Sela alikuwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo. Alimpata mpenzi siku ya tamasha za muziki na drama zilizoandaliwa shuleni mwao aliyeitwa Chris Masazu. Masazu alikuwa mwanafunzi wa shule ya wavulana ya Lenga Juu. Watoto hawa walijihusisha na uhusiano wa kimahaba kupitia mikutano ya faragha wakati wa likizo na katika tamasha za shule nafasi ilipojitokeza. Likizo ya muhula wa pili katika kidato cha pili iliwaletea wasichokitarajia wakati huo.

Kupitia kifungu kilichodondolewa, jambo alililoliogopa Sela katika uhusiano wake na Masazu ni lile la kuwa mja mzito. Uhusiano wake wa kimahaba na Masazu ulimsababishia ujauzito usiotarajiwa kwa wakati ule. Hivyo, Sela alipata ujauzito asioupangia kutokana na kushiriki mahaba utotoni.

Vilevile, Kananda alikuwa mja mzito na mzazi katika umri mdogo baada ya kunajisiwa na mwajiri wake Bwana Mwatela baada ya mkewe Maria kwenda safari. Uja uzito wake ulitokana na hali ya kulazimishwa na wala si kwa hiari. Nia yake pale kwa bwana Mwatela ilikuwa kufanya kazi ili aweze kuwasaidia wazazi wake ambao walikuwa katika hali ya umaskini na kukosa kumpeleka shule. Hata hivyo, matarajio yake hayakukamilika baada ya kunajisiwa na mwajiri wake bwana Mwatela. Kwa mfano:

> Siku moja, Maria aliwatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji. Jioni ya siku hiyo ulevi wa Mwatela ulimtuma kumtia doa Kananda. Kananda alifadhaika sana lakini akaona heri anyamaze. Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha! Baada ya miezi miwili Kananda alibaini alikuwa na kijusi tumboni. Alilia usiku na mchana. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 99).

Kwa mujibu wa nukuu hili, Kananda alilia kwa sababu alikuwa na nia ya kupata kibarua na kuwasaidia wazazi wake. Sasa hapa yu mja mzito, uja uzito wa kulazimishwa na mwajiri wake. Kananda alikuwa msichana mdogo ambaye alifaa kuwa shuleni. Kutokana na uchochole uliokuwa pale nyumbani, hakuweza kupelekwa shuleni. Ndoto yake ya kuwasaidia wazazi aliiona ikididimia alipopata ujauzito katika umri wake mdogo.

Mohammed Ghassany anazungumzia athari hii pia. Sara katika hadithi ya "Mame Bakari" aliadhirika kutokana na mimba ya mapema. Sara alikuwa mwanafunzi. Ujauzito wake ulitokea usiku mmoja majira ya saa tatu unusu alipobakwa na jitu asilolijua akitoka masomo ya usiku. Kwa mfano:

> "Leo ndiyo huyu hapa Sara, mja mzito wa miezi miwili u nusu. Ulikuwa uja uzito wa Jumatano ile. Uja uzito wa kubakwa na kulazimishwa. Wa kuvunjiwa ujanajike na utu wake. Wa kuharibiwa maisha yake" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* 2016, uk 47)

Kutokana na kifungu hiki, Sara alipata ujauzito asiotarajia kwa kubakwa. Sara alitamani jambo hili lingekuwa ndoto bila kuacha athari katika maisha yake kama inavyojitokeza katika dondoo hili:

> Taratibu alinyanyua mkono wake na kuupeleka kwenye kitumbo chake. Mkono ulipoigusa ile ngozi ya tumbo, Sara alishtuka. Mkono ulikuwa umegusa hisia za mabadiliko ya kitumbo chake kilichokwishaanza kufura. Katika ukweli wa mambo kitumbo kile hakikumletea maumivu yoyote lakini fikirani kitumbo kilimzushia ukiwa na udhaifu. Na hilo lilimwuma sana. Alitamani kuwa jambo lile lisingelikuwa ukweli. Jambo lile lililotokezea. Laiti ile ingelikuwa ndoto tu. Ndoto iliyomjia

> na kupotea bila ya kuathiri chochote katika mwili wake. (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 46).

Dondoo hili ni dhahiri kuwa Sara alikuwa amepata ujauzito asiotarajia kwa wakati ule. Hii ndio sababu anatamani kuwa tukio hilo lingelikuwa tu ndoto. Udhaifu na ukiwa aliokuwa nao ulikuwa kwa sababu alijipata mjamzito, tena wa kulazimishwa. Ni wajibu wa wanajamii kuwalinda watoto dhidi ya mimba zisizotarajiwa na kuwapa mwanga wa maisha ya baadaye.

Lozi katika hadithi ya "Malimwengu" alijihusisha kimahaba na wanaume matajiri. Msichana huyu ambaye alikuwa amefiwa na wazazi na kuachwa mikononi mwa shangazi Mashaka aliachishwa shule katika shule ya msingi. Baada ya mateso mengi na shangazi Mashaka, aliamua kwenda mjini kutafuta kazi ili aweze kujikimu na pia kumkimu nyanya yake Bibi. Huko, alipatana na wanaume matajiri na kujiusisha kimapenzi nao. Kupitia matajiri hawa, alikodisha chumba cha kifahari, kununua vyakula vya bei ghali na pia vifaa bora vya nyumba. Baada ya haya yote, alijipata kuwa alikuwa mja mzito. Mwajiri wake alimfuta kazi kutokana na tabia yake ya ukahaba. Isitoshe, alifukuzwa hata chumbani kile. Mwandishi wa hadithi hii Mumbo Kenga amefafanua haya kama ilivyo katika dondoo hili;

> Mchukue huyu kahaba wako umpelekee watu wengine. Mimi ninamsaidia, naye kazi yake kuniaibisha. Mara mlango ukafungwa kwa nguvu, Pacha akarudi ndani. Furaha alipomsaili Lozi, alifahamishwa kuwa alikuwa amepigwa kalamu na pia kufukuzwa kutoka kwa ile nyumba. Kisa na maana? Lozi alikuwa mjamzito. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 32-33)

Kilichompeleka Lozi mjini kwa mujibu wa mwandishi ni kutafuta riziki ili kujikimu na kumkimu Bibi. Kuwa mja mzito ilikuwa ni jambo ambalo hakulitaraji kwa wakati ule. Alikuwa katika umri mdogo na vilevile, nia yake pale kazini ilikuwa tofauti na kupata ujauzito.

Katika hadithi ya "Shogake Dada ana Ndevu", Safia alipata uja uzito akiwa katika darasa la nane. Ujauzito huu ulikuwa wa uhusiano wa kimahaba kati yake na Kimwana ambaye pia alikuwa mwanafunzi wa darasa lake. Safia alipofika darasa hili la kujitayarisha hili kujiunga na shule ya sekondari aliwaomba wazazi wake ruhusa ya kumruhusu amwalike shogake Kimwana wadurusu pamoja. Wazazi wake hawakuwa

na pingamizi yeyote kuhusu ombi hili. Watoto hawa walianza kusoma pamoja mle chumbani mwa Safia. Kutokana na usumbufu wa nduguye mdogo Safia aliyeitwa Lulua wa kuingia mle chumbani, wazazi wake Safia waliwaomba Safia na Kimwana kujifungia ndani mara waingiapo. Kilichotokea baada ya muda ni Safia kuwa mja mzito. Mama yake Safia aligundua kuwa mwanao alikuwa mja mzito. Hata hivyo hakutaka kuamini aliyoyaona. Siku moja alimuuliza mwanawe;

> "Uchangamfu wako haupo. Kila wakati nakuona doro siku hizi. Tena hwishi kutapikatapika" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 33).

Maneno haya yalikuwa ya kumhoji Safia baada ya kuona mabadiliko katika maisha yake. Hakuna aliyetarajia ujauzito kwa wakati ule. Mwishowe, siku moja wazazi wake walipokea simu ya kuwa Safia alikuwa ameenda kliniki kuavya mimba na kuaga.

Kwa mujibu wa dondoo zilizonukuliwa, uhusiano kimahaba utotoni umesababishia watoto wengi athari ya kuwa na ujauzito katika umri mdogo. Kwa mfano, Sara, Lozi Kananda, Sela na Safia ni waathiriwa wa mimba zisizotarajiwa.

### 4.2.2 Unyanyapaa

Ujauzito utotoni ni mojawapo wa hali ambazo hufanya watoto husika kutopata heshima kutoka kwa wenzao na hata jamii kwa jumla. Waandishi wa hadithi fupi wamedhihirisha athari ya unyanyapaa kupitia dondoo hizi:

> …Zamu ya mkuu wa shule ilitimia. Aliwakumbusha wanafunzi umuhimu wa kuwajibikia vitendo vyao. Baada ya hilo, aliita majina ya wanafunzi watatu na akatangaza kwamba baada ya kufumukana wafike ofisini mwake. Vicheko vya chini chini vilianguliwa. Sababu ya kuitwa kwa wanafunzi wale ilikuwa dhahiri (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 62).

Kutokana na nukuu hili, mwandishi wa hadithi "Kanda la Usufi" anaonyesha jinsi wasichana watatu ambao walikuwa wamethibitishwa kuwa waja wazito katika shule ya upili ya wasichana ya Askofu Timotheo walivyokosa kuheshimiwa na wanafunzi wengine. Majina yao yaliposomwa pale gwarideni na kuombwa wafike ofisini, wanafunzi wengine walianza vicheko vya chini chini kama njia ya kuwadharau kwa sababu walikuwa wanajua hali zao. Sela alikuwa miongoni mwa wasichana hawa watatu. Sela hakukosa kuheshimika na wanafunzi wenzake tu bali pia baba yake mzazi.

Baba yake alimfukuza nyumbani pamoja na mama yake kutokana na kuwa alipata uja uzito angali shuleni jambo ambalo hakulitarajia kwake.

> Aliendelea kububujika na machozi kila alipoyafikiria yaliyompata na yatakayompata miezi si mingi ijayo. Yaani ule muhuri mpya aliopigwa na jitu utakuwa muhuri wa balaa utakaobadilisha nafsi yake milele. Tukio ambalo lilikwisha mfungulia ukurasa mbaya katika maisha yake. Lilikuwa limeshamchipuza kule ambako hakumstahiki kwa sasa au kwa wakati wowote. Haikuwa stahiki yake kubebeshwa mzigo ule. Ungelimsababishia dhiki nyingi na mateso tele pamoja na aibu na uduni kwa wanadamu wenzake. Kila alivyofikiri aliona kutengwa kunakuja. Tena si kutengwa tu, na misuto na kashfa juu. Na zaidi ya hayo, laana na misubukio kutoka kwa kila mtu-wa karibu na wa kando (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 48).

Sara katika dondoo hili la pili alikuwa mjamzito wa kubakwa. Alifikiri jinsi alivyotarajia kutengwa na kubezwa kutokana na hali hiyo. Mhusika huyu alikumbwa na msukumo wa mawazo.

Katika dondoo zilizonukuliwa hapa juu, waandishi wa Hadithi fupi wameangazia unyanyapaa unaosababishwa na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyo kwa wahusika Sela na wanafunzi wenzake na pia Sara. Athari ya unyanyapaa miongoni mwa wasichana waja wazito umechangia watoto wengi wa kike kuacha shule na wengine kutoroka nyumbani ili wasipate kutengwa na kupokea misuto. Kwa hivyo, namna ya kuishi na wasichana walio na mimba ni muhimu kwani huwapunguzia mawazo na kujihisi wakamilifu

### 4.2.3 Usiri

Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zimechangia usiri miongoni mwa waathiriwa. Mtoto anapokuwa msiri hana uhuru wa kueleza hali yake barabara bila woga. Hili linadhihirishwa na waandishi wa hadithi teule kupitia dondoo hizi;

> Bi. Hamida alimtazama mwanawe usoni kwa macho makavu. Lakini Safia yeye aliendelea kutupa macho yake chini. Hakuweza kunyanyua uso.
> ‘Kama una jambo niambie mapema Safia,’ alitafadhalisha mama mtu.
> Lakini Safia alikupuka kwa hasira na kutumbukia chumbani mwake huku akibweka, Unanifikiria mambo mabaya mama. Unanifikiri mambo maovu mama. Pamoja na kujilinda kwangu. (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 33)

Safia alipata uja uzito kutokana na uhusiano wa kimahaba na shogake Kimwana wakiwa katika harakati za kudurusu kwa ajili ya kujiweka tayari kwa mtihani wa mwisho wa kujiunga na shule ya upili. Alipohojiwa na mama yake iwapo kulikuwa na tatizo, alikataa kata kata kueleza ukweli na kuiweka kuwa siri. Alimwambia kuwa alikuwa anamfikiria vibaya licha ya kuwa alikuwa anajilinda. Ukweli ulidhihirika alipokwenda kliniki kisiri kuavya mimba na kufariki katika harakati hizo. Wazazi wake walipata ujumbe kupitia simu ya mkononi kuwa Safia aliyekwenda kliniki kuavya mimba alikuwa amefariki wakauchukue mwili.

Usiri wa Safia ulisababishwa na kutoadilishwa vyema na wazazi wake. Wazazi wake walimuona malaika na hivyo hawakumpa mwelekeo bora wa maisha. Alipokuwa mja mzito, haliona vigumu kuwaambia wazaziwe.

Isitoshe, Mohamed Khelef katika hadithi yake "Mame Bakari" ana haya ya kusema:

> "Kwa nini hakutoa taarifa ya lile lililompata siku ile? Badala yake alipofika nyumbani, alikwenda kukoga na kujikomolea chumbani kulia na kuomboleza." (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 48)

Hii ni dondoo inayomrejelea mhusika Sara ambaye alipata ujauzito kupitia kubakwa. Aliamua kutowaambia wazazi wake kwa sababu alimuona baba yake kuwa mkali na katili. Pia alifahamu kuwa mama yake asingemsaidia kwani asingeweza hata kuitetea nafsi yake mbele ya mumewe. Aliiona jamii yake kuwa isingemtetea kwa lolote lile bali ingemkashifu. Alifanya uamuzi wa kuliweka jambo lile kuwa siri kwa kuoga na kujifungia chumbani na kuomboleza peke yake. Mawazo yalipomlemea alimwendea rafiki yake Sarina kwa usaidizi. Wote walikubaliana kuubeba uja uzito ule kwa siri kubwa.

> "Hatua ya mwanzo waliyokubaliana kuchukua ikawa ni namna ya kuuficha na kuutunza ujauzito ule katika siku hizi za mwanzo. Wakaamua kuuficha chini ya jilbabu, vazi ambalo tokea hapo kabla lilivaliwa na Sara kwa nadra." (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 51)

Vazi la jilbabu lilidhihirisha kuwa hawakutaka mtu yeyote kutambua kuwa alikuwa mjamzito pale nyumbani na hata shuleni. Waliamua pia kuwa mahali pa kujifungulia ni shambani mwa wazazi wa Sarina. Siri hii ilisababishwa na kuwaogopa wazazi kwa kuwaona wakali na katili wa kuambiwa ukweli kuwa mimba yake ilitokana na ubakaji.

Hadithi ya" Mwana wa Darubini" na mwandishi Kristina Mbai anaieleza athari hii pia. Kananda alikuwa mtoto mdogo na kijakazi kwa bwana Mwatela na mkewe Maria. Mwatela alikuwa mlevi na kila mara alipolewa alimchokoza Kananda kwa kutaka mapenzi naye. Kananda hakutaka kujihusisha na mahaba na hivyo kila mara Mwatela alipokuja na jambo hili, Kananda alitishia kuacha kazi. Siku moja Maria alipowatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji Mwatela alimnajisi Kananda. Baada ya miezi miwili, Kananda aligundua kuwa alikuwa mjamzito kutokana na kitendo alichokuwa ametendewa na mwajiri wake siku ile. Hapa ni dondoo:

> "Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha! Baada ya miezi miwili Kananda alibaini alikuwa na kijusi tumboni. Alilia usiku na mchana. Hakutaka wazazi wake wajue hali yake. Aliamua kunyamaza. Kimya chake kikawa kinamchoma ndani kwa ndani" *(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 100)

Kwa mujibu wa mwandishi huyu, Kananda aliujenga usiri wa kutowaarifu wazazi wake kwamba alikuwa mja mzito. Alipobaini kuwa alikuwa na mimba, aliamua kunyamaza na wala hakutaka wazazi wake wajue. Hii ni dhahiri kuwa usiri wake ulisababishwa na mimba ya mapema aliyopewa na mwajiri wake na kumwondoa katika lengo lake la kuwa kijakazi.

Kwa kurejelea vifungu hivi, uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zimewaathiri wasichana wadogo na kuwafanya kuwa wasiri katika maisha yao. Hii ni kwa sababu ya kuogopa matokeo ambayo yangeibuka kutokana na kugunduliwa kuwa wao ni wajawazito au wameshiriki mapenzi.

**4.2.4 Kifo**

Uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema miongoni mwa watoto zinasababisha vifo nchini na ulimwenguni kwa jumla. Vifo hivi hutokana na magonjwa ya zinaa kama vile ugonjwa wa UKIMWI ambao husambazwa kupitia uhusiano wa kimahaba wa kiholela. Watoto wengine hufa wakijaribu kuavya mimba ambayo inapatikana wakati usiotarajiwa. Vilevile, wengine hufa kutokana na kufuja damu nyingi wakati wa kujifungua.

Baadhi ya wahusika katika hadithi fupi teule wanakumbwa na athari ya kifo kutokana na uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Iribemwangi katika hadithi yake "Namchukia Babangu" anaangazia suala hili kama ifuatavyo:

> Nako jijini, dadangu aliyeitwa Kichomi alianza kukoga vizuri na kuwawinda wanaume na hatimaye akapata chake. Alikodi chumba katika mtaa wa Majengo. Tangu siku alipotuacha na kuhamia huko, sikumwona tena. Miaka kadhaa baadaye, nilipata habari kuwa kala tunda lenye dudu baya na hatimaye akajifia. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007 Uk 114).

Kichomi alikuwa mwanawe Mzee M'mali. Mzee huyu alikataa kagharamikia malezi na elimu bora kwa wanawe licha ya kuwa tajiri mtajika. Mateso yalipozidi, wanawe walitorokea mjini kuwa watoto wa mtaani. Kichomi aliamua kujihusisha mahaba na wanaume ili kujikimu. Mwishowe aliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na kufa. Hii ni dhihirisho kuwa mtoto yuyu yuyu alikufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI ambao aliambukizwa kwa kushiriki mahaba utotoni.

Mwandishi Timammy Rayya ana maoni yaya haya katika hadithi yake "Shimo la Mauti". Dada yake Hamisi katika hadithi hii aliaga dunia kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mtoto huyu aliacha shule na kuanza biashara ya kuuza nguo za mitumba ili kujikimu na nduguye kwani watoto hawa walikuwa mayatima. Alipoona biashara ya nguo haiwapi kipato alichoitaji, alijiuza yeye kama mtumba yaani kahaba kwa bei ya chini. Hapa ni nukuu kuhusu haya:

> …Maskini dadake alianza kuugua. Alianza kumumunyuka kama udongo. Nguvu zilianza kumwishia na biashara yake ikaanza kuzorota. Katika kule kuuza, aliuza zaidi ya nguo za mitumba kwa kuwa biashara ile haikuweza kukamilisha mahitaji yao yote, ikambidi yeye mwenyewe kuwa mtumba. Katika biashara hiyo alijipata taabani na ugonjwa wa ukimwi. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 77).

Nukuu hili linaonyesha dalili za ugonjwa uliomkumba dada yake Hamisi kutokana na kushiriki mahaba na wanaume. Dalili hizi zilionyesha wazi alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Ni kutokana na ugonjwa huu ambapo yafuatayo yalitokea:

> …Dadake naye alikuwa amelala kwa tani huku macho yake wazi yakiangalia juu. Maskini tayari alikuwa ameshakata roho sijuikutokea saa ngapi. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, uk 79)

Hili ni nukuu linalodhihirisha kuwa uhusiano wa kimahaba utotoni ulichangia kuambukizwa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa huu ulisababisha kifo cha dada yake Hamisi.

Gichamba katika hadithi yake "Safari ya Maangamizi" anaeleza jinsi Pendo aliaga kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Wanaume watano walijiusisha mapenzi naye kwa kumbaka ambapo baadaye alikuja kujua kuwa ata alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kutokana na kitendo kile. Katika mazishi yake, rafiki yake Faridi aliwasomea waombolezaji wosia aliokuwa ameuandika kuhusu jinsi alivyoambukizwa ugonjwa ule na vile alivyousambaza kwa wengi kama njia ya kulipiza kisasi. Wosia huu ulizua vilio vingi kwenye mazishi yale kwani kulikuwa na wengi waliokuweko ambao walikuwa wameshiriki mapenzi na Pendo. Hivyo nao, walikuwa wanaisubiri siku yao ya kufa.

Alifa Chokocho alikuwa na mtazamo tofauti katika hadithi yake ya "Shogake Dada ana Ndevu" kuhusu kisababishi cha athari ya kifo. Safia, msichana mdogo alikufa katika harakati za kuavya mimba. Mtoto huyu alikuwa kapachikwa mimba na Kimwana, mwanafunzi mwenzake ambaye alikuwa anakuja pale nyumbani kwao kudurusu pamoja ili kujiweka tayari kwa mtihani wa kujiunga na shule ya upili. Wazazi wake Safia hawakuwa wanamshuku Kibwana kwa lolote kwani walijua kuwa alikuwa na tabia njema kama mwanao Safia alivyokuwa akiwaambia. Walikuwa wanajifungia chumbani mwa Safia ili kudurusu kama walivyoelekezwa na wazazi wake Safia. Mama yake Safia alipomdadisi mwanawe kujua iwapo alikuwa mja mzito baada ya kuona dalili, Safia alikana kwa kusema kuwa alikuwa na homa ya malaria. Siku moja dada yake mdogo aliyeitwa Lulua aliwahadithia wazazi wake jinsi alivyoufungua mlango wa chumba cha Safia ili kutafuta mahali bora pa kujificha walipokuwa wanacheza na rafikiye. Alieleza kuwa mlango ulipofunguka, alimwona shogake dada ana ndevu. Ni katika harakati hii ambapo simu ya baba yake ilikirizwa na alipoipokea, alipata ujumbe kuwa Safia alikuwa amekufa pale kliniki alikokuwa ameenda kuavya mimba.

> …Ameshakufa…Ameshakufa…
> Naam, ujumbe ulikuwa wazi. Safia aliyekwenda kliniki kutoa mimba, amekufa. (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 35)

Kuavya mimba kwa msichana huyu kulisababisha kifo chake pamoja na cha mtoto aliyekuwa tumboni. Vifo hivi vyote vingezuiliwa iwapo hakujihusisha na uhusiano wa kimahaba angali mtoto.

Kwa mujibu wa dondoo hizi hapa juu ni dhahiri kuwa uhusiano wa kimahaba na uja uzito utotoni ni mambo ambayo yamechangia vifo vya watoto wa kike nchini na ulimwenguni kama ilivyo kwa Pendo, Kichomi, dada yake Hamisi na Safia. Ugonjwa wa UKIMWI unasambaa kwa kasi sana kutokana na hali ya kushiriki mapenzi ya kiholela. Vilevile, vifo vinavyotokana na kuavya mimba vimeongezeka pia kwa sababu ya mimba zisizotarajiwa kama ilivyo kwa mhusika Safia. Athari hii ni hatari na suluhu ya haraka inahitajika kukabiliana na uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

**4.2.5 Ndoa za Mapema**

Asilimia kubwa ya watoto walilazimishwa kuolewa wakiwa chini ya miaka kumi na minane. Kwa mfano, Sudan Kusini ina asilimia 52, Uganda asilimia 40, Tanzania 28 na Kenya 23 ya wasichana walioolewa wakiwa watoto. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF, 2017). Mwende (2020) alieleza kuwa takwimu za Baraza la Kitaifa Kuhusu Idadi ya Watu (NCPC) zilionyesha kwamba kuna ongezeko la mimba za mapema miongoni mwa wasichana wadogo.Ongezeko hili lilisababishwa na ndoa za mapema.

Uhusiano wa kimahaba utotoni umechangia watoto kujiingiza katika ndoa. Hii ni kutokana na matokeo yake yakiwemo mimba za mapema. Gharama za kuwalea watoto peke yao katika umri huu huwa ngumu. Wengine uona heri kuolewa ili wajukumike pamoja. Nchini Kenya, ndoa za mapema ni tatizo kubwa kwa wasichana hasa wa umri wa shule. Waandishi wa kazi teule wana haya ya kusema kuhusu athari hii.

Sela katika hadithi ya “Kanda la Usufi” alijihusisha na mahaba angali shuleni katika kidato cha pili. Alipata mpenzi aliyeitwa Masazu ambaye pia alikuwa mwanafunzi katika shule nyingine. Uhusiano huu ulihusisha mikutano ya siri ambayo hatimaye, Sela alijipata mja mzito. Kwa kuwa hakuna aliyekuwa na uwezo wa kumtunza mtoto, Sela alipojifungua alimwacha Rozina na jukumu la kumtunza mwanao ili arudi shuleni.

Baada ya kuhitimu kidato cha nne, alienda alikokuwa ameajiriwa Masazu ili waishi kama mume na mke. Nikinukuu:

> Sela alimfuata Masazu huko huko Dafina baada ya kumaliza masomo. Waliishi kama mume na mke. *(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 64)

Ndoa kati ya Sela na Masazu ilisababishwa na kuweko na mtoto ambaye walikuwa wamempata mapema maishani. Ndoa hii ya mapema ilikuwa na changamoto zake kwani mwandishi anatueleza kuwa Masazu hangemudu utaratibu wa wazi wa kwenda kwa akina Sela. Walipomwitaji mwanao walipanga kumchukua usiku wakati kila mmoja alikuwa amelala jambo ambalo liliwasababishia mkosi wa kutembea usiku na kusombwa na maji kidimbwini.

Kristina Mwende katika hadithi yake ya "Mwana wa Darubini" anaonyesha mtoto Kananda alivyokuwa tayari kujiingiza katika ndoa ya mapema baada ya kugundua kuwa alikuwa mjamzito. Kananda alipata mimba baada ya kunajisiwa na mwajiri wake Mwatela. Mwatela alimuahidi kuwa angemuoa kama mke wa pili iwapo asingelifanya kuwa siri na kukataa kumwambia mke yake kwa jina Maria. Mwatela alimnajisi kijakazi huyu siku moja ambayo Maria alikuwa ameenda kuwatembelea wazazi wake mbali jijini. Mwatela alimwambia Kananda amwambie bibiye kuwa uja uzito huo ulikuwa wa rafiki yake mvulana wa huko nyumbani alikotoka. Alimwambia kuwa baada ya kujifungua basi angehitimu kuwa bibi wake wa pili. Kwa mfano:

> "Siku moja alijasirika kumwambia Bwana Mwatela hali yake. Mwatela: Kama una mimba ya mtoto wangu basi nitakuoa uwe mke wangu wa pili Kananda: Utanioa lini? Mwatela: Utakapojifungua." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk100)

Kwa mujibu wa dondoo hili, Kananda alikuwa anataka kuolewa kama mke wa pili si kwa sababu alikuwa tayari wakati ule lakini alikuwa anasukumwa na hali yake ya kuwa mja mzito. Suluhu ya uja uzito wake Kananda aliiona katika ndoa ambapo baba yake mtoto angewajibika na kuzuia kumpata mtoto nje ya ndoa. Hivyo, mimba za mapema zimechangia ndoa za mapema miongoni mwa watoto. Ni jukumu la wanajamii kuwalinda watoto dhidi ya ndoa za mapema kwa kuwaepusha na mimba za utotoni.

### 4.2.6 Kufukuzwa Nyumbani

Watoto wengi hujipata bila makao kutokana na ujauzito wa mapema. Wanafukuzwa nyumbani na wazazi katili ambao hawana nafasi ya kuzungumza na wanao baada ya

kukumbwa na tatizo la uja uzito au hata kujua kisababishi chake. Jambo hili hukosesha familia amani kama wanavyoeleza waandishi wa hadithi fupi teule.

Mwandishi wa hadithi fupi ya "Kanda la Usufi" anaeleza jinsi familia ya mzee Butali ilikosa amani. Hii ni baada ya kuombwa kufika pale shule ya wasichana ya Askofu Timotheo alikosomea bintiye Sela na kuelezwa na mwalimu kwamba alikuwa mja mzito. Aliombwa kuondoka naye na kumtafutia shule iliyo karibu na nyumbani. Hali ilibadilika walipofika nyumbani. Alifoka si kwa mwanawe pekee bali pia kwa bibi yake akimkashifu kwa kutomtunza binti yake vyema. Lawama zote aliziwekea mama yake Sela na kusababisha wote wawili, mama na mwanawe kufukuzwa nyumbani. Mfano:

> "Boma la mzee Butali liligeuka jahanamu baada ya kutoka shuleni. Mzee Butali aliwazulia majopo Sela na mama yake. Majirani nao walishuhudia bughudha hizo kwa mbali." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 63)

Bughudha hizi zote zilitokana na kuwa mzee huyu asingeamini kuwa jambo kama hilo lingetokea kwake. Aliona kuwa kuzorota kwa maadili ya mwanawe kulichangiwa na mama yake na ndipo akawafukuza wote nyumbani. Anasema:

> "Leo ndio mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti? …Mtwae kilicho chenu mniondokee!
> "Ilibidi Sela na mama yake watorokee kwa jamaa yao aliyeishi karibu. Hapo ndipo walikaa kwa muda wa majuma matatu kabla ya mzee Butali kubadili nia." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 63)

Athari ya Sela na mama yake kufukuzwa nyumbani ilisababishwa na mimba ya mapema. Hiki ni kiwakilisho tosha kuwa watoto hufukuzwa nyumbani kwa kuwa waja wazito.

### 4.2.7 Msongo wa Mawazo

Msongo wa mawazo husababishwa na jambo au kitu chochote ambacho kinaleta usumbufu kwenye mawazo ya binadamu. Kuna dalili ambazo huonekana kwenye mtu anapokuwa na msukumo wa wawazo. Dalili hizi ni pamoja na kulia, huzuni, ukali, unyonge, kutomakinika katika ulifanyalo, mabadiliko katika mavazi na namna ya kuongea miongoni mwa dalili zingine.

Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni mojawapo ya matukio ambayo husababisha jaka moyo miongoni mwa watoto. Wanapojipata katika hali ya kuwa waja wazito bila kutarajia, wengi hupatwa na wasi wasi wa kutojua ni nani bora wa kukimbilia na kupata mawaidha. Iwapo mtoto huyu atakosa mtu wa kumshikilia na kumwelekeza kama mtoto uenda akafanya uamuzi usiofaa kama wa kuavya mimba, kuolewa mapema, kujitoa uhai, kutoroka nyumbani miongoni mwa maamuzi mengine yasiyo muhimu.

Waandishi wa hadithi fupi teule wanaeleza namna uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zinavyoathiri waathiriwa kimawazo. Mohammed Ghassany katika hadithi yake ya "Mame Bakari" anaanza kwa mbinu ya kiangaza nyuma ambapo anaeleza kuhusu maisha ya Sara yalivyokuwa kama ilivyo katika dondoo hili;

> Yale macho yake laini na maangavu yalizidi kububujika chemchemi ya machozi. Chemichemi ilipomwaga mito miwili, machozi yakatoka kama yalivyotoka kwa wingi na kumwangukia mapajani mwake. Kila machozi yalipogusa ngozi yake ndivyo yalipozidi kuzidisha michomo ya mishale nafsini mwake. Huzuni za ukiwa na unyonge zikamzidisha uchungu. Hatimaye akaanza kuhisi anakatika matumbo (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 46).

Dondoo hili linaonyesha jinsi Sara alivyokuwa na msukumo wa mawazo ambayo yalijionyesha kupitia kulia, huzuni, unyonge na pia maumivu ya tumbo. Mawazo haya yalimpata Sara baada ya kubakwa na janaume usiku mmoja wa bahati mbaya huku akitoka katika masomo ya usiku. Kubakwa huku kulimwacha na alama ya maisha kwani alijipata mja mzito. Mwandishi anaendeleza kuwa;

> Aliendelea kububujikwa na machozi kila alipoyafikiri yaliyompata na yatakayompata miezi si mingi ijayo. Yaani ule muhuri mpya aliopigwa na jitu lile utakuwa muhuri wa balaa utakaobadilisha nafsi yake milele. Tukio ambalo lilikwishamfungulia ukurasa mbaya katika maisha yake. Lilikuwa limeshamchupiza kule ambako hakumstahiki kwa sasa au kwa wakati wowote. Haikuwa stahiki yake kubebeshwa mzigo ule. Ungelimsababishia dhiki nyingi na mateso tele pamoja na aibu na uduni kwa wanadamu wenzake. (*Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 47-48).

Licha ya haya yote, Sara alikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi jamaa na marafiki wangalivyomtenga. Aliona kutengwa katika pande zote wakiwemo wazazi, jamaa, marafiki na hata shuleni alikosomea. Mawazo haya yote yalisababisha mafikira si haba katika akili ya mtoto huyu.

Katika diwani hii hii, Alifa Chokocho kwenye hadithi yake ya "Shogake Dada ana Ndevu" anaonyesha dalili za jaka moyo kwa mhusika Safia. Safia alipata uja uzito akiwa katika darasa la mwisho la kujiandaa kujiunga na shule ya sekondari. Kimwana, kijana mdogo wa darasa lao aliyekuwa rafiki yake wa kudurusu pale nyumbani na aliyeaminika sana na wazaziwe Safia alikuwa kisababishi cha mimba hii. Mama yake Safia aliona mabadiliko katika maisha ya mwanawe na kumdadisi ili kujua kiini na kisababishi cha mabadiliko yale. Majibu aliyoyatoa Safia yalikuwa dhahiri kuwa mtoto huyu alikuwa na masukumo wa mawazo kama ilivyo kwenye dondoo hili:

> Bi. Hamida alimtazama mwanawe usoni kwa macho makavu. Lakini Safia yeye aliendelea kutupa macho yake chini. Hakuweza kunyanyua uso.
> 'Kama una jambo niambie mapema Safia,' alitafadhalisha mama mtu.
> Lakini Safia alikupuka kwa hasira na kutumbukia chumbani mwake huku akibweka, Unanifikiria mambo mabaya mama. Unanifikiri mambo maovu mama. Pamoja na kujilinda kwangu. (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 33)

Kuangalia chini bila kumtazama unayezungumza naye ni mojawapo wa dalili za kusema uongo au kuwa na aibu kama ilivyo kwenye nukuu hili. Safia alikuwa anajua ukweli kuwa alikuwa mja mzito lakini hakutaka wazazi wake wajue. Hasira alizokuwa nazo pia ni njia ya kujikinga ukweli usifahamike. Mtoto huyu alikataa kumweleza mama yake mambo yalivyokuwa na mwishowe alijipeleka kliniki kuavya mimba. Huko ndiko aliaga dunia katika harakati za kuavya mimba hiyo.

Kananda katika "Mwana wa Darubini" ni mhusika aliyekumbwa na athari ya msukumo wa mawazo kutokana na uja uzito utotoni. Kananda alipachikwa mimba na mwajiri wake Mwatela kwa kumnajisi mkewe Maria alipokuwa mbali na jiji kwa wazazi wake. Hali ilikuwa hivi:

> Siku moja, Maria aliwatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji. Jioni ya siku hiyo ulevi wa Mwatela ulimtuma kumtia doa Kananda. Kananda alifadhaika sana lakini akaona heri anyamaze.
> Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha! Baada ya miezi miwili Kananda alibaini kuwa alikuwa na kijusi tumboni. Alilia usiku na mchana. *(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 99).

Dalili zilizoashiria kwamba mtoto huyu alikuwa na msononeko wa mawazo kama ilivyonukuliwa ni pamoja na kufadhaika, kunyamaza na kulia. Isitoshe, hakutaka kuwaambia wazazi wake kilichotendeka na kuwa alikuwa mja mzito. Kuwa msiri

kiwango hicho ni dalili ya jaka moyo. Watoto wanapokuwa na dalili zinazoonyesha usumbufu wa kiakili wanafaa kushughulikiwa barabara hili kuzuia athari zingine zinazoweza kuibuka kutokana na mawazo mengi.

### 4.2.8 Kutwika Wazazi na Jamaa Majukumu Zaidi

Waswahili husema kuwa kuzaa si kazi bali kazi ni kumlea mwana (Mkota, 2009). Watoto wanapojihusisha na uhusiano wa kimahaba uenda uhusiano huu ukaleta mimba za mapema. Kutunza mimba ni kazi inayohitaji umakinifu wa hali ya juu na gharama yake pia ni ghali. Watoto wapatapo mimba za mapema hutwika wazazi na walezi jukumu la kuwatunza wangali waja wazito na pia kuwatunzia watoto wao wanapojifungua. Jukumu hili huwa mzigo kwa wazazi na walezi ambao tayari wana jukumu lingine la kuwalea wao kama wanao. Watoto wengine hujipata wakiwa na uhusiano wa karibu na walezi wao kuliko wazazi wao wenyewe kutokana na hali hii ya kubadilishana majukumu na kukosa kuwajibika kama mama au baba mtoto. Waandishi wa kazi teule wameangazia jamii inavyotwikwa majukumu ya ulezi kwa sababu ya mimba za mapema miongoni mwa wanao.

Katika hadithi ya "Kanda la Usufi", Sela alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili. Alishiriki mahaba akiwa katika kidato cha pili na mvulana aliyeitwa Masazu, mwanafunzi katika shule jirani. Mwanzo wa muhula wa tatu, Sela aligundulika kuwa alikuwa mja mzito kutokana na ukaguzi wa pale shuleni. Mwalimu mkuu wa shule aliwapa wazazi wa Sela na wanafunzi wenzake wawili waliopatikana waja wazito jukumu la kuwatafutia shule tofauti zilizokuwa karibu na kwao. Sababu ya kupendekeza shule hizi kutwa na za karibu ni hili watoto hawa wapate kutunzwa na wazazi wao kwani uja uzito huhitaji uangalifu mwema. Kwa kuwa watoto hawa hawajakomaa kiwango cha kuweza kujitunza wenyewe, basi jukumu lile linatwikwa wazazi wao au walezi.

Isitoshe, Sela alipojifungua mwanawe Kadogo, alimpa mama yake na haratiye Kadogo jukumu la kumlea. Nguo alizovaa Kadogo zilitafutwa na mama yake Sera. Hii ni kwa sababu Sela alikuwa mwanafunzi na asingekuwa na hela za kumgharamia mwanawe. Isitoshe, Masazu pia asingeweza kumkimu kwa lolote. Mama yake Sela alikuwa na jukumu hili:

> "Katika ufukara wa pale nyumbani, mama yake Sela hangeweza kukinunulia kitoto viguo. Ilibidi matambara yatumiwe kukivisha kitoto." *(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 63)

Rozina ambaye alikuwa harati yake Kadogo alitwikwa jukumu la kumlea kadogo pia. Mfano:

> "Rozina (harati yake Kadogo) ndiye alikuwa mlezi wake katika kipindi ambacho mama yake Kadogo alirudi kuendelea na masomo yake na baadaye Sela alipomaliza masomo ya shule ya upili na kuenda kuishi na Masazu." (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 64)

Sela hakuwajibikia kitendo chake cha kujihusisha na uhusiano wa kimahaba angali mwanafunzi. Matendo yake yaliwagharimu jamaa zake kumtunzia mwanawe na pia kumlea kama inavyodhihirishwa na vifungu vilivyonukuliwa.

Katika hadithi ya "Mame Bakari", iwapo ujauzito wa Sara ulitokana na kubakwa, uliwapa wazazi na marafiki jukumu la kutunza mimba na kulea mtoto. Sara hakutaka wazazi wake wajue kuwa alikuwa amebakwa na hapa yu mja mzito. Alimkaribia rafiki yake wa dhati aliyeitwa Sarina ili amsaidie kuitunza mimba ile tena kwa siri kubwa. Mpango huu ulikamilika barabara kwani Sarina alikuwa tayari kumsaidia kwa vyovyote vile. Dada yake Sarina aliyeitwa Beluwa na aliyekuwa daktari wa uzazi alikuwa pia na jukumu kwa uja uzito huu. Alichukua vifaa vya kupima mimba kila mwezi na kuvipeleka nyumbani ili aweze kumhudumia Sara ambaye alitaka kila kitu kiwe siri, Uk 52. Baada ya miezi sita, iligundulika kuwa matibabu yote ambayo Sara alikuwa anayapokea pale nyumbani yalikuwa yanagharamiwa na wazazi wake ambao walikuwa wamepaswa habari na Beluwa siku tatu tu baada yake kuipokea. Wazazi wake Sara, Sarina na Beluwa walikuwa na jukumu la kuitunza mimba ya Sara kwani katika umri ule hangeweza kujua wala kufanya lolote peke yake. Baada ya kujifungua, mtoto wake Mame Bakari alitunzwa na wazazi wake pia.

Uhusiano wa kimahaba utotoni na mimba za mapema huwagharimu wazazi na wazazi. Hii ni athari ambayo imekuweko kwa muda na suluhu ya haraka inahitajika hili kukomesha gharama hizi.

### 4.2.9 Kuambukizwa Virusi vya UKIMWI

Uhusiano wa kimahaba unaweza kusababisha magonjwa ya zinaa kama vile ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa huu umekuwa tishio kubwa nchini na ulimwengu mzima. Baada ya kuripotiwa kwa kisa cha kwanza nchini Kenya mnamo mwaka wa 1980, kufikia mwaka wa 1999, ugonjwa huu ulikuwa umesambaa na kuwaangamiza watu wengi na kusababisha kutangazwa kwake kama janga la kitaifa. Ugonjwa huu hauna tiba na wala haubagui jinsia wala umri wowote. Njia kuu ya kusambaza ugonjwa huu ni kushiriki ngono kiholela na mtu aliye na virusi vinavyosababisha ugonjwa huu. Watoto wanapojihusisha na uhusiano wa kimahaba kiholela wanaweza kujipata wakiwa waathiriwa kwani huu ni ugonjwa usiobagua. Isitoshe, wengine hujipata wameshiriki mapenzi bila kwa hiari yao jambo ambalo huweza kuwaletea ugonjwa huu pia.

Iribemwangi katika hadithi yake "Namchukia Babangu" kwenye diwani ya *Alidhani kapata na hadithi nyingine* anaeleza jinsi msichana mdogo kwa jina Kichomi alivyopata ugonjwa wa UKIMWI alipoanza kuwawinda wanaume ili atafute chake. Hii ni baada ya baba mzazi kukataa kujukumika katika malezi ya wanawe jambo ambalo lilisababisha kifo cha nduguye Kichomi kwa jina Mafutu na wengine kutorokea mjini kuwa watoto wa mtaani. Huku ndiko Kichomi alianza kuwatafuta wanaume na kuhusiana nao kimapenzi ili aweze kujikimu. Kwa mfano:

> Nako jijini, dadangu aliyeitwa Kichomi alianza kukoga vizuri na kuwawinda wanaume na hatimaye akapata chake. Alikodi chumba katika mtaa wa Majengo. Tangu siku alipotuacha na kuhamia huko, sikumwona tena. Miaka kadhaa baadaye, nilipata habari kuwa kala tunda lenye dudu baya na hatimaye akajifia. (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, uk 114)

Hata hivyo, hatua hii haikufika mbali kwani inasemekana kuwa mtoto huyu alivyoendelea kushiriki mapenzi na wanaume, alijipata kashiriki na aliye na virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UKIMWI na mwishowe akafa. Athari mojawapo ya kujihusisha katika mahaba ni kukumbana na ugonjwa wa UKIMWI.

Vile vile, Kichomi alikuwa ameiambukiza familia mpya ya baba yake ugonjwa huu. Baada ya watoto wake mzee M'mali kutorokea mjini alipokataa kuwajibika kama mzazi, mkewe aliaga kutokana na msongo wa mawazo. Mzee M'mali alioa bibi wa pili

ambaye alikuwa na wasichana wawili na wavulana watatu. Wasichana hawa walikuwa wa baba tofauti na wavulana. Kichomi alipogundua kuwa alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI kutokana na uhusiano wake na wanaume, aliamua kulipiza kisasi kwa baba yake. Kichomi alikuwa ameielewa familia hii vyema. Alianza uhusiano wa kimahaba na wavulana hawa wa mama wa kambo ambao nao walikuwa na uhusiano na wasichana waliosemekana si wa baba mmoja. Kwa kuwa paka mzee alitaka kunywa maziwa, mzee M'mali alikuwa na uhusiano wa kimahaba na mabinti hawa ambao alijiambia si wanawe halisi. Hivi ndivyo ugonjwa huu ulisambaa katika familia ya pili ya mzee M'mali. Walionekana wakipitana hewani kwenda na kutoka ng'ambo kwa matibabu. Hapa ni nukuu:

> "Ugonjwa upi huu usiosikia dawa? Na mbona ukaikumba jamaa nzima? Ama ni walichokila? Au kunywa? Au hata kuonja! Baba, mama, kaka, dada wote hupitana angani-huyu yuaelekea Urusi, yule atoka huko." (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 116)

Ugonjwa usiosikia dawa kwa mujibu wa mwandishi huyu ulikuwa ugonjwa wa UKIMWI. Ugonjwa huu ulisababishwa na uhusiano wa kimahaba kiholela.

Pendo kwenye hadithi ya "Safari ya Maangamizi" aliambukizwa ugonjwa wa ukimwi kutokana na kubakwa na wanaume watano. Alipogundua kuwa alikuwa kaambukizwa ugonjwa huu, aliamua kulipiza kisasi kwa kushiriki ngono na wanaume wengi awezavyo bila kubagua yeyote kwa umri wala kwa tabaka. Aliwaangamiza wengi kwa kuwanasa katika mtego wake. Wengi waliangalia urembo wake na kuingia mtegoni barabara. Alisema:

> "Umbo langu bado lilikuwa la kutamanika. Wengi walilitamani na kuomba urafiki nami. Sikuwakatalia. Niliapa kuwanasa wengi tu kwenye ulimbo. Nilikuwa nimeanza safari ya mangamizi." (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 170)

Wote waliohusiana kimapenzi na Pendo, wakubwa kwa wadogo walikuwa wameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kwani alikuwa amebeba virusi vile kutokana na ubakaji. Wote waliambukizwa. Anasema:

> Wengi walikuja kujifurahisha kwa kuogelea baharini. Waliogelea na kucheza ufukweni. Wana wa Adamu wa umri, jinsia na matabaka mbalimbali. Wanafunzi wa shule za upili, wa vyuo vikuu, madaktari, viongozi wa kisiasa, wahadhiri, walimu, watalii kutoka nchini za mbali, viongozi wa kidini, polisi, walevi, wavuvi, wavuta rukwama…Wote

> hawa sasa wanasubiri kutumbukizwa kaburini. Wachimba kaburi nna kazi kubwa! (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 171).

Timammy kwa upande wake katika hadithi ya "Shimo la Maisha" anaeleza jinsi dada yake Hamisi aliuuza mwili wake tena kwa bei nafuu kama mtumba ili aweze kuyakidhi mahitaji yake na nduguye Hamisi. Hii ni baada ya kugundua kuwa biashara aliyokuwa ameianzisha ya kuuza nguo za mitumba haikuwa inafanya vyema. Kujiuza huku kwa kushiriki ngono na wanaume kulimsababishia kubeba virusi vya ugonjwa wa UKIMWI. Baadaye, mtoto huyu aliaga kutokana na ugonjwa huu wa ukimwi. Nduguye Hamisi anasema:

> Kwa hivyo, dadake alipoamua kuingia katika biashara ya nguo za mitumba, moyoni alijiambia kuwa angesoma kwa bidii ya mchwa ili nguvu za nduguye zisipotee…Maskini dadake alianza kuugua. Alianza kumumunyuka kama udongo. Nguvu zilianza kumwishia na biashara yake ikaanza kuzorota. Katika kule kuuza, aliuza zaidi ya nguo za mitumba kwa kuwa biashara ile haikuweza kukamilisha mahitaji yao yote, ikambidi yeye mwenyewe kuwa 'mtumba'. Katika biashara hiyo alijipata taabani na ugonjwa wa ukimwi. (*Alidhani Kapata na Nyingine*, 2007, Uk 77).

Kwa mujibu wa dondoo hizi, uhusiano wa kimahaba wa kiholela unasababisha ugonjwa wa UKIMWI. Mwishowe, mwathiriwa hufa. Ugonjwa huu haubagui umri wala jinsia. Watoto pia wanafaaa kuhamasishwa kuhusu ugonjwa huu na athari zake.

### 4.2.10 Ukosefu wa Amani Katika Familia

Mafanikio ya familia yeyote ile uchangiwa pakubwa na amani. Amani ni ule utulivu na kuwa na mwelekeo mmoja katika familia au maisha. Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni zinachangia ukosefu wa amani katika familia zilizoathirika. Imani potovu huweza kumuona mwanamke kama kisababishi cha hali hii.

Rhoda Nyaga, mwandishi wa hadithi fupi ya "Kanda la Usufi" anaeleza jinsi familia ya mzee Butali ilikosa amani kutokana na uja uzito wa Sela. Sela alikuwa mwanafunzi katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo. Sela alijihusisha na uhusiano wa kimahaba angali mwanafunzi uhusiano ambao ulimsababishia kupata uja uzito wa mapema na usiotarajiwa. Baada ya kugundulika kuwa alikuwa mja mzito, wazazi wake Sera waliombwa kufika shuleni ili kupashwa habari ile. Ukosefu wa amani katika

familia hii ulianza moja kwa moja mzee Butali alipoipata habari ile kama ilivyo katika nukuu hii:

> Boma la mzee Butali liligeuka jahanamu baada ya kutoka shuleni. Mzee Butali aliwazulia majojo Sela na mama yake. Majirani nao walishuhudia bughudha hizo kwa mbali. Mzee Butali alichanganyikiwa asijue la kufanya. Hakuwahi kufikiria hali kama ile ingetokea nyumbani kwake. 'Leo ndio mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti? Sikutumia hela zangu mimi katika elimu yake hadi nikaitwa pangu pakavu? Mtwae kilicho chenu mniondokee!' (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 63

Kwa mujibu wa nukuu hili, ukosefu wa amani katika familia ya mzee Butali ulisababishwa na ujauzito wa Sela. Baba yake hakuwa anaamini kuwa uja uzito utotoni ungetokea katika familia yake. Alihusisha ujauzito huu na ukosefu wa uwajibikaji wa mama mzazi. Hivyo lawama zote zilielekezwa kwa mkewe na mwanawe.

### 4.2.11 Kunyimwa Nafasi ya Kukaa na Mwanao

Mtoto anapozaliwa, anafaa kukaa na mama mzazi kama mlezi wa kwanza na pia kukuza upendo wa mama na mtoto. Mtoto anapozaliwa na mtoto mwingine, huenda nafasi hii isipatikane. Watoto hawa hupata walezi wapya ambao wakati mwingine huchukua nafasi ya mama mzazi ata katika kujitambulisha.

Kananda alimpata mwanawe Mwakitawa akiwa na umri mdogo. Kristina Mbai anatueleza haya katika hadithi yake "Mwana wa Darubini" katika diwani ya *Damu nyeusi na Hadithi nyingine*. Kananda alikuwa kijakazi nyumbani mwa Mwatela na Maria. Alimpata mwana huyu kupitia kunajisiwa na Mwatela siku ambayo Maria alikuwa ameenda kuwatembelea wazazi wake mbali jijini. Mwatela alikuwa amemuahidi msichana huyu kuwa angemuoa mara tu ajifunguapo. Badala ya kutimiza ahadi yake baada ya kujifungua, Mwatela alitenda yafuatayo:

> Kananda alipata mtoto wa kiume. Bwana Mwatela hakumuoa Kananda kama alivyoahidi. Badala ya kumuoa, alipanga njama ya kinyama. Alijuana na mtu mmoja kutoka Kongo ambaye alikuwa dereva wa malori makubwa ya shehena. Alimnyang'anya Kananda mwanawe. 'Mchukue mwanamke huyu ukamfanye mkeo,' Mwatela alimwambia dereva (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 100).

Nia yake Mwatela ni kuwa na mtoto na siri ya kuwa alikuwa baba wa mtoto yule isijulikane. Hii ndio sababu aliamua kumuuza Kananda kwa kumnyang'anya

mwanawe. Hapa, Kananda alinyimwa nafasi ya kukaa na mwanawe. Mtoto huyu alipokua alimjua Mwatela kuwa baba yake naye Maria kuwa mama. Hata hivyo ukweli ulibainika baadaye Kananda alipokombolewa na kurejeshwa nchini na kuanza harakati za kumtafuta mwanawe.

Pia, Sela katika hadithi ya "Kanda la Usufi" alikuwa hana nafasi bora ya kukaa na mwanawe. Hii ni kwa sababu baada ya kujifungua na kukaa nyumbani kwa miezi mitatu alirudi tena shuleni. Jukumu la kumlea mwanawe lilipewa Rozina haratiye mwanawe Kadogo. Hata baada ya kukamilisha masomo na kuenda kuishi na Masazu kama bibi na bwana, alikuwa na wakati mrefu kumpata mwanawe. Hii ni kutokana na umaskini waliokuwa nao Sela na Masazu na hivyo hawangemudu njia bora ya kumwendea mwanao. Hili linadhihirishwa na maneno yafuatayo:

> "Masazu alielewa hangemudu utaratibu wa kawaida wa kuenda kwa wazazi wa Sela. Kutokana na misingi hiyo, mpango kabambe ulipangwa…" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 64)

Mpango unaorejelewa hapa ni ule wa kuweza kumchukua mwanao bila kufuata taratibu zinazofaa. Walifanya mpango na Rozina ili awakabidhi mwanao bila ya wazazi wake Sela kujua. Mambo haya yote yalichangiwa na ukosefu wa nafasi ya kukaa na mwanao.

#### 4.2.12 Kutomakinika Masomoni

Uhusiano wa kimahaba miongoni mwa watoto umesababisha ukosefu wa umakinikaji masomoni. Hii ni kutokana na mafikira kadha ambayo huwajia akilini ya kutafuta suluhisho. Uanafunzi na uhusiano wa kimahaba utotoni ni shughuli mbili kwa wakati mmoja na lazima moja iathirike. Masomo huathirika kwa sababu ya ukosefu wa utulivu darasani ambao husababisha matokeo duni. Mokua (2020) alitoa mawaidha kwa wanafunzi kuwa uhusiano wa kimapenzi ungeyeyusha masomo yao na hivyo wayaepuke. Msichana anapojua kuwa amekuwa mja mzito hali hubadilika kabisa na anashindwa kumakinika darasani. Hii ndio sababu wengine hufanya uamuzi wa kuacha shule.

Rhoda Nyaga katika hadithi ya "Kanda la usufi" anaieleza athari hii. Sela na Chris Masazu walikuwa na uhusiano wa kimahaba wangali wanafunzi. Uhusiano huu

ulimpelekea Sela kuwa mja mzito akiwa katika kidato cha pili. Sela alihofia sana kuwa mja mzito na hivyo hakuweza kumakinika tena masomoni. Kwa mfano;

> Muhula wa tatu wa kidato cha pili ulipoanza Sela alijiunga na wanafunzi wengine. Mwezi wa kwanza wa muhula uliisha. Ulipoisha akathibitikiwa na kile alichohofia katika uhusiano wake na Masazu. Kijusi kilikuwa kimetungika! Hapakuwa na nafasi ya kugeuza mambo. Sela alidhurika sana kutokana na hali yake. Hakuwa na utulivu masomoni. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61)

Chris vile vile alipoipokea habari kuwa Sela alikuwa mja mzito, hakuweza kutunza makini shuleni pia. Mfano:

> "Sela alimwandikia Masazu barua ya kumjuza hali ya mambo. Masazu alipoipokea, aliisoma mara ya kwanza. Akairudia mara ya pili na ya tatu. Ukweli ukambainikia. Ukweli huu uimuathiri kiasi kwamba naye hakuweza kutunza makini yake masomoni" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine, 2007,* Uk 61).

Hadithi ya "Safari ya maangamizi" na Julius Gichamba katika diwani ya *Kurudi nyumbani na hadithi nyingine* (2007) inaendeleza hoja hii. Pendo alipojipata kabakwa na wanaume watano na kumuambukiza virusi vya UKIMWI aliapa kulipiza kisasi. Alikuwa mwanafunzi mzuri mchana lakini usiku alikuwa katika harakati za kulipiza kisasi. Anaeleza;

> "Mchana nilikuwa mwanafunzi stadi ilhali usiku nilikuwa katika mstari wa mbele kuona kuwa jamaa wanafagiliwa. Nia yangu haikuwa kupata tija. La hasha! Ilikuwa ni kuwaogesha wana wa Adamu kwenye bahari ambayo tayari walikuwa wameichafua wao wenyewe" *(Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 170).

Katika mifano ya hapo juu, waandishi wa hadithi fupi teule wamerejelea visa ambapo watoto wameshindwa kumakinikia masomo yao kwa sababu ya kuwa wahanga wa uhusiano wa kimahaba utotoni na pia kuwa wajawazito wangali shuleni. Katika "Kanda la Usufi", Sela alikuwa mjamzito katika kidato cha pili. Hakuweza kumakinika darasani tena. Vilevile, mpenziwe Masazu alikosa kutunza makini masomoni alipofahamishwa kuhusu habari hizo. Pendo katika *Safari ya Maangamizi* hakutilia masomo maanani tena baada ya kuhusishwa mahaba ya kulazimishwa kwa kubakwa na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI. Hakuwa na nia ya kuwa mwanafunzi sasa bali kulipiza kisasi kwa kujihusisha mahaba na wanaume wengi awezavyo hili nao wapate kuambukizwa ugonjwa ule. Wanajamii wanapaswa kupinga uhusiano wa kimahaba miongoni mwa watoto jambo ambalo litakuza umakinifu wao masomoni.

### 4.2.13 Kuachishwa Kazi

Kazi ni kile mja hufanya ili kujipa kipato cha kila siku. Kuna aina nyingi za kazi zikiwemo za kibarua na zile za kiofisi. Malipo katika kazi hizi hutegemea mwajiri. Wengine watawalipa wajiriwa wao kila siku, baada ya wiki na wengine mwisho wa kila mwezi. Kila mwajiri huwa na sheria zake kwa wafanyakazi wake ili kuwe na utendakazi bora. Sheria hizi zikikiukwa huenda matokeo ya kazi yake yakawa duni. Ni wajibu wa kila mwajiri kuhakikisha kuwa sheria hizi zinazingatiwa na waajiriwa wote. Mwajiriwa anapozikiuka kanuni zile, kuna matokeo mbalimbali ya adhabu yakiwemo kuachichwa kazi. Kuna waajiri ambao pia uwadhulumu wafanyikazi wao na matokeo yake yakawa ni kuwaachisha kazi ili wasitambulike. Licha ya haya, ajira kwa watoto ni ukiukaji wa haki za watoto kwani ni kuwadhulumu, (Mayieka 2015). Njia mojawapo ya kuwadhulumu wafanyikazi hasa wasichana ni kuwaajiri na pia kuwa na uhusiano wa kimahaba nao.

Kristina Mbai ni mwandishi wa hadithi ya "Mwana wa Darubini" katika diwani ya *Damu nyeusi na hadithi nyingine*. Katika hadithi hii, Bwana Mwatela anamwajiri mtoto aitwaye Kananda kama kijakazi. Mwatela alikuwa mumewe Maria na babake Sami. Hivyo, Kananda alipewa jukumu la kumtunza mwanao Sami. Hata hivyo, mwajiri huyu alianza tabia za mara kwa mara za kumchokoza Kananda kwa kutaka awe na uhusiano wa kimahaba naye. Siku moja, Maria alipokwenda kuwatembelea wazazi wake, Mwatela alimnajisi Kananda kitendo ambacho kilimfanya kuwa mja mzito. Mwatela alipofahamishwa kuhusu uja uzito huu, alijaribu kwa hali zote bibi yake Maria asijue. Alimuahidi Kananda kuwa angemuoa kama bibi wa pili baada ya kujifungua iwapo angeiweka kuwa siri. Alimwambia Kananda amwambie Maria ya kwamba uja uzito huo ulikuwa wa rafiki yake mvulana wa huko kijijini alikotoka. Kananda alifuatilia yote aliyoambiwa na mwajiri wake. Alipojifungua mambo yalikuwa tofauti. Mwatela alimnyang'anya mwanawe na kumpeana kwa dereva wa malori makubwa ya shehena kutoka kongo ili amfanye bibi yake. Kwa mfano:

> "Mchukue mwanamke huyu ukamfanye mkeo" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 100)

Matokeo ya uja uzito wa Kananda yalikuwa ni kufutwa kazi na kukabidhiwa dereva wa malori. Kuachishwa kazi kwa Kananda kulitokana na makosa ya mwajiri mwenyewe ya kukosa kuwaheshimu waajiri wake. Pia alifanya kosa la kumwajiri mtoto. Ni wito

kwa waajiri wote kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anaajiriwa. Pia, waajiri wanaowadhulumu waajiri wao wachukuliwe hatua ya kisheria.

Mfano mwingine humo katika hadithi ya “Malimwengu”. Lozi alikuwa mtoto yatima ambaye hakuweza kuendeleza masomo yake ya shule ya msingi baada ya kufiwa na wazazi wake na kuachwa mikononi mwa shangazi Mashaka. Aliachishwa shule na kuwa kijakazi pale kwa shangazi Mashaka. Mateso na matusi yalizidi pale. Aliamua kwenda mjini kujitafutia chake. Mle mjini alipatana na wanaume matajiri ambao walimweka maisha ya starehe. Hata hivyo mwajiri wake hakufurahishwa na matendo yake ya ukahaba. Alimfuta kazi. Matendo yale pia yalikuwa yamempa mimba. Mfano:

> “Mchukue huyu kahaba wako umpelekee watu wengine. Mimi ninamsaidia, naye kazi yake kuniaibisha” (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 32)

Haya yalikuwa maneno ya mwajiri wa Lozi bwana Pacha. Alikuwa anamwambia Furaha ambaye alikuwa amemtafutia Lozi kazi pale kwa kampuni yake. Baada ya maneno haya yafuatayo yalitendeka:

> “Mara mlango ukafungwa kwa nguvu, Pacha akarudi ndani. Furaha aliposaili Lozi, alifahamishwa kuwa alikuwa amepigwa kalamu na pia kufukuzwa kwa ile nyumba. Kisa na maana? Lozi alikuwa mjamzito” (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 32)

Dondoo hizi ni dhihirisho kwamba Lozi aliachishwa kazi kwa sababu ya kushiriki mahaba angali kazini. Isitoshe, Lozi alikuwa mtoto na mja mzito. Athari ya kujihusisha mahaba kulimsababishia kufutwa kazi na pia kuwa mja mzito utotoni.

### 4.2.14 Kuacha Shule

Kila mwaka, watoto wengi wasichana huripotiwa kuacha shule. Sababu za watoto hawa kuacha shule kabla ya kukamilisha masomo yao huwa nyingi. Nchini Tanzania, wasichana laki nane huacha shule kutokana na kuwa na ujauzito kila mwaka. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya HakiElimu (2011). Kiarie (2015) anaeleza kuwa sababu mojawapo ambayo huwafanya watoto wa kike kuacha shule huwa ni mimba za mapema. Pia, ripoti ya Shirika la Kimataifa la Human Right Watch (2016), Tanzania, iliyopewa jina “Nilikuwa na ndoto ya kumaliza shule,” ilionyesha kuwa asilimia 40 ya wanafunzi nchini humo hukatiza masomo yao ya sekondari kutokana na ujauzito.

Isitoshe, Mutheu (2020) alieleza kuwa mimba za mapema hufanya wasichana kupata changamoto kama vile kuwalazimu wasiendelee na masomo.

Watoto hawa wanapokuwa waja wazito wangali shuleni uona aibu ya kuendelea na masomo. Wanaanza jukumu la kuwa wazazi na kusahau kuwa walikuwa wanafunzi. Wengine wanapojipata katika hali hii hujiingiza katika ndoa za mapema ili wasionekana kwamba uhusiano wao ulikuwa nje ya ndoa.

Rhoda Nyaga katika hadithi yake ya "Kanda la Usufi" anaonyesha jinsi mtoto Sela na wenzake wawili hawangeweza kuendelea na masomo yao katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo baada ya kugundulika kuwa walikuwa waja wazito. Ilikuwa desturi katika shule hii ya wanafunzi kukaguliwa iwapo walikuwa waja wazito kila mwanzo wa muhula wa kwanza. Ni kutokana na desturi hii ambapo ukaguzi ulifanywa Sela akiwa muhula wa kwanza wa kidato cha tatu na kupatikana yeye na wenzake wawili wakiwa wajawazito. Wazazi wao waliombwa kufika shuleni mara moja na uamuzi wa kuombwa watoke shuleni mle ulitolewa. Mfano:

> Baada ya mazungumzo kati ya mwalimu mkuu na wazazi wa Sela, uamuzi ulitolewa. Sela na wenzake wawili hawangeweza kusoma pamoja na wengine baada ya hali zao kubainika. Bi. Margaret alipendekeza watafutiwe shule za kutwa karibu na watokako ili waendelee kusoma huku wazazi wakiwatunza. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 62-63)

Watoto hawa wasingeendelea kusomea shuleni humo kwani walikuwa wamevunja sheria za shule hiyo. Vile vile, utunzaji ambao wangehitaji katika hali hiyo usingepatikana shuleni humo. Sela alikaa bila kuhudhuria masomo kwa majuma matatu kwani baba yake alimfukuza nyumbani pamoja na mama yake hadi pale alipata kushawishiwa na wazee na kuwakubali tena. Baada ya shule kupatikana Sela alianza kuhudhuria masomo hadi pale alishindiwa na kuenda kujifungua. Baada ya kujifungua, tena alikaa nyumbani miezi mitatu kabla ya kurudi shuleni tena. Mfano:

> "Sela alikaa nyumbani kwa muda wa miezi mitatu akikitunza kitoto chake" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 63).

Muda huu wote ambao Sela alikaa bila kuenda shule na pia harakati za kubadilishiwa shule ulitokana na uhusiano wa kimahaba utotoni ambao ulichangia mimba ya mapema. Jambo hili lingeepukika kwa kutoshiriki mahaba utotoni.

Mohamed Khelef katika hadithi yake ya "Mame Bakari" anaonyesha vile mimba ya mapema ingelivyomsababishia Sara kufukuzwa shuleni. Sara alibakwa usiku mmoja wa bahati mbaya akitoka masomo ya usiku. Alishindwa kuwaambia wazazi wake kilichotendeka kwa sababu aliona kuwa lawama zote zingeelekezwa kwake. Alisema:

> "Kila siku linapotokezea jambo la mwanamke kubakwa basi mwanamume hana kosa. Mwanamke ndiye shetani**"** (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 48).

Basi aliamua kujinyamazia. Baadaye, alifahamu alikuwa mjamzito. Mafikira mengi yalimjia na kuona jinsi angefukuzwa shuleni kwa kuwa alikuwa mjamzito. Hakuona haki ikitendeka popote pale nyumbani na shuleni. Alisema kuwa mwalimu mkuu pale shuleni angekuwa na haya ya kumwambia:

> "Hii ni skuli ya wanafunzi, mama, sio ya wazazi. Hatufundishi wanawake hapa, tunafundisha wasichana. Na wewe 'mama' yaonesha umeshakuwa ulivyotaka kuwa. Sasa skuli haina maana na wewe. Wewe ni mwanamke, ni mama kamili, basi bora wende ukasome maisha mbele ya safari" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 49).

Kutokana na maelezo haya, watoto huacha shule wanapokuwa waja wazito ili kuzuia maneno kama haya kutolewa mbele yao hadharani. Jamii inachukulia shule kama mahali pa kusomewa na wasichana tu na bali si msichana aliye na mimba. Mtazamo huu uwanyima watoto wengi nafasi ya kuendeleza masomo yao na kuwafanya kuacha shule wanapogundua kuwa waja wazito. Jamii inafaa kufahamishwa kuwa si ujauzito wote huja kwa sababu mtoto alikuwa na uhusiano wa kimahaba wa hiari ila wengine hujipata wajawazito kutokana na kulazimishwa. Vilevile, kuwaongoza watoto vifaavyo ni muhimu kuliko kuwafukuza shuleni.

### 4.2.15 Majuto

Uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema usababisha majuto katika maisha ya waathiriwa. Waandishi wa kazi teule wameyaangazia majuto haya. Kwa mfano:

> "Aliwaza na kuwazua kuhusu ile mimba. Angemwelezea nini Bibi ambaye alimuenzi mno? Alijuta kwa aibu aliyomletea." (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 34)

Katika dondoo hili, Lozi alijuta kwa kujihusisha na ukahaba na kuwa mja mzito. Alikuwa ameenda kutafuta ajira akiwa na umri mdogo ili kujikimu baada ya kufiwa na wazazi wake na kuachishwa masomo katika shule ya msingi na mlezi shangazi

Mashaka. Pale mjini alijihusisha mahaba na mwishowe kujipata mja mzito. Nyanya yake aliyeitwa Bibi pale nyumbani alimuenzi sana. Lozi alijutia jinsi angemwambia kuwa alikuwa mjamzito na kwa aibu aliyokuwa amemletea Bibi.

> Sela alidhurika sana kutokana na hali yake. Hakuwa na utulivu masomoni. Hakujua maisha yake yangechuka mkondo upi. Mzo wa majuto ulimwandama. Ulimwengu wake ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61)

Katika dondoo hili, Sela alijihusisha na mahaba angali mwanafunzi wa kidato cha pili na mvulana wa shule jirani. Katika muhula wa tatu wa kidato cha pili, Sela alikuwa mja mzito. Alijutia matendo yake kwani hakujua maisha yake yangekuwa vipi.

### 4.2.16 Kisasi

Kulipiza kisasi ni athari nyingine ya uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Watoto wanapodhulumiwa kimapenzi wanaweza kuapa kulipiza kisasi. Kwa mfano, Pendo katika hadithi ya "Safari ya Maangamizi" anafanya uamuzi wa kulipiza kisasi dhidi ya wanaume kwa sababu ya kushirikishwa mahaba kwa kubakwa. Mtoto huyu alikuwa amebakwa na wanaume watano waliovalia vinyago wasitambulike. Isitoshe, ubakaji huu ulimwambukiza Pendo ugonjwa wa UKIMWI. Mtoto huyu alijishirikisha na mahaba na wanaume wengi alivyoweza kwa nia ya kulipiza kisasi unyama aliotendewa.

Sara katika hadithi ya "Mame Bakari" alikuwa na moyo wa kulipiza kisasi pia. Mtoto huyu alikuwa amebakwa usiku mmoja akitoka katika masomo ya ziada na kusababishiwa ujauzito. Hata baada ya kujifungua, alitamani kuliona janadume lililomtendea unyama huo. Hii ndio maana siku moja aliposikia kelele za kuliadhibu jitu lile alibeba tofali tayari kuliangamiza pia.

Isitoshe, Kichomi katika hadithi "Namchukia Babangu" alihapa kulipiza kisasi kwa baba yake mzazi kwa sababu alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kutokana na kujihusisha kimahaba ili ajikimu. Hii ni baada ya baba yake kukataa kuwajibikia malezi yake na yale ya ndugu zake licha ya kuwa mkwasi mtajika.

Kw mujibu wa maelezo ya hapa juu, athari mojawapo ya uhusiano wa mahaba na mimba za mapema ni kuwa na nia ya kulipiza kisasi. Kulipiza kisasi huku ni hatari

kwani kunaweza kuangamiza waliohusika na wasiohusika kama alivyofanya Pendo na pia Kichomi. Watu wengi waliambukizwa ugonjwa wa UKIMWI hata wale wasiokuwa katika mstari wa kuadhibiwa.

### 4.3 Hitimisho

Sura hii iliangazia jinsi suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni lilivyoathiri jamii kwa mujibu wa waandishi wa hadithi fupi teule. Utafiti huu ulitambua kuwa miongoni mwa athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema ni kuacha shule, kufukuzwa nyumbani, kutomakinika masomoni, kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi, vifo, kisasi na mimba isiyotarajiwa. Vilevile, ilibainika kwamba athari mabalimbali zinatokana na visababishi mbalimbali. Hali kadhalika, imegunduliwa kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema na athari zake. Madhara ya uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema si ya waathiriwa pekee bali ni athari kwa maendeleo ya nchi mzima. Katika sura iliyofuata, mtafiti aliangalia mtazamo wa waandishi wa hadithi fupi teule kuhusu suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

# SURA YA TANO

# FALSAFA YA WAANDISHI KUHUSU SULUHU KWA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI

## 5.1 Utangulizi

Falsafa ya mwandishi ni msimamo wa msanii kuhusu jambo fulani. Kuna baadhi ya mapendekezo yanayotolewa na jamii katika kulitatua suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Mapendekezo haya yanatolewa na viongozi mbalimbali na vyombo vya habari. Kwa mfano, Mutheu (2020) anaeleza maoni ya viongozi kuhusu kulikabili suala la mimba za mapema. Mapendekezo yao ni pamoja na kuwapa wasichana elimu ambayo itawasaidia kujiepusha na ngono za mapema, elimu kuhusu uzazi kujumuishwa katika silabasi, wahudumu katika vituo vya afya kuunda mazingira yanayowezesha vijana kuongea kuhusu matatizo yao, kutolewa kwa tembe za kuzuia mimba bila malipo, sheria zote za kulinda watoto kutokana na vitendo vya ngono vifuatiliwe na pia kuwahamasisha wanajamii kuhusu tamaduni potovu kama vile ukeketaji wa wasichana.

Isitoshe, kuna ripoti za mara kwa mara katika vyombo vya habari yakiwemo magazeti kuhusu watu waliofunguliwa mashtaka kutokana na kushiriki ngono na watoto na wengine kuadhibiwa vikali na wanajamii. Kwa mfano, Ominde na Chepkemboi (2020) walitoa ripoti kuhusu wanaume watatu waliokuwa kizimbani kwa madai ya kuwanajisi watoto wa umri mdogo. Munene (2020) anaeleza jinsi pasta alivyoshtakiwa kwa kosa la kuwapachika binti wake wawili mimba. Hii ni dhahiri kuwa wanajamii wana mtazamo kuwa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni janga linalohitaji suluhu na wana namna mbalimbali za kukabiliana nalo.

Vivyo hivyo, waandishi wa fasihi ya Kiswahili wana maoni yao kuhusu suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kwa mfano, Kavuria (2008) anapendekeza baadhi ya suluhu hizi kama; uundaji wa vyama vya kutetea maslahi ya watoto, jamii kuwashauri wanajamii wengine wanaotekeleza dhuluma dhidi ya watoto, jamaa kuchukua jukumu la kuwasaidia watoto wanaodhulumiwa, serikali kutunga sheria mwafaka zinazoweza kulinda haki za watoto, na pia watoto kuwa na jukumu lao binafsi la kusimama wima kupinga dhuluma zinazowakabili. Kiarie (2010) ana suluhu kuwa wazazi waweze kuzungumza na wanao kuhusu ushiriki mapenzi ili waweze kujiepusha nalo mapema.

Waandishi wa hadithi fupi teule wana msimamo wao pia kuhusu suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Madhumuni ya tatu katika utafiti huu yalikuwa kujadili falsafa ya waandishi wa kazi teule za Kiswahili kuhusu suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Waandishi wa hadithi fupi teule wamejadili mbinu mbalimbali za kukabiliana na suala hili kutegemea kisababishi na pia athari yake kwa jamii. Mbinu hizi ni kama zifuatazo:

### 5.1.1 Kuweko na Sheria ya kutoa Adhabu kali kwa Wanaoshiriki Mapenzi na Watoto

Nchini Kenya, kuna sheria zinazowalinda watoto zikiwemo sheria za watoto mwaka 2012, sheria za Katiba ya Kenya (2010) na zile za bunge. Hata hivyo, sheria hizi zimekiukwa au hata kupuuzwa mara kwa mara na kuwafanya watoto kutopata haki zao wanapodhulumiwa kimapenzi. Onyango (2014) anaeleza jinsi kesi za watoto wawili walionajisiwa na jirani yao zilivyotupiliwa mbali kwa njia isiyoeleweka katika kaunti ya Vihiga. Katika kaunti hiyo hiyo, msichana mwenye umri wa miaka kumi na minne alikuwa na ujauzito wa kutungwa na babu yake wa miaka sitini na minne na kesi yake haikuzingatiwa vifaavyo. Mtoto aliye na ulemavu wa kiakili pia aliripotiwa kunajisiwa na jamaa yake mara ya kwanza akielekea shuleni na ya pili akielekea dukani. Visa hivi vyote havikusikizwa vifaavyo kwani vyote vilitupiliwa mbali mahakamani kwa njia ya kutatanisha. Ongezeko la waathiriwa wa mimba za mapema ulichangia Muungano wa Kitaifa wa Wazazi Nchini Kenya (2019) kubaini mbinu za kukabiliana na mimba za mapema kwa kupendekeza kuwa vyombo vya serikali vianze kuwakamata na kuwachukulia hatua kali wanaohusika na mimba hizi kwa mujibu wa sheria.

Waandishi wa kazi teule wana msimamo wa kuwa na sheria inayotoa adhabu kali kwa wanaowadhulumu watoto kimapenzi. Kwa mfano, mwandishi wa hadithi ya "Shetani hana hatia" anatoa msimamo huu akimrejelea mhusika Pakashume ambaye alikuwa amemdhulumu mtoto kimapenzi. Pakashume aliyekuwa nduguye baba Toto alikuwa shambaboi pale kwa ndugu yake. Pakashume alipewa jukumu lingine la kumchukua mpwa wake Toto kutoka shule ya chekechekea ya pale karibu na nyumbani kwa sababu ya ukosefu wa usalama katika mtaa kwani kulikuwa na visa vingi vya ubakaji wa watoto. Siku moja, Pakashume alipokwenda kumchukua mtoto huyu na kufika njiani aliingiwa na unyama na kumbaka malaika Toto. Toto alinusuriwa na wapita njia ambao

walimshika Pakashume na kumwadhibu. Aliponusurika kifo kutokana na wapita njia waliokuwa na hamaki, alijipata hospitalini kwa ulinzi mkali wa askari. Pale, nesi wawili Waridi na Vundemile na daktari walienda kumuhudumia. Wanasikika wakijadiliana kuhusu sababu zinazochangia wanaume kuwabaka watoto wadogo. Hapa ni maneno ya nesi Vundemile:

> "Kwa hakika ni vigumu kuelewa ni kwa nini wanaume huwabaka watoto wanaohusiana nao" (Uk 62)

Katika kuendeleza mawasiliano yao, daktari alimjibu kama vifuatavyo;

> "Ni suala linalohitaji kutafitiwa kubainisha iwapo wabakaji huwa na matatizo ya kiakili au hata kisaikolojia" (Uk 62)

Kwa upande wake Waridi, alikuwa na yafuatayo ya kusema;

> "Unyama huu unaendelea kwa sababu hakuna sheria iliyotoa adhabu kali dhidi ya wabakaji. Wanafungwa miaka michache tu na kuachiliwa. Wengine wanapoachiliwa hurudia kufanya uhalifu ule ule." *(Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 62)

Isitoshe, mwandishi kupitia mhusika daktari anatoa hakikisho lifuatalo kumjibu Waridi;

> "Msitie shaka, hali hii itabadilika hivi karibuni…Kuna mswada wa sheria ambao utawasilishwa bungeni hivi karibuni. Kwa kweli nishausoma na nikafurahishwa nao. Utakapopitishwa, adhabu ya wabakaji itakuwa kali kiasi cha kuwakomesha kabisa." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 62)

Kwa mujibu wa dondoo hizi, bunge lina jukumu katika kukomesha dhuluma za kimapenzi dhidi ya watoto. Dhuluma hizi zikikoma, watoto watapata haki zao na pia mimba za utotoni hazitakuwemo. Bunge lina jukumu la kupitisha miswada na sheria ambazo zitakuwa na adhabu kali kwa wote wanaoshiriki mapenzi na watoto. Sheria hizi ziwe kali kwamba hakuna atakayeweza kuepuka mkono huo wa sheria wala kujaribu kurudia kosa hilo tena.

### 5.1.2 Wanajamii Washirikiane Kuwasaidia watoto Wanaodhulumiwa Kimapenzi na Kuwaadhibu Wanaowanyanyasa

Jamii ina jukumu katika kukomesha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kulingana na tamaduni za Kiafrika, mtoto humilikiwa na jamii bali si wa mtu binafsi. Ni wajibu wa wanajamii kuja pamoja na kuwalinda watoto dhidi ya dhuluma za kimapenzi zikiwemo dhuluma nyinginezo na kuhakikisha kuwa wanazitetea haki za

watoto. Kavuria (2008) anasema kuwa mojawapo ya suluhu kwa dhuluma za watoto ni kuchukua jukumu la kuwasaidia watoto wanaodhulumiwa. Waandishi wa hadithi fupi teule wanasadidia haya pia.

Mwandishi Matundura katika hadithi ya **"**Shetani hana Hatia" ni mmoja wa waandishi hawa. Anatoa suluhu ya wanajamii kushirikiana kuwaokoa watoto wanaohusishwa kwenye mahaba ya kulazimishwa na kuwaadhibu wanaoshiriki mapenzi na watoto. Kwa mfano:

> "Ndipo walimfikia watu waliokuwa wakikimbizana naye. Wacha waanze kumwadhibu. Vibao vilimnyeshea kama mvua." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61)

Hili ni dondoo linalomrejelea mhusika Pakashume aliyembaka mpwa wake aliyeitwa Toto akiwa ametoka kumchukua shuleni. Walipofika mahali pa kichaka, Pakashume alimgeukia mtoto huyu wa chekechea na kumbaka. Wapita njia walisikia kilio cha Toto akiomba msaada wa kuokolewa. Moja kwa moja walijifikisha pale na kumpata Toto akiwa hoi huku Pakashume akipandisha suruali yake tayari kutoroka. Walimkimbiza mbakaji huyu ambaye hakufika mbali kwani gogo lililokuwa njiani lilimwangusha na kufikiwa na watu hawa wenye hamaki. Walimwadhibu vikali kama ilivyo katika nukuu hapo juu.

Pakashume alinusuriwa na askari wawili ambao walipita mahala pale. Walimchukua na kumpeleka hospitalini. Walipokuwa wakimlinda pale hospitalini, askari hawa walikuwa na haya ya kusema;

> Tusingalikuwa hapa wangalimwandama hadi chumbani humu na kummaliza kabisa.
> Ni kweli maanake waliazimia kutopumzika hadi watu wa sampuli yake wamalizwe kabisa kutoka dunia hii." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 54)

Dondoo hili linadhihirisha kuwa wanajamii wana jukumu la kutochoka hadi pale watoto watakoma kudhulumiwa kimapenzi. Watu wazima ni sauti kwa watoto na hivyo wana nafasi ya kuwatetea. Katika hospitali mumo humo alimolazwa Pakashume, kulikuwa na nesi aliyeitwa Waridi. Waridi aliwaambia maafisa wa polisi waliokuwa wamemlinda Pakashume kuwa;

> "Mlifanya kosa sana kumuokoa. Alistahili kifo. Lingekuwa funzo kwa mamburukenge wengine wenye nia na tabia ya kuwavizia watoto wa kike, wanawake na maajuza na kuwanajisi." (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 56)

Vundemile alikuwa nesi pia katika hospitali hii. Yeye pia alishikilia msimamo wa kuwaadhibu wanaoshiriki mapenzi na watoto. Anapozungumza na afisa hawa wa polisi alikuwa na haya ya kuwaambia:

> "Mlifanya kosa kubwa sana kumuokoa. Mbona hamkuacha sheria ya mikononi ya papo hapo, imfunze kuwaheshimu wanawake na watoto wa kike?" (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 56)

Wahusika wote walionukuliwa wana msimamo wa kuwaadhibu wote wanaoshiriki mahaba na watoto. Wanapendekeza kutopumzika hadi watu wanaowadhulumu watoto kwa kushiriki nao mahaba kumalizwa duniani kupitia adhabu kali.

Mohammed Khelef katika hadithi ya "Mame Bakari" ana msimamo huu pia. Kwa mfano:

> "Mpigeni, mmalizeni, hakikisheni kwamba anamalizika kabla polisi hawajafika. Hawa ndio wanaotuharibia watoto wetu. Twanga! Piga! Sagasaga kabisa!" (*Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, Uk 54)

Dondoo hili lilitolewa kulirejelea janadume lililombaka Sara, msichana wa shule aliyekuwa akitoka katika masomo ya usiku. Pia, lilijulikana kwa kuwabaka wasichana wengine katika eneo hilo. Lilipewa adhabu ya kuuawa na wanakijiji kwa kupigwa matofali hadi kufa kama inavyodhibitishwa kwenye dondoo lifuatalo:

> "…mvua ya matufali ilianguka juu ya jimwili lile lililokuwa maiti kasorobo. Hujuma iliposita, jimwili lililozidi kumiminika damu lilipiga mapindi mawili matatu kisha likasita na kugeuka kitu kisicho na uhai." (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016 Uk 55)

Msimamo wa waandishi hawa wa kazi teule hapa ni kuwahamazisha wanajamii kukomesha suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za ututoni na kuwapa watoto mwanga wa kuendelea na maisha kupitia kuwaadhibu wanaodhulumu watoto kimapenzi. Mojawapo ya adhabu wanazoweza kuwapa wanaoshiriki mahaba na watoto ni kuwachapa na kuwapiga hadi wakaaga dunia kama lilivyofanyiwa jana dume

lililombaka Sara na wasichana wengine wa eneo hilo. Huu ni msimamo dhabiti ambao unaweza kukomesha ushiriki ngono na watoto.

### 5.1.3 Kuwaadilisha Watoto ifaavyo Kuhusu Suala la Kushiriki Mahaba

Ni wajibu wa wazazi na jamii mzima kuwaelekeza watoto katika njia inayofaa kuhusiana na uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Kwa maoni ya Kiarie (2015), wazazi wana jukumu la kuwaelekeza watoto kuhusu suala la ushiriki mahaba na kuwapa mawaidha vipasavyo. Ripoti ya Baraza Kuu la Makanisa Nchini Kenya (NCCK,2019) kwa Seneti kuhusu ongezeko la idadi ya watoto wanaopata mimba, inahimiza uzingatifu wa sheria kikamilifu kuhusu dhuluma kwa watoto, hasa dhuluma za kimapenzi. Ripoti hii inaeleza kuwa mimba za utotoni zinasababishwa na ulegevu wa nidhamu na maadili katika jamii. Baraza hili linasisitiza kuwepo na uwajibikaji wa wanajamii katika kuwaadilisha watoto.

Alifa Chokocho, mwandishi wa hadithi "Shogake dada ana Ndevu" ameweka jambo hili wazi kwa kutuonyesha madhara yanayoweza kutokea kutokana na kutowaadilisha watoto vyema. Safia alikuwa mtoto wa darasa la mwisho la kujiandaa kujiunga na kidato cha kwanza. Bwana Hasudi na Bi. Hamida walikuwa wazazi wake Safia. Wazazi hawa walimwamini mwanao kiwango cha kumwita malaika. Hawakuona jambo geni la kumwambia Safia kwani walisema kuwa Safia huwa halindwi bali hujilinda mwenyewe. Wakati mmoja, Safia aliwaomba wazaziwe ruhusa ya kumleta shoga yake Kimwana nyumbani kwa nia ya kudurusu pamoja. Wazazi hawa hawakuchukua nafasi yoyote kujisemezea. Walimwamini moja kwa moja kwa kumuona malaika na hata kuwapa ruhusa ya kujifungia chumbani peke yao walipodurusu. Hapa ni maneno ya wazaziwe Safia:

> "Acha aje Kimwana-walimwambia, maana hakuna cha kuogopa. Safia halindwi, hujilinda mwenyewe" (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 31).

Baada ya muda, Safia alikuwa mja mzito. Dalili za kutapikatapika na kuwa mnyonge zilidhihirika wazi kwa wazazi wake kuwa ni mja mzito. Hata hivyo Safia alikana kwa kusema kuwa ilikuwa tu homa ya malaria.

Maelezo ya mwandishi wa hadithi hii ni kuwa Safia alichukuliwa kuwa mtu aliyejielewa na wazazi wake na hivyo hakuhitaji mwongozo wowote katika maisha

yake. Msimamo huu hukuweza kumzuia kujihusisha na mahaba utotoni pengine kwa kuwa hakujua kuwa ni vibaya au hakuweza kujifanyia uamuzi bora. Wazazi wake pale walikuwa wamefeli katika kumwadilisha vyema kama njia ya suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema.

Isitoshe, Sela katika hadithi ya "Kanda la Usufi" alikosa mafunzo kuhusu maadili mema. Huko shuleni katika shule ya wasichana ya Askofu Timotheo, mwandishi hakutueleza lolote kuhusu mafunzo yanayotolewa kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za kimahaba na mimba za mapema. Jambo waliloliihimiza pale shuleni lilikuwa la kuwakagua wasichana ambao wangeweza kuwa waja wazito katika mwanzo wa kila muhula. Vilevile, pale nyumbani Sela hakupata mafunzo ya aina yoyote kuhusu uhusiano wa kimahaba. Alipogundulika kuwa alikuwa mja mzito mwanzo wa kidato cha tatu wazazi wake waliombwa kumwondoa katika shule ile. Kabla hawajaondoka pale, baba yake Sela alikuwa na hili la kumuuliza mwalimu mkuu,

> "Mwalimu, nina swali moja ambalo ningetaka unijibu. Je, ni kwa nini sisi huwaletea watoto shuleni?" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 63)

Walipofika nyumbani, baba yake alikuwa mkali na kuwaamrisha waondoke nyumbani mwake pamoja na mama mzazi. Alifoka;

> "Leo ndio mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?...Mtwae kilicho chenu mniondokee!" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 63)

Kwa mujibu wa maelezo hapo juu, inadhihirika kuwa wazazi na walimu wanafaa kutoa mafunzo kwa watoto kuhusu maadili mema katika jamii. Nchini Kenya, wazazi wengi wamewaachia walimu jukumu la kuwafundisha watoto wao kila kitu na kuwalaumu popote jambo liendapo kombo. Hii ndio maana baba yake Sela alimuuliza mwalimu mkuu wa shule ya wasichana wa Askofu Timotheo sababu yao kama wazazi ya kuwapelelea watoto. Aliwaona walimu kuwa wa kulaumiwa kwa kuwa binti yake alikuwa mja mzito jambo ambalo lilitokea wakati wa likizo. Ni vyema ijulikane kuwa kila mmoja ana nafasi yake katika maisha ya mtoto ikiwema kuwaadilisha vifaavyo. Ni tarajio la jamii kuwa wazazi wajukumike katika kuwaadilisha wanao kwa kuwa kielelezo bora kwao.

Iribe Mwangi katika hadithi “Namchukia Babangu” anaangazia suala hili kwa kuonyesha ukiukaji wa maadili wa hali ya juu ambapo baba anashiriki mapenzi na binti zake. Jambo hili si geni katika jamii. Munene (2020) anaeleza jinsi pasta alivyoshtakiwa kwa kosa la kuwapachika binti wake wawili mimba. Wazazi badala ya kuwa mfano mwema kwa watoto wao wanageuka kuwa wanaowadhulumu. Katika hadithi hii, Mzee M’mali alikuwa na uhusiano wa kimahaba na binti zake ambao walikuwa wa mke wake wa pili. Alifanya vile kwa madai kuwa hawakuwa wanawe halisi kwani alikuwa amemuoa mama yao akiwa nao. Nikinukuu:

> “Naye Mzee Mkata M’mali aliwaendea mabinti wale (hawakuwa wanawe halisi, halijituliza) na kwa kutumia mapesa yake akaweza pia kucheza ngoma goya nao” (*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine,* 2007, Uk 117).

Kwa mujibu wa yaliyoelezwa hapa juu, Mzeee M’mali alifaa jukumu la uzazi na kuwaadilisha wago bora kwao na wala sio kishiriki mahaba nao. Ni wajibu wa jamii kushirikiana katika kuwaadilisha watoto.

### 5.1.4 Watoto Kufundishwa Namna za Kujikinga na Mimba za Utotoni

Kujikinga ni mojawapo ya njia ya kuzuia mimba zisizotarajiwa. Baadhi ya njia za kujikinga ni pamoja na kusubiri bila kushiriki mapenzi hadi wakati wa ndoa, kutumia tembe, mipira au sindano za kuzuia mimba miongoni mwa njia nyingine. Njia hizi zinapatikana katika vituo vya afya nchini. Watoto wa kike hujiingiza katika mahaba ya mapema bila kujua chochote kuhusiana na kujikinga na wengi wanajipata kuwa wahanga wa mimba za utotoni. Hii ni kutokana na kutoadilishwa ifaavyo kama kisababishi cha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Pia, wengine hupotoka maadili na kushiriki mahaba utotoni. Hali hii imechangia mimba zisizotarajiwa. Kupitia elimu mwafaka, watoto hawa wanaweza kusaidika na kupunguza ushiriki mapenzi wa kiholela na hivyo kuzuia mimba za utotoni. Elimu hii inaweza kutolewa na wahudumu katika vituo vya afya, wazazi, walimu na mtu yeyote aliye na nia njema ya kumsaidia mtoto. Kwa mfano, Mutheu (2020) anaeleza kuhusu mapendekezo ya viongozi nchini ya kuomba vijana kupewa elimu kuhusu maswala ya uzazi ili waweze kujiepusha kupata mimba za mapema. Hili linaweza kufanyika kupitia kujumuisha suala hili katika silabasi za viwango mbalimbali.

Waandishi wa kazi teule wanaunga mkono suala la kujikinga kama njia mojawapo ya suluhu ya kukabiliana na mimba za mapema. Mwandishi wa hadithi “Kanda la Usufi”, Rhoda Nyaga anaangazia suluhu hii. Katika hadithi hii, Sela alikuwa mwanafunzi katika shule ya upili ya Askofu Timotheo. Alijiingiza katika uhusiano wa kimahaba na mwanafunzi wa shule ya upili ya Lenga Juu aliyeitwa Chris Masazu. Wakati wa likizo, watoto hawa walifanya mikutano ya faragha. Baada ya likizo ya mwisho wa kidato cha pili, Sela alikuwa mja mzito. Alidhurika sana kutokana na hali hiyo. Alimwandikia mpenziwe Masazu barua ili kumjulisha mambo yalivyokuwa. Masazu aliijibu barua ile. Hapa ni nukuu:

> “Masazu aliandika barua ya kujibu ile ya Sela. Katika barua alimuuliza ni kwa nini hakujikinga. Alimaliza kwa kuandika, ‘Yajapo yapokee’. Mimba ile kwa Masazu ilikuwa kanda la usufi. Sela alilia sana alipoisoma barua ya Masazu.” *(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 62)

Kwa mujibu wa dondoo hili, mojawapo ya suluhu ya mimba za mapema ni kujikinga. Mwandishi anamtumia mhusika Masazu kutuonyesha umuhimu wa watoto kujikinga wanaposhiriki mapenzi ili waweze kujiepusha na mimba za utotoni. Isitoshe, anaonyesha umuhimu wa kuwajibikia matendo yote. Sela alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili na haikuwa haki yake kujihusisha na mapenzi akiwa bado shuleni. Tendo la kushiriki mahaba lilikuwa kinyume cha matarajio ya wengi. Nchini Kenya, elimu dhidi ya kujikinga ili kutopata mimba za mapema linahitaji kutiliwa mkazo. Hili linaweza kusisitizwa kupitia kutoa elimu ya uzazi. Iwapo watoto watapata elimu kuhusiana na mbinu za kujikinga, wataweza kujiepusha na mimba za mapema.

### 5.1.5 Wanaume Wanaoshiriki Mapenzi na Watoto Wanyofolewe

Waandishi wa hadithi fupi teule wanapendekeza njia hii kama mojawapo ya suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Mwandishi Bitugi Matundura katika hadithi yake “Shetani hana Hatia” anaeleza jinsi Pakashume alishiriki mapenzi na mpwa wake Toto aliyekuwa mtoto katika masomo ya chekechea. Kitendo hiki kilitokea alipokuwa ameenda kumchukua shuleni. Walipokuwa njiani mahali kulikuwa na kichaka, Pakashume alimgeukia Toto na kumbaka. Wapita njia walisikia sauti ya kilio ya Toto ikitokea kichaka. Walikimbilia humo na kumpata Toto yu hoi naye Pakashume anajaribu kutoroka. Walimkimbiza Pakashume ambaye hakuenda mbali kwani gogo la

mti lilikuwa njiani na kumwangusha. Walipomfikia hali ilikuwa kama vifuatavyo kwenye nukuu hili:

> Ndipo walimfikia watu waliokuwa wakikimbizana naye. Wacha waanze kumwadhibu. Vibao vilimnyeshea kama mvua. Wanawake waliokuwa kwenye umati mkubwa wa watu walioitikia kilio cha Toto waliamua kumhasi papo hapo. Hasira ilikuwa imewatia wazimu. Mmoja alitoa kisu mfukoni, wengine wakaivuta suruali ya mbakaji iliyokuwa na mabaka ya damu. Alikatwa viungo vilivyomchochea kumbaka mpwa wake. (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 61-62).

Kwa mujibu wa dondoo hili, wapita njia walijaribu kusuluhisha kitendo cha ubakaji dhidi ya watoto kwa kumnyofoa Pakashume ili asikirudie kitendo kile. Pakashume aliponusunuriwa na askari waliokuwa wakipita, alijipata hospitalini. Mle hospitalini alihudumiwa na nesi wawili ambao katika mazungumzo yao wanasikika wakisema kuwa mwanaume yule hawezi kukirudia kitendo kile kwani tena hakuwa na mishale. Nikiwanukuu:

> "Vundemile: Ingawa aliponea chupuchupu daima dawamu atajutia siku ya kuzaliwa kwake. Hatawahi kurudia unyama huo.
> Waridi: Kwa nini?
> Vundemile: Atafumaje na hana mishale"
> (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 56-57).

Kwa mujibu wa vifungu vilivyonukuliwa, mwandishi alidhihirisha kuwa wanajamii wanaweza kulitatua suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kama ilivyo katika "Shetani hana Hatia". Hili linawezekana kwa kushirikiana na kuwanyofoa wale wanaopatwa wakishiriki mapenzi na watoto hasa kwa kuwabaka kama alivyofanyiwa mhusika Pakashume.

### 5.1.6 Mtoto Kutafuta Rafiki wa Kumfaa awapo Mhanga wa Mahaba au Ujauzito

Kumtafuta mtu wa kuzungumza naye wakati wa tatizo ni njia mojawapo ya kupunguza mawazo. Watoto wengi nchini huwa wahanga wa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema bila hiari yao. Kwa mfano wengine ushiriki mahaba kwa kulazimishwa na kubakwa huku wengine wakishiriki bila kujua ni jambo lisilofaa. Mtoto ajipatapo katika hali hii, anahitaji msaada wa kumwonyesha ana thamani tena na kuifanya roho yake kuwa na nafasi ya kuyabeba yaliyomkabili. Pia, anaweza kusaidika kwa kupata mwelekeo bora wa kulitatua lililomkumba. Msaada huu unapokosekana, wengi huchukua hatua zisizofaa.

Waandishi wa kazi teule wameangazia suluhu hii katika kazi zao mbalimbali. Mohammed Khelef katika hadithi ya "Mame Bakari" anapendekeza suluhu hii katika kutatua uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Kwa mfano:

> Alihisi anahitaji kupata msaada wakati ule wa dhiki na ukiwa wake, vinginevyo mambo yangemwelemea. Wala hakupoteza muda zaidi kufikiria mtu ambaye angelimpa msaada huo. Shoga yake wa chanda na pete Sarina alihisi anatosha. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Baadaye kusimuliwa kila jambo lilivyokwenda hadi ikafikia pale lilipo, na hapana shaka, baada ya kulizana na kufutana machozi, Sara na Sarina wakahakikishiana kuubeba mzigo ule kwa gharama yoyote ile (*Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*, 2016, uk 51).

Mfano huu uliodondolewa unamrejelea mtoto Sara. Sara alikuwa mwanafunzi ambaye alipata kubakwa na janadume asilolijua akitoka masomo ya ziada usiku mmoja. Hakuwaharifu wazazi wake kuhusu kutendewa unyama huu kwani aliogopa ukali wa baba yake na pia kutengwa na kufukuzwa nyumbani. Alifika nyumbani akakoga na kujifungia chumbani akilia. Baada ya muda, Sara alikuwa mja mzito uliotokana na ubakaji ule. Alihuzunika sana. Mawazo yalipomsonga sana, alitafuta mtu ambaye angemfaa na kumpa moyo. Alimwendea rafiki yake wa karibu aliyeitwa Sarina kama ilivyonukuliwa ambaye alimsaidia kuyaona maisha kwa wepesi. Dada yake Sarina aliyeitwa Beluwa alikuwa daktari wa uzazi. Kupitia Sarina, Sara aliweza kupata msaada wa kupokea matibabu ya ujauzito kwa Beluwa. Ni kupitia Beluwa pia ambapo wazazi wake Sara waliweza kuyapata yaliyomkumba mwanao na kujukumika katika kugharamia matibabu yake.

Dondoo hili ni ithibati kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema ni tatizo linalohitaji mtu wa kukusikiliza na kukupa msaada unaostahili. Ni baada ya Sara kumpata Sarina ambapo aliona urahisi wa kuubeba ujauzito ule na kujihisi mwepesi tena.

Gichamba, mwandishi wa hadithi ya "Safari ya Maangamizi" ana msimamo huu pia. Pendo alikuwa mwathiriwa wa uhusiano wa kimahaba utotoni. Alibakwa na wanaume watano na kumuacha katika hali mahututi. Aliambukizwa maradhi ya UKIMWI kutokana na kitendo hiki. Hakuwaambia wazazi wake kuhusu lolote lile. Badala yake, aliamua kulipiza kisasi kwa wanaume bila ubaguzi wowote. Alishiriki mapenzi na yeyote aliyetaka mapenzi bila kumpa habari yoyote. Alipokaribia kufa, alimweleza

rafiki yake Farida kuhusu aliyoyapitia kwa kumkabidhi wosia ambao ungesomwa katika mazishi yake ili kuwafahamisha wazazi wake na waombolezaji wengine kilichotokea maishani mwake.

Urafiki kati ya Pendo na Faridi uliwasaidia wengi kujihadhari na mapenzi ya kiholela kupitia wosia uliosomwa pale mazishini. Kupitia wosia huu, waombolezaji walijua kuwa Pendo alibakwa na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na hivyo kuwahadharisha wanajamii kuhusu yanayotendeka katika jamii yao.

### 5.1.7 Watoto wanaokuwa Wajawazito Kurudishwa Shuleni

Watoto wengi wanapokuwa waathiriwa wa uhusiano wa kimahaba utotoni na kuwa wajawazito huacha shule. Hii ni kwa sababu wanapokuwa waja wazito hukemewa na kutengwa na marafiki na jamaa na kuyasahau maisha yao ya masomo. Kwa mfano nchini Tanzania, wasichana laki nane huacha shule kutokana na kuwa na ujauzito kila mwaka na maelfu ya wengine huripotiwa kuwa watoro kwani wakipata mimba hawarudi shuleni tena kwa kuhofia kufukuzwa (HakiElimu, 2011). Nchini Kenya, sababu mojawapo inayochangia watoto wasichana kuacha shule ni ile ya kuwa na ujauzito (Kiarie, 2015). Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni si mwisho wa masomo na maisha ya mtoto msichana. Mtoto anapaswa kupewa nafasi ya kuendeleza masomo yake na kutimiza ndoto zake za maisha. Hili linaungwa mkono na wizara ya elimu ambalo baada ya kipindi kirefu cha kuzuka kwa ugonjwa wa korana nchini na shule zote kufungwa, watoto wengi walikuwa wahanga wa mimba za mapema. Wizara hii iliagiza watoto wote kuruhusiwa kurudi shuleni, walio na watoto na pia waja wazito (Kazungu na Atieno, 2021).

Waandishi wa kazi teule wana suluhu ya kurudi shule kama mojawapo ya njia ya kukabiliana na uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema. Mwandishi Rhoda Nyaga ana haya katika hadithi yake “Kanda la Usufi”:

> “Shule ilipopatikana, Sela alihudhuria masomo hadi pale ilishindikana; siku zake za kujifungua zilipokaribia” (*Damu nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 63)

Anayerejelewa katika kifungu hiki ni Sela ambaye alikuwa mjamzito alipokuwa anaanza masomo ya kidato cha tatu. Ujauzito huu ulitokana na uhusiano wa kimahaba

kati yake na rafiki yake wa kiume Masazu ambaye alikuwa mwanafunzi pia. Alipogundulika pale shuleni kuwa alikuwa mjamzito, wazazi wake walishauriwa na mwalimu mkuu wampeleke shule ya kutwa iliyokuwa na nyumbani. Sela aliendeleza masomo yake katika shule ya kutwa hadi wakati alienda kujifungua. Isitoshe, baada ya kumpata mtoto alimlea kwa miezi michache na kumwacha mikononi mwa harati yake Rozina ili arudi kuendeleza masomo yake ya shule ya sekondari. Kwa mfano:

> "Rozina ndiye alikuwa mlezi wake katika kipindi ambacho mama yake Kadogo alirudi kuendelea na masomo yake na baadaye Sela alipomaliza masomo ya shule ya upili na kuenda kuishi na Masazu" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, Uk 63)

Kwa mujibu wa mwandishi huyu, mimba za mapema zinafaa kukabilianwa nazo kwa kumpa mtoto nafasi ya kuendeleza masomo yake. Hatua hii itasaidia kupunguza idadi ya watoto wa kike wanaoacha shule kila mwaka kutokana na kuwa na ujauzito wangali shuleni.

### 5.1.8 Wanaoshiriki Mahaba na Watoto Wakanunue Mapenzi kwa Makahaba

Nchini, kuna makahaba ambao ni watu wazima na hupata kipato chao cha siku kupitia kuiuza miili yao. Ingawa biashara hii hairuhusiwi kisheria, imekuwa njia ya kujipa kipato kwa wengi. Pia, imesaidia walio na nia ya kushiriki mahaba bila kuwadhuru watoto. Hivyo, kununua mapenzi kwa watu wazima ni mojawapo ya njia ya kuzuia uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwa mujibu wa hadithi fupi teule.

Bitugi Matundura ana msimamo huu kupitia wahusika wa hadithi yake "Shetani hana Hatia". Pakashume alikuwa mpwa wake Toto. Alipewa kazi pale kwao ya kuwa shambaboi. Isitoshe, aliongezewa jukumu la kumchukua mpwa huyu kutoka shule ya chekechea iliyokuwa karibu na nyumbani. Siku moja Pakashume aliingiwa na unyama fulani walipokuwa njiani wakielekea nyumbani na kumbaka malaika huyu. Toto aliokolewa na wapita njia ambao walimwadhibu Pakashume vikali. Punde, askari walitokea na kumchukua Pakashume ambaye alikuwa katika hali mbaya na kumpeleka hospitali kwa ulinzi mkali. Mle hospitalini, nesi walitaka kujua kilichomsababisha Pakashume kumbaka mtoto yule mdogo. Kwa maswali hayo yote Pakashume alikuwa akimsingizia shetani kuwa kamjaribu. Nesi mmoja aliyeiwa Vundemile alikuwa na haya ya kumwambia:

> "Mwanaume mzima wewe na akili zako unageuka mnyama na kuyatenda haya-huna soni? Katili mkubwa we! Mbona hukwenda Koinange au Majengo ukanunua mapenzi-kuna hata na ya mbao ati! Uliwamaliza makahaba wote wa jiji hili ndiposa ukawageukia watoto?" (*Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 57-58)

Kupitia dondoo hili, Mwandishi ana msimamo kuwa wanaoshiriki mahaba na watoto waache tabia ile. Iwapo ni lazima, basi waweze kuzituliza hisia zao na makahaba ambao wamejitolea kufanya kazi hiyo na wala si watoto. Anaeleza kuwa kuna mapenzi kwa makahaba ambayo si ya bei ghali kwani kuna hata ya ishirini kama ilivyo kwenye kifungu. Kulingana na kazi hii teule, mojawapo ya njia za kukomesha uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema ni kupitia kuyanunua mapenzi kwa watu wazima katika mitaa ya makahaba.

### 5.1.9 Watoto Wanaodhulumiwa Kimapenzi Wapate Fidia

Pesa na mali vimetumika kwa muda kama njia ya kutolea fidia kwa watu mbalimbali nchini. Dhamana ya fidia imepunguza maovu mengi katika jamii kwani wengi huogopa kuilipa. Kwa mfano, wanaoshiriki uhusiano wa kimahaba na watoto wanaweza kutozwa faini ambayo ni ghali kiwango cha kutorudia kosa lile tena.

Kristina Mwende Mbai katika hadithi yake "Mwana wa Darubini" anahimiza hoja hii**.** Mwatela alikuwa bwana yake Maria. Familia hii ilimwajiri kijakazi aliyeitwa Kananda. Kananda alikuwa mtoto ambaye hakuwa shuleni kutokana na umaskini wa wazazi wake. Siku moja Maria alienda kuwatembelea wazazi wake walioishi mbali na jiji. Mwatela alipobaki nyumbani, alimnajisi kijakazi wao kitendo kilichomfanya kuwa mja mzito. Kananda alipomjulisha Mwatela kuhusu hali yake, alimwambia kuwa aiweke kuwa siri na asimwambie Maria kwani angemuona kama bibi wa pili mara tu akijifungua. Hata hivyo, mambo yalikuwa tofauti na matarajio ya Kananda. Alipojifungua na kurudi nyumbani, Maria alikimbizwa hospitali kutokana na mkasa wa moto. Mwatela alichukua nafasi hii kumuuza Kananda kwa dereva wa malori ya shehena kutoka Congo baada ya kumnyang'anya mtoto. Kananda aliteseka sana kule ambapo mwishowe alirudi Kenya kupitia usaidizi wa askofu mzungu. Alikuwa na wakati mgumu kumtafuta alikokuwa mwanawe Mwakitawa.

Kupitia usaidizi wa wazaziwe na marafiki aliweza kupata darubini aliyoitumia kumtazama mwanawe kutoka nyumbani mwa Mwatela kwani asingeenda pale kwa sababu ya kuujali usalama wake. Mwatela alipopata ujumbe kuwa kuna mtu anaonekana akitazama kwake kwa darubini, alipatwa na wasiwasi kuhofia kuwa ni mama yake Mwakitawa. Alimtahadharisha Mwakitawa kwa kumpa manati ya kumlenga yeyote aliyemshuku. Siku moja Kananda alienda na darubini yake kama kawaida kumtazama mwanawe. Hapo ndipo Mwakitawa alimlenga kwa jiwe kichwani na kumwangusha chini. Wapita njia walisaidia kumfikisha hospitalini. Mwakitawa alisubiri kupongezwa kwa kitendo chake lakini baba yake alionyesha wasiwasi mwingi. Mwakitawa alipogundua alikuwa anamuua mama yake mzazi kupitia ubishi wa Mwatela na bibiye Maria alitoroka nyumbani na kuapa kutorudi huko tena. Wakati huu wote, Mwatela alijutia sana. Kananda alipotoka hospitali Mwatela alifanya yafuatayo:

> Mwatela alimkimbilia wakili wake akiwa amemwandikia Kananda barua ya kumuomba msamaha. Alikuwa amefikiria jinsi angemlipa Kananda kwa maovu aliyomfanyia. Aliamua kumpa Kananda ile nyumba ya kifahari. Alitaka wakili wake amwakilishe katika kumtafuta Kananda na kukamilisha malipo hayo ya kuomba msamaha. Alitaka Kananda atie sahili makubaliano hayo yote. (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 107)

Mwatela alikuwa na haya ya kusema;

> "Nimebaini nimekosa mwisho wa kukosa. Dhambi zangu ni nyingi na sitaki ziniandame kaburini. Nakukabadhi mwanao. Gharama ya kufanya hivyo itakuwa maumivu moyoni mwangu milele. Kananda, kumbe maisha ni fumbo!" (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 108)

Mwishowe Kananda alikubali malipo ya Mwatela ya kukabidhiwa mwanawe na kupewa jumba la kifahari ambalo angeishi pamoja na mwanawe kama inavyonukuliwa:

> "Kananda alikubali malipo ya Benjamin Mwatela"
> (*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, 2007, uk 108)

Nukuu hizi zinaonyesha njia ambazo Mwatela alizitumia kumfidia Kananda kwa makosa aliyokuwa amemtendea. Kwanza, alimkabidhi mwanawe Mwakitawa ambaye alikuwa ametenganishwa na upendo wa mama yake. Pili, Kananda alipewa nyumba ya kifahari ambayo aliweza kuishi na wanawe. Masomo ya Mwakitawa yalishughulikiwa na Mwatela pia. Kwa mfano:

> “Benjamin Mwatela alijitolea kumuelimisha Mwakitawa mpaka afike alikotaka. Alitenga mali ya kumsaidia Kananda mpaka atakapoweza kujikimu. Mwakitawa hakurudi kuishi na baba yake” Uk 108.

Dondoo zilizonukuliwa zinadhihirisha kuwa uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema zinaweza kuzuiliwa au kupunguzwa kupitia kuwatoza faini wanaoshirikisha watoto mahaba haya. Kupewa adhabu ya kugharamia watoto hawa pamoja na wanao pia ni fidia itakayosaidia kutatua tatizo hili.

## 5.2 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alichunguza jinsi waandishi wa hadithi fupi teule yalivyoliangalia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni na kutoa suluhu kwa jambo hili. Imedhihirika kuwa wanajamii kwa ushirikiano na serikali wanaweza kulitatua suala hili ambalo limewaangaisha wanajamii kwa muda. Waandishi wote wa kike na wa kiume wanaunga mkono kukomeshwa kwa uhusiano wa kimahaba miongoni mwa watoto jambo ambalo litachangia pakubwa katika kukabiliana na mimba za mapema nchini.

Imebainika kuwa kupitishwa kwa sheria itakayotoa adhabu kali kwa wanaoshiriki mahaba na watoto, ushirikiano wa wanajamii katika kuwaadhibu wanaoshiriki mapenzi na watoto, kutolewa kwa elimu kuhusu dhidi ya kujikinga, kuwaadilisha watoto vifaavyo, kutafuta rafiki wa kukufaa, kurudishwa shuleni na kununua mapenzi kwa watu wazima ni baadhi ya njia za kusuluhisha na kukomesha uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Imekuwa dhahiri kuwa wanajamii wana jukumu katika kulitatua tatizo hili kabisa.

Katika sura ifuatayo, mtafiti aliangalia mahitimisho ya utafiti huu. Hapa, muhtasari wa kila sura ulitolewa pamoja na matokeo ya utafiti. Mapendekezo ya tafiti za baadaye pia yalitolewa.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa yale ambayo yalishughulikiwa katika tasnifu hii. Pia inaonyesha matokeo ya utafiti huu kulingana na maswali na madhumuni ya utafiti yaliyotolewa. Isitoshe, mapendekezo ya tafiti za baadaye yametolewa.

## 6.2 Muhtasari

Utafiti huu ulishughulikia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Hadithi teule zilipatikana katika diwani za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007), *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine* (2007), na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza chanzo au visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni, kuchunguza athari za uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni pamoja na kuonyesha maoni ya waandishi wa kazi teule kuhusu suluhu za uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema.

Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa kuwahamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa fasihi ya Kiswahili ikiwemo kumulika yanayotendeka katika jamii pana. Vilevile, waandishi wa fasihi watanufaika na utafiti huu kwa kuwawezesha kutambua masuala ibuka na masuala nyeti katika jamii. Waandishi hawa watahamasishwa pia kuhusu nafasi ya fasihi kama chombo cha kuyafichua maovu yanayoiathiri jamii na kupendekeza suluhu. Pia, ulikuwa unatoa mchango katika mijadala ya kijamii kuhusu suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Isitoshe, ulikuwa wenye manufaa kwa watetezi wa haki za watoto nchini na kimataifa kuwasaidia kuelewa mchango wa fasihi ya Kiswahili kuhusu visababishi, athari na hata suluhu kwa uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kama ilivyosawiriwa na waandishi wa kazi teule za Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktabani ambapo mtafiti alisoma hadithi fupi teule ili kupata data iliyochanganuliwa.

Mtafiti aliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ambayo waasisi na watetezi wake wakuu ni pamoja na; Wolfgang Iser (1974,1978), Stanley Fish (1980) na Jane Tompkins (1980). Nadharia hii humweka msomaji katikati ya uhakiki wa fasihi na

hujihusisha na namna kazi za kifasihi hupokelewa na wasomaji katika wakati fulani kwa kuangalia athari inazozua kwa msomaji katika kipindi maalum. Kazi teule zilihusishwa na wakati huu ambapo suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni limezidi kuongezeka na athari zake kuwaathiri wanajamii kwa kiwango kikubwa. Uchanganuzi wa data uliegemezwa katika madhumuni ya utafiti ili kubaini mtazamo wa waandishi wa kazi teule kuhusu suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema.

**6.3 Hitimisho**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza vile waandishi wa hadithi fupi teule za Kiswahili wameangazia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ili kubaini chanzo chake, athari zake kwa wanajamii na pia suluhu kwa suala hili. Kupitia ukusanyaji na pia uchanganuzi wa data imekuwa bayana kuwa fasihi ya Kiswahili hasa utanzu wa hadithi fupi ni nyenzo ya kuangazia masuala yanayotendeka katika jamii pana pakiwemo suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Waandishi wa hadithi fupi teule wamebaini suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kama suala nyeti nchini na hata ulimwenguni kutokana na athari zake kwa wanajamii. Waandishi hawa wamelishughulikia tatizo hili kwa kuangazia visababishi vyake, athari zake na pia suluhu ya tatizo hili. Ilibainika kuwa visababishi vya uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni pamoja na ubakaji, kutowajibika kwa wazazi na walezi, shinikizo la wanarika, ukiukaji wa maadili, nia ya kulipiza kisasi, kukidhi mahitaji ya kila siku miongoni mwa visababishi vingine. Uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni huwa na athari kama vile kusababisha kifo, kuwa na ujauzito usiotarajiwa, unyanyapaa, kujiingiza katika ndoa za mapema, kuacha shule na kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema linaweza kusuluhishwa na wanajamii kupitia kuwasaidia watoto wanaodhulumiwa kimapenzi na kuwaadhibu wanaowanyanyasa, kuwaadilisha watoto ifaavyo, kuwaelimisha watoto namna za kujikinga na mimba za utotoni miongoni mwa suluhu nyinginezo.

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, imebainika kuwa utanzu wa hadithi fupi ni nyenzo muhimu katika kuyamulika maovu yanayotendeka katika jamii na kutoa suluhu

mwafaka kwa maovu hayo. Ilibainika kuwa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni inatokana na wanajamii wenyewe na suluhu yake pia imo mikononi mwa wanajamii hao.

### 6.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu ulijihusisha katika uchunguzi wa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni. Kwa kuwa suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni ni suala nyeti ambalo limekuwepo na linaendelea kuwasumbua wanajamii nchini na ulimwenguni kutokana na athari zake, mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe katika tanzu zingine za fasihi kama vile riwaya, tamthilia na ushairi. Tafiti hizi zitabaini jinsi waandishi wa kazi hizo wameangazia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni kwani utafiti huu ulijikita kwenye utanzu wa hadithi fupi.

Vilevile, kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa kimaktabani. Utafiti wa nyanjani unaweza kufanywa ili kupima ukweli wa yale ambayo yameandikwa na waandishi wa hadithi fupi zilizotumiwa katika utafiti huu. Utafiti huu utasaidia kuonyesha iwapo kuna uhusiano wa matokeo ya maktabani na yale ya nyanjani kuhusu suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji iliyompa mtafiti uhuru wa kufasiri matini ya mwandishi na kuibua maana mpya kutoka kwayo kutegemea mazingira anamoishi, tajriba aliyo nayo na hata wakati wa matumizi ya matini yale. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za mapema kwa kuongozwa na nadharia tofauti.

Hali kadhalika, utafiti huu ulikuwa wa fasihi ya Kiswahili. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika fasihi ya Kiingereza hasa katika utanzu wa hadithi fupi ili kubaini jinsi waandishi wake wameangazia suala la uhusiano wa kimahaba na mimba za utotoni.

## MAREJELEO


APHRC. (2020, June 17). *The Potential Impacts of covid-19 on-Teenage Pregnancy in Kenya.* Imechukuliwa toka https://aphrc.org/blogarticle/the-potential-impacts-of-covid-19-on-teenage-pregnancy-in-kenya/.

Atieno, W. (2019, Machi 1). *Wazazi Wamevumbua Mbinu ya Kukabiliana na Mimba za Mapema*. Imechukuliwa toka https://taifaleo.co.ke/?p=18831.

Burke, C. (1999) *Covenanted Happiness, Love and Commitment in Marriage,* 2nd Ed. New Jersey: Screptree Publishers

CDF & FORWARD. (2018). *Utafiti Shiriki Kuhusu Mimba na kuwa Mama katika Umri Mdogo Uliofanyika Wilaya ya Mpwapwa.* Tanzania: CDF & FORWARD.

Chokocho, A., & Kayanda, D (Wah). (2016). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Fish, S. (1980). *Is There a Text in This Class? The Authority of Interpretive communities.* Cambridge: Havard University Press.

Greenblatt, S. (1980). *Renaissance Self Fashioning.* Chicago: University of Chicago Press.

HakiElimu. (2011). *Watoto wetu Waendelee na Masomo baada ya Kujifungua: Watanufaika wao wenyewe, watoto wao na jamii.* Dar es salaam: HakiElimu.

Human Right Watch. (2016). *Nilikuwa na ndoto ya kumaliza shule.* Tanzania: Human Right Watch.

Iribemwangi, P. (Mh). (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Kavuria, P. (2008). *Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya za Kiswahili*. (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kazungu, K. & Atieno, W. 'Wanafunzi wajawazito wasakwa na serikali' Taifa Leo, Januari 6, uk 4.

Kiarie, K. (2015). *Factors Influencing Teenage Pregnancy in Public Secondary Schools in Imenti North Sub-county Meru County Kenya.* (Unipublished M.A Project Report). University of Nairobi.

Matheka, B. (2018, Novemba 8). *Ripoti yafichua maeneo wanafunzi hupata mimba*. Imechukuliwa toka https://taifaleo.nation.co.ke/?p=13118.

Maundu, P. (2020, June 17). *Alarm as 3964 girls Impregnated in Machakos County in Five Months.* Imechukuliwa toka https://www.nation.co.ke>DailyNation >counties >Machakos.

Mayieka, M. (2015). *Masuala Ibuka katika Riwaya za Kisasa; Kidagaa Kimemwozea na Mhanga Nafsi yangu.* (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mbatiah, M. (Mh). (2007). *Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Mkota, A. (2009). *Kamusi ya Methali; Maana na Matumizi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

M'Ngaruthi, T.K (2019). Vijana na Mshikamano wa Kitaifa: Mchango wa Hadithi Fupi ya Kiswahili. Katika Kobia, J., Kandagor. M., na Mwita, L.C., *Lugha na Fasihi katika Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika.* Eldoret: Moi University Press (uk. 175-182).

Mokou, H. (2020). 'Uhusiano wa kimapenzi utayeyusha umakinifu wako masomoni' Taifa Leo, Februari 12, uk 13

Munene, G. (2021). 'Pasta akiri kuwapachika mabinti wake wawili mimba'. Taifa Leo, Januari 6, uk 1-2

Murfin, R. (1991). *Case Studies in Contemporary Criticism.* New York: St Martins Press.

Mutheu, D. (2020). ' Wataka mimba za mapema zikabiliwe'. Taifa Leo, Februari 28, uk 5

Mwenda, M. (2018). *Uwasilishaji wa Maudhui katika Hadithi Fupi teule za Said, A Mohamed.* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwende, M. (2020) 'Mimba zimeongezeka kwa wasichana wadogo-ripoti'. Taifa Leo, Machi 6, uk 4

Naliaka, R. (2012) Uhakiki wa Hali ya Vijana katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Namlola, J. (2020, Juni 23). *Serikali yakiri corona inachangia mimba za mapema*. Imechukuliwa toka https://taifaleo.nation.co.ke/?p=54511.

NCCK. (2019). *Our Presentation to the Senate on High Rates of Teenage Pregnancies.* Nairobi: NCCK.

Njeru, K. (2018). *Suala la Ardhi katika Riwaya teule za Kiswahili: Tathmini ya Kovu Moyoni na Kufa Kuzikana.* (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Chuka, Chuka.

Njogu, K. (1997) *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntiba, G. (2011). *Taathira ya Dhamira kwa Mtindo katika Hadithi Fupi Teule za Kiswahili.* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyaberi, W. (2020). ' Wanafunzi waliokosa kurudi shuleni wasakwa na machifu'. Taifa Leo, Oktoba 15, uk 3.

Nyamasege, W. (2018, Novemba 1). *Gov't Alarmed by High Rate of Teenage Pregnancies in Primary Schools*. Imechukuliwa toka https://citizentv.co.ke /news/govt-alarmed-by-high-rate-of-teenage-pregnancies-in-primary-schools.

Ojamaa, B. (2020) 'Mwalimu Anayedaiwa Kunajisi Mwanafunzi nje kwa Dhamana' Taifa Leo, Februari 14, uk 5

Ominde, T. na Chepkemboi, J. (2020). 'Wanaume Watatu Kizimbani kwa Madai Kunajisi Watoto'. Taifa Leo, Januari 25, uk 5.

Ondieki, F. (2015). *Usawiri wa Watoto katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili Zilizoandikwa na Mohamed Suleiman na Euphrase Kezilahabi.*(Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro.

Pettifor, A.E, Rees, h.V., Kleinschmidt, I.,Steffeson, A.E., Macphail, C., Hlongwa-madikizela, L., Vermaak, K. and Padian, N.S. (2005). Young peoples sexual health in South africa: HIV Prevelance and Sexual Behaviours from a Nationally Representative Household Survey. AIDS, 19, 1525-1534.

Republic of Kenya. (2010). *Constitution of Kenya.* Nairobi: Government Printer.

Rono, P. (2013). *Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea.* (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Ruto, M. (2015). *Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso ya Mwanamke.* (Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Sayagie, G. (2020). 'Walimu Waombwa Watambue Wasichana Walio nje ya Shule'. Taifa Leo, Januari 8, uk 5

Tompkin, J. (1980). *Reader Response Criticism.* Baltimore and London: John Hopkins.

UNESCO. (2017). *Early and Unintended Pregnancy and Education Sector; Evidence Review and Recommedations.* Paris: UNESCO.

UNFPA & UN. (2013). *Adolescent Pregnancy: A Review of the Evidence.* New York: UNFPA & UN.

UNFPA. (2017). *UNFPA Kenya Annual Report 2017.* New York: UNFPA.

UNICEF. (2017). *State of the World's Children 2017.* New York: UNICEF.

________ (2017). *UNICEF Report 2017.* New York: UNICEF.

Wafula, R & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* . Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K & Mohamed, S.A (wah). (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Moran (E.A) Publishers Limited.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi; Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited

Wanjala, J. (2015). *Usawiri wa Malezi Unavyoathiri Utambulisho wa Vijana katika Riwaya ya Kiswahili; Anasa na Asali Chungu.* (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Wasonga, C. (2018, Novemba 9). *Wabunge kuchunguza mimba za mapema*. Imechukuliwa toka https:/taifaleo.nation.co.ke/?p=13125.

WHO. (2011). *Preventing Early Pregnancy and Reproductive Outcomes among Adolescents in Developing Countries.* Geneva: WHO.

WHO. (2013). *Global and regional estimates on violence against women: Prevalence and health effects of intimate partner violence and non-partner sexual violence.* Geneva: WHO.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Idhini ya Utafiti

**THARAKA UNIVERSITY COLLEGE**
P.O BOX 193-60215,
MARIMANTI, KENYA

Telephone :|+(254)-0202008549,
+(254)-02020076920
email: info@tharaka.ac.ke
Website: https://www.tharaka.ac.ke

***(A Constituent College of Chuka University)***

**OFFICE OF THE DIRECTOR**
**BOARD OF POST-GRADUATE STUDIES**

---

**Our Ref/ TUC/BPGS/26/11/2020**

11th November, 2020

**TO WHOM IT MAY CONCERN.**

Dear Sir/ Madam,

**Introductory Letter**

**Name:** Joyce Karimi **Reg. No.** AM12/29221/17.

The above named is our postgraduate student undertaking a Masters' degree Programme **(M.A) in Kiswahili**. The student has finished course work and is expected to collect data. The title of the research is *"SUALA LA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI KATIKA HADITHI FUPI TEULE ZA KISWAHILI"*. The study will be conducted in **SELECTED UNIVERSITY LIBRARIES**.

The candidate has defended the proposal successfully at the faculty and has submitted the required number of corrected copies to the Office of the Director, Postgraduate Studies. The candidate is expected to begin collecting data, analyse and write a report on the findings. This is expected to take twelve (12) months (November 2020 to November 2021). The proposal has passed the University Ethics Review Committee requirements.

Any assistance accorded to her will be highly appreciated. Thank you in advance.

Yours faithfully,

Dr. Kiptui David Kipkorir Ph. D
**Director**
**Board of Postgraduate Studies**
**cc.**
**1. The Principal/ CEO**
**2. Deputy Principal (ARSA)**
**3. Registrar (AA)**

THARAKA UNIVERSITY COLLEGE
BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES AND RESEARCH
26 NOV 2020
DIRECTOR
P.O.Box 193 - 60215, MARIMANTI

**Kiambatisho 2: Kibali cha Utafiti**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 130401

Date of Issue: 02/December/2020

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. joyce karimi of Chuka University, has been licensed to conduct research in Tharaka-Nithi on the topic: SUALA LA UHUSIANO WA KIMAHABA NA MIMBA ZA UTOTONI KATIKA HADITHI FUPI ZA KISWAHILI for the period ending : 02/December/2021.**

License No: **NACOSTI/P/20/8074**

**130401**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.